Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA TANO

**Kikao cha Pili - Tarehe 14 Aprili, 2004**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

## D U A

*Spika (Mhe. Pius Msekwa) Alisoma Dua*

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Taarifa ya Mwaka na Hesabu zilizokaguliwa za Bodi ya Pareto Tanzania kwa Mwaka ulioishia Tarehe 30 Juni, 2003 *(The Annual Report and Audited Accounts of the Tanzania Pyrethrum Board for the Year ended 30th June, 2003).*

Taarifa ya Mwaka na Hesabu za Taasisi ya Utafiti wa Wadudu Waharibifu wa Ki-Tropiki kwa Mwaka ulioishia Tarehe 30 Juni, 2002 *(The Annual Report and Accounts of the Tropical Pesticides Research Institute for the Year ended 30th June, 2002).*

**SPIKA:** Ninapenda kuwajulisha Wenyeviti wa Kamati za Kudumu kwamba, Taarifa zao zitawasilishwa Mezani kesho na keshokutwa, nusu ya Wenyeviti watawasilisha kesho nusu iliyobaki watawasilisha keshokutwa Ijumaa, bora wajiandae. Tunaendelea na *agenda* inayofuata Katibu.

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 15

**Matatizo mbalimbali katika Zahanati na Vituo vya Afya Nchini**

**MHE. JOEL N. BENDERA** aliuliza:-

Kwa kuwa wananchi wengi vijijini wanategemea kupata matibabu mbalimbali katika zahanati na vituo vya afya na kwa kuwa zahanati na vituo hivyo vya afya vina matatizo mbalimbali kama yale ya ukosefu wa Wataalam wa kutosha kama vile Madaktari, Wakunga, vifaa vya kisasa vya kupimia wagonjwa, maabara na kadhalika kiasi cha kufanya huduma zinazotolewa kutoridhisha kulingana na dunia ya leo, kwa mfano, kwa zaidi ya miaka kumi sasa wananchi wamejenga maabara katika Kituo cha Afya cha Magoma kwa nguvu zao wenyewe wakisaidiana na *World Vision,* lakini hadi leo hii maabara hiyo haitumiki kwa sababu ya kukosa mtaalam wa maabara na kwa sababu hiyo Tarafa ya Magoma imepoteza watoto wengi sana kwa kukosa damu na magonjwa ya malaria kiasi kwamba kama kungelikuwa na maabara watoto hao wangepatiwa vipimo muhimu ili kubaini matatizo yao na kupatiwa matibabu sahihi:-

(a) Je, Serikali haioni kuwa kuna umuhimu wa haraka wa kukisaidia kituo hicho kwa kupeleka mtaalam wa maabara na wataalam wengine kama Madaktari, Wakunga hasa baada ya juhudi za Halmashauri kushindikana kwa muda mrefu ili kuokoa maisha ya watoto wengi wanaopoteza maisha?

(b) Je, Serikali haioni kwamba huu ni wakati wa kuviimarisha vituo vyetu vya afya na zahanati zetu kote nchini kwa kuzipatia vifaa vya kisasa na wataalam ili viendane na ulimwengu wa sasa wa sayansi na teknolojia?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Joel Bendera, Mbunge wa Korogwe Mashariki, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, napenda kuwapongeza na kuwashukuru wananchi wa eneo la Magoma pamoja na Shirika la *World Vision,* kwa kuamua kujenga maabara katika Kituo cha Afya cha Magoma, Maabara hiyo imekamilika katika mwaka wa fedha wa 2002/2003 na sio miaka kumi iliyopita kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Spika, kwa hivi sasa Kituo cha Afya cha Magoma kina idadi ya watumishi wapatao 21 kati ya 29 wanaohitajika. Hivyo, kituo kinao upungufu wa watumishi 8 ikiwa ni pamoja na mtumishi wa maabara. Vile vile, Kituo cha Magoma kinavyo baadhi ya vifaa vya kisasa vya maabara kama vile Darubini 3, *BP Machine* 3,

*Stellescopes* 3, *Sterelizer* 3, *Pressure Cooker* 2, *Stove* 7, *Examination Coach* 4, *Fridge* 1, *Weighing Scale*, Mikasi, *Forceps* na *Sunction Machine.* Kutokana na umuhimu wa kukisaidia Kituo cha Afya cha Magoma na vituo vingine Wilayani Korogwe, katika mwaka wa fedha wa 2003/2004, Halmashauri ya Korogwe imeomba kibali cha kuajiri watumishi wa Afya 56 wakiwemo wataalamu wanne wa Maabara ambapo mmoja kati yao atapelekwa katika Kituo cha Magoma. Kwa hivi sasa mtumishi mmoja wa kituo hicho ameteuliwa kupatiwa mafunzo ya maabara katika Hospitali ya Wilaya. Aidha, kupitia programu ya Mfuko wa pamoja wa Afya, Serikali inaendelea kuvipatia Vituo vya Afya na Zahanati zote nchini baadhi ya vifaa na madawa muhimu yanayohitajika.

Mheshimiwa Spika, Serikali ilikwishatambua umuhimu wa kuimarisha huduma zitolewazo na zahanati, vituo vya afya na hospitali za Wilaya na Mikoa mara baada ya kupata uhuru mwaka 1961. Hivyo, kupitia ruzuku na misaada ya wahisani kama vile *UNICEF* na Programu ya Mfuko wa pamoja wa Afya, Serikali imefanya juhudi kubwa ya kuimarisha vituo vya afya na zahanati nchini. Kazi kubwa iliyofanyika ni ukarabati wa majengo yaliyopo, ujenzi wa majengo mapya, kuendesha mafunzo mbalimbali kwa wataalamu wa afya na vile vile kuvipatia vituo vya afya na zahanati vifaa muhimu na vya kisasa vinavyohitaika. Napenda kutumia furusa hii kuwashukuru wahisani wote waliosaidia kuimarisha vituo na zahanati hizo. Aidha, Serikali itaendelea kuzihimiza Halmashauri kujaza mapengo ya watumishi yaliyopo kwa kuzingatia taratibu zilizowekwa na kulingana na uwezo wa Serikali wa kifedha.

**MHE. JOEL N. BENDERA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu yenye matumaini. Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri ameshatamka kwamba, mtaalam wa maabara atapatikana katika kipindi hiki cha mwaka 2003/2004 na sasa hivi hakuna mtaalam pale sehemu kama nilivyosema ni sehemu ambayo ina matatizo sana, ndiyo Tarafa inayotegemewa. Je, Serikali haioni tukiwa tunawasubiri tukapata angalau kwa haraka mmoja wa wataalam hao ili angalau waokoe hali iliyopo pale?

Pili, kutokana na hali halisi iliyojitokeza kwamba Zahanati nyingi nchini na Vituo vya Afya ndiyo tegemeo lakini upo ukosefu mkubwa wa Madaktari. Je, Serikali haioni kwamba ingefanya mpango kama wa MMEM wa kuwa na *Crash Programme* ya kufyatua madaktari wengi ili Zahanati nyingi ziweze kupata wataalam hao katika nchi yetu?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, nimeeleza hapa kwamba, tunao utaratibu huu wa kupata watalaam ambao tunatumaini watapatikana kwa ajili ya kuajiriwa kama taratibu zinavyozingatia, lakini tumesema vile vile kwamba, tumepeleka mtalaam mmoja Wilayani kwa ajili ya kupata hiyo *training* ili kwa muda huu wakati tunasubiri huo ufumbuzi wa kudumu aweze kusaidia. Kwa hiyo, mimi nafikiri tufanye subira, nina hakika tutapata huyo mtalaam baada ya muda si mrefu.

Kuhusu swali la pili, nakubali kabisa kwamba ni kweli kabisa Zahanati na Vituo vya Afya ndivyo kwa sehemu kubwa vinavyotoa huduma kwa wananchi walioko katika ngazi ya chini na ambao ndiyo wengi. Lakini kama ambavyo tumekuwa tukieleza muda

wote, tatizo la upungufu wa wataalam ni ni kubwa na ni la Kitaifa na si kwamba labda Serikali inazembea. Lakini rai yake kwamba labda tuwe na mpango kamambe kama ule wa MMEM kwa maana ya *training* kwa upande wa wataalam ni jambo jema lakini nalo linahitaji vile vile kutazamwa kwa kina kwa sababu lina gharama zake ambazo itabidi kuzitazama. Lakini kwa sababu *training* iko chini ya Wizara ya Afya, tutawasilisha jambo hili kwao waone uwezekano wa kulifanya.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali dogo la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina swali la nyongeza.

Kwa kuwa darubini ni muhimu sana katika kuchunguza magonjwa na kwa kuwa katika Zahanati nyingi hakuna darubini hivyo inakuwa ni vigumu kwa waganga kutambua magonjwa kama vile malaria. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri atakubaliana nami kwamba iko haja ya kuweka mikakati ya kusambaza darubini katika zahati zote hapa nchini?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa kwamba darubini ni kifaa muhimu sana sana katika sekta ya afya hasa kwa ajili ya kutambua magonjwa mbalimbali yakiwemo malaria. Vituo vingi vya Afya hata vya Zahanati bado havina vifaa hivyo kwa namna ambayo wote tungeweza tukaridhika. Lakini tuliwahi kueleza siku za nyuma hapa kwamba, kuwa na vifaa hivi ni jambo moja lakini tatizo tunalokuwa nalo zaidi ni kwa sababu hatuna wataalam wa kutosha kwenye maabara.

Lakini vile vile tulieleza kwamba, kwa *training* wanazopata madaktari ambao wako katika vituo vya afya wamewezeshwa vile vile kuweza kutambua magonjwa ambayo yanajidhihirisha wazi wazi kama malaria kwa utaratibu wa kawaida wakati utaratibu wa kudumu unatafutwa kwa maana ya vifaa pamoja na wataalam wake.

Na. 16

**Barabara ya Mabuki - Maswa**

**MHE. JACOB D. SHIBILITI (k.n.y. MHE. ESTHER K. NYAWAZWA)** aliuliza:-

Kwa kuwa hali mbaya ya barabara ya Mabuki - Jojiro - Ngudu -Igoma - Kimiza - Malya - Malampaka - Maswa imekuwa ni kero kwa wananchi wanaoishi maeneo hayo:-

(a) Je, Serikali itakubaliana nami kwamba kutoifanyia matengenezo barabara hiyo kunaathiri kwa kiwango kikubwa biashara kwa Wilaya za Misungwi, Kwimba na Maswa?

(b) Je, ni lini barabara hiyo itatengenezwa kwa kiwango cha lami au changarawe ili kupunguza kero kwa wakazi wa maeneo hayo?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Esther Nyawazwa, Mbunge Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali inakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba, kutoifanyia matengenezo barabara ya Mabuki-Jojiro-Ngudu-Igoma-Kimiza-Malya-Malampaka na Maswa, kutaathiri shughuli za kibiashara kwa Wilaya za Misungwi, Kwimba na Maswa.

(b) Mheshimiwa Spika, barabara ya Mabuki-Jojiro-Ngudu-Igoma-Malampaka hadi Maswa inahudumiwa na Wizara yangu na inapita katika Mikoa ya Mwanza na Shinyanga. Maeneo yaliyoko Mkoa wa Mwanza ni Mabuki-Jojiro-Ngudu-Igoma hadi Malya na yale ya Mkoa wa Shinyanga ni Malya, Malampaka hadi Maswa. Kwa upande wa Mkoa wa Mwanza, Wizara yangu kupitia Wakala wa Barabara Mkoa wa Mwanza, imekuwa ikiifanyia ukarabati barabara hii kama ifuatavyo:-

Katika mwaka wa fedha 2002/2003, sehemu ya Mabuki hadi Jojiro yenye urefu wa kilomita 10 ilifanyiwa ukarabati kwa gharama ya shilingi milioni 100. Katika mwaka huu wa fedha wa 2003/2004, sehemu ya Jojiro hadi Malya kilomita 6 imefanyiwa ukarabati kwa gharama ya shilingi milioni 59. Ukarabati kwa sehemu iliyobakia utaendelea kwa mwaka ujao wa fedha kutegemeana na upatikanaji wa fedha hizo.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Mkoa wa Shinyanga, barabara hii ilikuwa ikipitika kwa taabu miaka ya nyuma kutokana na ufinyu wa Bajeti. Lakini kuanzia mwaka wa 2001/2002, matengenezo ya sehemu korofi yalianza kufanywa kwa awamu na hivyo kuifanya barabara hiyo kupitika kwa wakati wote kama ifuatavyo: Katika mwaka wa fedha wa 2001/2002, maeneo ya barabara kati ya Ikungu na Malampaka kilomita 18 na kilomita 8 kati ya Malampaka na Malya yalifanyiwa matengenezo kwa gharama ya shilingi milioni 80 na hivyo kuifungua barabara na kupitika kwa wakati wote.

Katika mwaka wa fedha wa 2002/2003, maeneo ya barabara ya Malampaka hadi Malya yalifanyiwa matengenezo kwa gharama ya shilingi milioni 25 na katika mwaka wa fedha wa 2003/2004, sehemu ya barabara kati ya Malampaka hadi Malya ilifanyiwa matengenezo kwa gharama ya shilingi milioni 23 na sehemu ya Ikungu hadi Maswa kilomita 27 ilifanyiwa matengenezo kwa gharama ya shilingi milioni 39. Baada ya matengenezo hayo kukamilika, barabara ya Malya hadi Maswa kupitia Malampaka na Ikungu inapitika kwa uhakika mwaka mzima.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu kupitia Wakala wa Barabara, itaendelea kuzifanyia matengenezo ya kawaida barabara hizi ili ziendelee kupitika kwa urahisi na hivyo kutoathiri shughuli za kibiashara na za kijamii.

**MHE. JACOB D. SHIBILITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri na Mheshimiwa Naibu Waziri, ningependa niulize swali moja la nyongeza. Ni kweli kabisa *TANROAD* Mkoa wa Mwanza inafanya kazi nzuri na inaonekana. Lakini ningependa niulize upande wa Jojilo-Gatuli na baadaye Gatuli-Igunguli mpaka Runere ni lini itatengenezwa barabara hii inayoshughulikiwa na Mkoa?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, barabara ya Jojilo hadi Gatuli na baadaye kuelekea kutoka Gatuli hadi Lunere (haya ni majina ya Kisukuma kidogo), ni matumaini yangu kwamba, itatengenezwa kufuatana na utaratibu wa kutumia pesa za *Road Toll* kwa kadri *Regional Manager* anavyoona barabara hiyo inahitaji kufunguliwa na kadri ya upatikanaji wa pesa. Lakini nina imani kabisa zitatengenezwa barabara hizi kwa sababu sasa hivi tumewasiliana na *Regional Manager* wa Mwanza na *Regional Manager* wa Shinyanga wawasiliane kufungua hizo barabara kwa pamoja kwa sababu zinaungana mno.

Na. 17

**Wapiganaji wa Vita vya Kagera - 1978/79**

**MHE. ERNEST G. MABINA (k.n.y. MHE. KABUZI F. RWILOMBA)** aliuliza:-

Kwa kuwa vita vya Kagera vya mwaka 1978/79 vilishirikisha watu mbalimbali wa kawaida, wanamgambo na watumishi; na kwa kuwa baada ya vita hivyo wengi wao walirudi nyumbani kama walivyokwenda; na kwa kuwa wengi wao hususan wasio watumishi wa Serikali bado hali zao ni mbaya sana kimaisha:-

(a) Je, Serikali haioni kuwa sasa ni muda muafaka wa kuwakumbuka kwa kuwapa motisha?

(b) Je, kutofanya hivyo, Serikali haioni kuwa inawakatisha tamaa wananchi hao ya kulinda nchi yao kwa pamoja na pindi likitokea janga jingine kama hilo hawatajitolea kama waenda vitani, bali watakwenda na moyo wa kupora mali badala ya kupigania nchi yao?

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Faustine Kabuzi Rwilomba, Mbunge wa Busanda, naomba kutoa maelezo ya ufafanuzi kama ifuatavyo:-

Amiri Jeshi Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi alipokuwa akitangaza vita dhidi ya majeshi ya uvamizi ya nduli dikteta wa karne, Iddi Amin Dada mwaka 1978, aliomba na aliwaagiza wananchi wa Tanzania kushiriki kwa hali na mali katika kuikomboa sehemu ya ardhi ya nchi yetu iliyovamiwa na dikteta huyo na kuitangaza dunia kuwa sehemu hiyo ya ardhi ya Tanzania itakuwa chini ya himaya ya utawala wake wa kijeshi na

kupandisha bendera ya nchi yake katika ardhi yetu. Wananchi wote wa Tanzania wake kwa waume, wazee kwa vijana, Wafanyakazi wa Taasisi, Asasi mbalimbali, Watumishi wa Serikali, Makampuni Binafsi, Mashirika ya Umma na Madhehebu ya Dini, umma wote wa Tanzania uliitikia wito wa Baba wa Taifa kwa moyo wa uzalendo kumchapa nduli Iddi Amin na majeshi yake na kuwang'oa kutoka katika ardhi yetu na ikibidi kumnyamazisha milele.

Hivyo basi, vita ya Kagera ilipiganwa na Watanzania wote waliokuwa mstari wa mbele katika uwanja wa mapambano na waliobaki nyumbani nao pia walikuwa vitani kwa kuwa walikuwa wakilinda taasisi, viwanda, majengo, mashirika na mali za umma na za wananchi ili zisihujumiwe na maadui, walitoa fedha, magari, nyumba, vyakula, mifugo, vifaa mbalimbali, madawa na wengi walitoa damu kwa ajili ya wapiganaji waliojeruhiwa. Ushindi mkubwa uliopatikana ulikuwa ni heshima ya Watanzania wote bila kujali waliokuwa uwanja wa vita na waliokuwa nyumbani kwa kuwa wote walishiriki. Wote walikuwa wakitekeleza wajibu wao wa Kikatiba kama ilivyoainishwa na Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya mwaka 1984 iliyorekebishwa mwaka 2000 katika Aya ya 28(1) inayoeleza kuwa kila mwananchi ana wajibu wa kulinda, kudumisha ulinzi na uhuru wa Taifa.

Baada ya ushindi kupatikana, wapiganaji wote waliokuwa katika uwanja wa vita, walirudi nyumbani na kupokelewa kishujaa kwa heshima kubwa Kitaifa na Mikoani. Kila aliyeshiriki katika vita alitunukiwa nishani kama heshima ya kutambua na kuthamini mchango wake. Watu wote walioshiriki vitani walilipwa kiinua mgongo na mishahara yao ya kipindi chote walichokuwa vitani. Kwa mashujaa wetu waliopoteza maisha yao, kumbukumbu zao zimehifadhiwa kwa kujengewa Mnara wa Mashujaa katika makaburi yaliyoko Kaboya Mkoani Kagera.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa maelezo hayo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Faustine Kabuzi Rwilomba, Mbunge wa Busanda, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Serikali na umma wote wa Tanzania kamwe haitasahau michango ya wananchi wa Tanzania waliotoa katika vita ya kumng'oa nduli, dikteta wa karne, Iddi Amin, kutoka katika ardhi yetu. Thamani ya michango ya Watanzania haiwezi kupimika kwa thamani ya fedha. Hakuna motisha inayotosheleza kuwalipa wananchi wote kwa kazi nzuri waliyoifanya kumng'oa Iddi Amin kutoka katika ardhi yetu zaidi ya kuendelea kuheshimu na kuenzi michango yao. Nchi yetu ilipata heshima mbele ya Mataifa. Umoja, mshikamano na Sera safi ya Ulinzi wa Taifa letu, ndiyo siri ya ushindi wa vita ya Kagera, kama ilivyodhihirishwa na kauli ya Baba wa Taifa kuwa "Umoja unaweza kushinda nguvu ya mizinga ama mabomu."

(b) Sikubaliani na Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali inawakatisha tamaa wananchi waliojitoa mhanga vitani. Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, inawapongeza wale wote walioshiriki vita ya Kagera kwa kitendo chao cha uzalendo na kuweka mbele maslahi ya Taifa letu, badala ya maslahi binafsi. Ulinzi na Usalama wa Taifa hili ni jukumu letu sote. Kila Mtanzania hasa kila Mzalendo,

anawajibika kulinda hifadhi na kudumisha uhuru na Umoja wa Taifa, kulingana na Katiba.

Siamini kuwa wananchi wenye maadili mema, wazalendo, waadilifu, wenye desturi, mila na utamaduni wa Taifa letu, wakajitoa kwenda vitani kutetea Taifa lao wakiwa na lengo la kupora mali, kwani uporaji mali wakati wa vita ni kosa la kivita *(War Crime)*. *(Kicheko/Makofi)*

**SPIKA:** Napenda kukumbusha kanuni inayotaka majibu ya maswali yawe mafupi. Sasa sikupenda kumwingilia Mheshimiwa Waziri wakati anatoa kauli ya Serikali lakini napenda kuliarifu Bunge kwamba, amemaliza muda wote wa swali hilo.

Kwa hiyo, hakuna maswali ya nyongeza, tunaendelea na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto. *(Kicheko)*

Na. 18

***Women Development Fund***

**MHE. AGGREY D. J. MWANRI** aliuliza:-

Kwa kuwa kwa muda mrefu sasa Serikali imekuwa ikitoa mikopo ya *Women Development Fund* kwa vikundi mbalimbali vya akina mama nchini na kwa kuwa mfuko huo umekuwa na manufaa kwa jamii ya Kitanzania:-

(a) Je, ni vikundi vingapi vimewahi kupewa mikopo hiyo katika Jimbo la Siha?

(b) Je, ni nini thamani ya mikopo hiyo kwa ujumla kwa kila kikundi?

(c) Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba vikundi vingi zaidi vinapatiwa mikopo hiyo ili jamii iweze kuondokana na umaskini?

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Aggrey Mwanri, Mbunge wa Siha, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, vikundi vilivyopewa mikopo kutoka Mfuko wa Maendeleo wa Wanawake *(WDF)* kupitia Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kwa Jimbo la Siha ni vikundi 12 vyenye wanawake 100.

(b) Thamani ya mkopo kwa kila kikundi ni kama ifuatavyo: Azimio Sh. 200,000/=, Tumaini Sh. 200,000/=, Jiendeleze Sh. 250,000/=, Jitafutie Sh. 300,000/=, Nifa Sh. 300,000/=, Tupendane Sh. 100,000/=, Urumwi Sh. 200,000/=, Faraja Sh. 200,000/=, Jitegemee Sh. 200,000/=, Fuka Sh. 200,000/=, Fungameno Sh. 600,000/=,

Isanja Kaboko Sh. 200,000/=, jumla ni Sh. 2,950,000/=. Mwezi Februari, 2004, Halmashauri ya Wilaya ya Hai ilipelekewa Sh.4,000,000/= za *WDF* za mwaka 2002/2003 ambazo zinategemewa kugawiwa kwa vikundi mbalimbali vikiwemo hivyo nilivyovitaja.

(c) Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha kwamba, vikundi vingi zaidi vinapata mikopo na kuiwezesha jamii kuondokana na umaskini Serikali imefanya yafuatayo:-

(i) Kiwango cha fedha za mikopo kimeongezwa kutoka shilingi laki saba miaka ya 1998/1999 hadi shilingi milioni nane kwa mwaka 2002/2003.

(ii) Serikali imepunguza kiwango cha riba kutoka asilimia 24 iliyokuwa inatozwa mwaka 1994 Mfuko ulipoanzishwa kufikia asilimia 10 kuanzia Julai Mosi, 1999 hadi sasa.

(iii) Wizara imeweka utaratibu wa kuwekeana Mikataba Maalum ya marejesho ya mikopo kati ya Wizara na Halmashauri za Wilaya ili kuhakikisha fedha zinarejeshwa kwa wakati na kuwezesha wanawake wengi zaidi kukopa. Vile vile Wizara imeelekeza riba ya asilimia kumi inayotozwa mikopo hiyo itumike kutoa mafunzo ya mbinu bora za kibiashara na kuzifanya biashara hizo kuwa stahimilivu.

(iv) Serikali imeziagiza Halmashauri za Wilaya kuchangia asilimia tano za mapato yake katika Mfuko huu ili kuutunisha zaidi.

**MHE. AGGREY D. J. MWANRI:** Nakushukuru Mheshimiwa Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Naomba nichukue nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Waziri, kwa majibu yake mazuri kwa kuvitaja hivi vikundi na kiasi hicho ambacho kimetolewa. Kwa kuwa inaonekana kwamba idadi ya vikundi vinavyotoka katika Jimbo la Siha kwa sababu nina hakika kwamba vimetajwa vingine vinavyotoka katika Jimbo la Hai ameangalia Hai nzima kama Wilaya. Je, Mheshimiwa Waziri baada ya hayo yote aliyoeleza, atakubaliana na mimi kwamba kuna haja ya kuongeza mkopo kwa ajili ya vikundi vya akina mama walioko katika Jimbo la Siha?

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyokwishasema katika jibu langu la msingi, hivi sasa Wizara imeongeza mkopo hadi kufikia shilingi milioni 8 kwa kila Wilaya. Kwa hiyo, nina imani kwamba, Mheshimiwa Mbunge ikiwa atashirikiana na wananchi wa Siha kuanzisha vikundi zaidi, watanufaika zaidi kwa sababu mkopo sasa umetunishwa. Pamoja na hayo tunafahamu kwamba, Halmashauri ya Siha inaendelea kuchangia Mfuko huu kwa hiyo tuna imani fedha zitaongezeka.

Na. 19

**Msamaha kwa Akina Mama Wakopaji**

**MHE. ESHA H. STIMA** aliuliza:-

Kwa kuwa akina mama wengi walichukua mikopo kwa ajili ya kuanzisha miradi ya kiuchumi ili waondokane na umaskini kwa kujenga migahawa, maduka, nyumba, shughuli za bustani, kilimo na ufugaji; kwa kuwa kwa bahati mbaya wakopaji hao hushindwa kurudisha mikopo yao kutokana na maafa ya moto, ukame, magonjwa, wizi na ubomoaji wa vibanda au nyumba kwa ajili ya kupanua barabara bila kulipwa fidia:-

(a) Je, Serikali na Taasisi zinazotoa mikopo zina mpango gani wa kusamehe waliopata matatizo ya aina hiyo?

(b) Je, Serikali na Taasisi zinazohusika na utoaji wa mikopo wanaweza kuwaongezea muda wa kulipa madeni yao wakopaji hao badala ya kuwapeleka Mahakamani?

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla sijajibu swali la Mheshimiwa Esha Stima, lenye sehemu (a) na (b), ningependa kutoa maelezo mafupi yafuatayo:-

Kati ya Mifuko mingi inayotoa mikopo kwa wanawake, Wizara yangu inasimamia fedha za Mfuko wa Maendeleo wa Wanawake *(WDF),* zinazotolewa na Serikali. Mfuko huu ulianzishwa kwa nia ya kufanya uwe wa mzunguko na azma hiyo bado ipo hadi leo hii. Kwa kuzingatia azma hii, Wizara yangu imeweka utaratibu mahsusi unaolenga kuhakikisha kwamba, fedha zilizotolewa zinarejeshwa kwa wakati ili wanawake wengi zaidi waweze kukopeshwa. Kwa upande wa Mfuko huu, Wizara haijawahi kupokea taarifa zozote kuhusu wakopaji kushindwa kurejesha na kulazimika kufikishwa Mahakamani kutokana na sababu alizozitaja Mheshimiwa Mbunge.

Tathmini ya urejeshaji wa mikopo hiyo iliyofanywa na Wizara yangu inaonyesha kwamba, sababu kubwa ya kutorejesha mikopo ni ukosefu wa mbinu za kibiashara, tatizo la upatikanaji wa masoko na wakopaji wachache kukosa uaminifu.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Esha Stima, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Kwa kuwa azma yetu ni kuendesha Mfuko huu kibiashara na kwa utaratibu wa mzunguko, Serikali haioni kama ni muafaka kusamehe madeni hayo ambayo hayajalipwa, badala yake Serikali inaona ni vema kutafuta ufumbuzi wa tatizo la urejeshaji linalotokana na ukosefu wa mbinu za kibiashara na vile vile tatizo la urejeshaji linalotokana na ukosefu wa mbinu za kibiashara na vile vile tatizo la ukosefu wa masoko.

Kwa mantiki hiyo, Wizara yangu imetoa maelekezo kuwa asilimia 10 inayotozwa kama riba itumike kwa ajili ya mafunzo ya mbinu bora za kibiashara. Hali kadhalka Wizara imetoa taarifa kupitia Waheshimiwa Wabunge Wanawake wote zinazohusu upatikanaji wa masoko kwa ajili ya vikundi vya wanawake.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inaamini kwamba, hatua hizi ni muafaka zaidi kuliko kufikiria kutoa msamaha wa jumla kwa wote walioshindwa kurejesha mikopo hiyo.

(b) Mheshimiwa Spika, hivi sasa Wizara imeweka utaratibu mpya wa Mkataba kati ya Halmashauri na Wizara yenyewe. Utaratibu huu unazielekeza Halmashauri kurejesha fedha za mikopo kwenye akaunti maalum iliyofunguliwa katika Benki ya *CRDB,* Tawi la Azikiwe Dar es Salaam katika muda wa mwaka mmoja kabla hazijapewa mkupuo mwingine. Wizara inaamini kuwa muda huu unatosha kuziwezesha Halmashauri kukopesha, kufuatilia na kukusanya marejesho. Nia ya Wizara kuweka utaratibu nilioutaja ni kuufanya Mfuko huu uwe endelevu na wanawake wengi zaidi waweze kukopa. Haja ya kuweka muda maalum na kusisitiza urejeshaji kwa wakati uliopangwa inatokana na azma ya Serikali ya kuzingatia kanuni bora za fedha zilizopitishwa na Bunge hili Tukufu kupitia sheria mbalimbali.

**MHE. ESHA H. STIMA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri aliyoyatoa Mheshimiwa Waziri, lakini nilikuwa na swali dogo la nyongeza ambalo linahusu wanawake wa nchi hii ndiyo wanaofanya kazi nzito zinazowezesha, kuinua hali ya uchumi katika nchi yetu na ndani ya jamii zao. Je, Mheshimiwa Waziri, haoni kwamba kuna umuhimu wa wanawake waliokopa mikopo hiyo na baadaye kuvunjiwa vibanda vyao kutokana na utaratibu huu wa kupanua barabara wakasamehewa walau riba za madeni yao kwa sababu hawakukusudia suala hilo limetokea kwa utaratibu wa Kitaifa? *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, mikopo hii inapotolewa inatarajiwa kwamba wakopaji watakuwa wanazingatia kanuni na taratibu za kawaida za kuendesha biashara zao. Lakini pia ikitokea kwa namna moja au nyingine, mkopaji ameingia katika matatizo ambayo Mheshimiwa Mbunge ameyazungumzia, basi itabidi kurejea masharti ya Mkataba yanasemaje. Yapo masharti ambayo yanaweza kuelekeza nafuu au upunguzaji wa riba kutokana na matatizo yaliyompata mkopaji lakini hii itategemea Mkataba ule unasemaje kwa sababu Mikataba mingi huwa inaweka kipengele kwamba endapo yatatokea maafa yaliyopo nje ya uwezo wa binadamu yaani maafa yanayotokana na nguvu za Mungu, basi labda hilo linaweza likapewa nafuu chini ya Mkataba huo lakini vinginevyo itakuwa ni vigumu. Tunasisitiza biashara tuzifanye kwa kuzingatia kanuni zilizopo ili kuepuka matatizo kama hivyo, mfano kuvunjiwa vibanda kama tumejenga karibu na barabara.

**MHE. HALIMA OMAR KIMBAU:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na kwamba kuna vikundi vinavyodaiwa lakini pia kuna Halmashauri za Wilaya ambazo hazijatoa ile *percent* ambayo

wanawajibika kuitoa. Je, Serikali kupitia Wizara Mama ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto wanachukua hatua gani kuhakikisha kwamba hizi Halmashauri nazo zinalipa madeni makubwa kwa ajili ya Mfuko huu?

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, inawezekana kama alivyosema kwamba, baadhi ya Halmashauri zinashindwa kutenga asilimia tano kama agizo la Mheshimiwa Waziri Mkuu linavyosema. Lakini tatizo ambalo tumelibaini katika Halmashauri nyingi ni ukusanyaji hafifu wa mapato. Pale ambapo Halmashauri imeshindwa kukusanya mapato kwa lengo walilojiwekea, inatokea kwamba fungu linakuwa dogo.

Lakini utafiti tuliofanya na mazungumzo tuliyofanya na Halmashauri mbalimbali ni kwamba, pale makusanyo yanapokuwa mazuri, wanalipa kwa kufidia kiwango ambacho hawakukitoa wakati ule walipotakiwa kukitoa.

Mheshimiwa Spika, lakini napenda kumuarifu Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako Tukufu kwamba, Wizara yetu itaendelea kushirikiana kwa karibu na Halmashauri ili waweze kujazia Mfuko huu wa Maendeleo ya Wanawake.

Na. 20

**Mradi wa Maji Matwiga - Mtanila**

**MHE. NJELU E. M. KASAKA** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali ilikubali kufufua Mradi wa Maji wa Matwiga - Mtanila na ilitenga Sh.3,000,000/= katika mwaka wa fedha 2001/2002 kwa ajili ya kufanya maandalizi:-

(a) Je, hatua za kufufua Mradi huo zimefikia wapi?

(b) Je, kuna mipango gani iliyoandaliwa kushughulikia tatizo la maji katika Tarafa za Kiwanja na Kipembawe ambako vijiji vingi havina maji ya uhakika?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Njelu Kasaka, Mbunge wa Lupa, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mradi wa Maji Matwiga/Mtanila ulibuniwa mwaka 1972 ukilenga kuhudumia vijiji 7 vya Kata za Matwiga, Mtanila, Lupatingatinga na Mamba.

(b) Ujenzi wa Mradi uligharamiwa na fedha za Benki ya Dunia kupitia Mamlaka ya Tumbaku. Mwaka 1977 Benki ilisitisha utoaji wa fedha na kuufanya Mradi kutokamilika kama ulivyobuniwa. Hadi msaada unasitishwa, vijiji vyote isipokuwa Kijiji cha Mamba vilikuwa na huduma ya maji.

Huduma ya maji iliendelea kupatikana hadi mwaka 1992 iliposimama kabisa kutokana na vitendo vya wizi wa mitambo ya kusukuma maji, mabomba, uharibifu wa mabirika ya maji, vituo vya kuchotea na mtego wa maji.

Mwaka 2001/2002, Wizara yangu ilituma wataalam kuandaa taarifa ya awali ya Mradi na kuwezesha Serikali kutenga shilingi milioni 3 ili kufanya upembuzi yakinifu, uliolenga kupendekeza mkakati wa kufufua Mradi. Gharama za kurejesha Mradi kwenye hali ya utoaji huduma kwa walengwa zinakadiriwa kuwa shilingi milioni 200.

Mheshimiwa Spika, kutokana na upembuzi huo, imependekezwa kuwa lijengwe bwawa dogo kwenye Mto Mkowiji ili kuhifadhi maji ya kutosheleza mahitaji halisi ya Mradi kwa sasa. Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kazi hiyo.

(c) Mheshimiwa Spika, Tarafa ya Kipembawe na Kiwanja ambazo zina Kata 13 zenye jumla ya vijiji 37, zinategemea maji ya chini ya ardhi kama vyanzo vya kuaminika. Kutokana na hali hiyo, Halmashauri ya Wilaya ya Chunya imefanya upimaji wa sehemu za kuchimba visima viwili kwenye Vijiji vya Mlimanjiwa, Gogima, Igundu na Shoga. Baada ya upimaji kufanyika, kazi ya uchimbaji itaanza baada ya fedha kupatikana.

**MHE. NJELU E. M. KASAKA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali ya nyongeza kama ifuatavyo:-

(a) Huo Mradi kama alivyoeleza mwenyewe ni wa miaka ya 1970, inapokuwa baada ya zaidi ya miaka 20 Serikali inasema bado inatafuta hela mpaka zipatikane, hivi kweli jibu hilo linaweza kuaminika na wananchi wa sehemu husika kama kule Matwiga na Mtanila?

(b) Kwa kuwa pale sasa kuna kisima ambacho kinahitaji kuwekwa mashine ya dizeli, wakati wanaposubiri kupata fedha nyingi kwa ajili ya hilo bwawa, Serikali inaweza kuwa tayari kukipatia Kijiji cha Matwiga mashine ya dizeli angalau waanze kupata maji hadi hapo bwawa litakapojengwa?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, ni kweli kama nilivyoeleza, Mradi umechukua miaka 20 lakini katika majibu yangu ya awali nimeeleza Mradi huo ulikuwa unafanya kazi mpaka pale baadhi ya watu ambao hawakuutakia mema Mradi huo walipoanza kuuharibu kwa kuiba vifaa vyake na hivyo ikafikia wakati ambapo pia Serikali nguvu zake kifedha zilikuwa sio nzuri ndio maana imechukua muda wote huo.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kulingana na taarifa ambazo tunazipata kutoka Wilayani, vipaumbele vinatakiwa kutengenezwa na Wilaya zenyewe na katika kipindi hicho hicho, Serikali kwa kushirikiana na Halmashauri tumechimba visima vingi vya maji mfano Mbugani, Mapogoro, Mabagala, Upendo Mashari na Mpembe. Visima hivi

vimegharimu karibu shilingi milioni 25. Sasa haina maana kwamba, kwa Serikali kuendelea kutafuta Mradi wa Maji katika maeneo hayo, haiangalii matatizo ya wananchi. Tunaendelea kuangalia matatizo ya wananchi na wakati huo huo pia tumetoa fedha kwa ajili ya malambo madogo kwa sehemu za wafugaji wa Wilaya ya Chunya.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa jitihada ambazo Mheshimiwa Mbunge anazifanya na Serikali pamoja na Halmashauri ya Wilaya, nina hakika matatizo haya tutafikia mahali tutayatatua kwa kushirikiana pamoja.

Na. 21

**Bodi ya Maji Kigoma**

**MHE. DR. AMANI W. A. KABOUROU** aliuliza:-

Kwa kuwa Mji wa Kigoma-Ujiji tayari una Bodi ya Maji:-

(a) Je, Mradi wa Maji Kigoma-Ujiji umegharimu fedha kiasi gani tangu uanzishwe?

(b) Je, ni lini tanki la maji la Mlole litaanza kufanya kazi kwa uhakika?

(c) Je, Serikali ina mpango gani wa kuiwezesha Bodi ya Maji ya Kigoma-Ujiji kuwa na Kitengo cha Maji Taka kinachofanya kazi zake barabara?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Amani Kabourou, Mbunge wa Kigoma Mjini, lenye sehemu (a) (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mamlaka ya Majisafi na Majitaka Mjini Kigoma-Ujiji ilianzishwa kwa Sheria Na.8 ya 1997 katika kundi “C” la Mamlaka hizo ambapo Serikali iliwajibika katika kulipa mishahara ya watumishi, umeme na gharama za uendelezaji wa miundombinu. Julai, 2002 Mamlaka ilipanda daraja na kuingia katika kundi “B” ambapo ilianza kulipia gharama zote za umeme wa mitambo ya kusukuma maji.

Mheshimiwa Spika, naomba niendelee kujibu swali kama ifuatavyo:-

(a) Wizara yangu kwa kushirikiana na Mamlaka ya Maji Mjini Kigoma, imekuwa ikitekeleza mradi wa kupeleka maji katika vitongoji vya Mlole na Masanga toka mwaka 2000/2001 kwa wakazi wapatao 10,000. Hadi sasa shilingi milioni 150 zimetumika kwa ajili ya kufunga bomba kuu km. 1.8, kulaza mabomba ya kusambaza maji km. 3.5, kujenga tanki lenye meta za ujazo 225 na kununua mitambo miwili ya kusukuma maji.

(b) Tanki la Mlole lenye mita za ujazo 225 limekamilika mwishoni mwa mwaka 2002/2003 na litaanza kufanya kazi kwa uhakika Juni, 2004 baada ya kufungwa mitambo miwili mipya ya kusukuma maji yenye thamani ya Sh.60.7 milioni iliyoagizwa na Wizara yangu toka Australia.

(c) Mamlaka ya Majisafi na Majitaka Mjini Kigoma-Ujiji haina mfumo wa majitaka. Huduma hii bado inatolewa na Halmashauri ya Mji kwa kutumia magari ya kunyonya majitaka. Ili kuanzisha Kitengo cha Majitaka katika Mamlaka inahitajika pawepo na mfumo huo. Serikali inatafuta fedha ili kuimarisha Mamlaka ya Majisafi na Majitaka ya Mji wa Kigoma-Ujiji ikiwa ni pamoja na mfumo wa uondoaji wa majitaka. Lengo la ujenzi wa mifumo hiyo ni kuondoa tatizo sugu la kutitirisha majitaka yasiyosafishwa katika Ziwa Tanganyika ambacho ni chanzo cha majisafi kwa Mji huo.

**MHE. BERNADINE R. NDABOINE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa hiyo mitambo ya kusukuma maji aliyoitaja Mheshimiwa Naibu Waziri inategemea umeme na kwa kuwa Kigoma haina umeme wa uhakika, je, Serikali itauhakikishia lini Mkoa wa Kigoma kupata umeme wa uhakika?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Spika, suala la umeme utapatikana lini kwa Mji wa Kigoma, nina hakika Wizara na Serikali kwa ujumla, inafanya bidii ili gridi ya Taifa iweze kufika Mikoa yote nchini Tanzania.

Mheshimiwa Spika, ningependa pia nieleze kwamba, hata kama umeme ukipatikana kwa saa moja, ikiwa wananchi wana vyombo vya kutosha vya kutunza maji, unaweza kuteka maji ya kutosha kwa matumizi ya siku nzima haitalingana na kufuata maji mtoni kwenye ndoo ya lita 20.

Na. 22

**Fedha za Wafadhili Kupitia *Health Basket Fund***

**MHE. DR. WILLBROD P. SLAA** aliuliza:-

Kwa kuwa Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2002 imeonyesha kwamba Wizara ya Afya ilihamisha kwa taasisi mbalimbali jumla ya Sh.15,086,013,939/= na kwamba hadi taarifa hiyo ilipowasilishwa Bungeni hapakuwa na maelezo yoyote ya matumizi ya fedha hizo kisheria; na kwa kuwa mwaka 2003 Wizara ilitumia wakaguzi wa *Price-Water-House Coopers* kutathmini fedha hizo zilizotolewa na wafadhii kupitia Mfuko wa *Health Basket Fund* na Wilaya ya Karatu ni miongoni mwa Wilaya zilizokaguliwa:-

(a) Je, hadi kufikia tarehe 30 Desemba, 2003 ni jumla ya fedha kiasi gani zaidi ya hizo zimepelekwa kwenye taasisi hizo na kila taasisi na Wilaya hususan Wilaya

ya Karatu zimepata kiasi gani kutokana na fedha hizo ambazo hazijatolewa maelezo ya matumizi?

(b) Je, tumejifunza nini kutokana na utaratibu huo wa *Health Basket Fund,* matatizo gani yamejitokeza katika utekelezaji wa mpango huo na kama yapo matatizo yaliyojitokeza kutokana na matumizi ya fedha hizo, Wizara imechukua hatua gani kurekebisha kasoro hizo na imechukua hatua gani za kinidhamu kwa wahusika waliosababisha hali hiyo?

(c) Je, ni lini sasa taarifa hizo za ukaguzi wa *Price-Water-House Coopers* zitatolewa kwa wadau wote ili zijadiliwe wakiwemo Baraza la Madiwani la Wilaya husika?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Willbrod P. Slaa, Mbunge wa Karatu, lenye sehemu (a), (b) na (c), napenda kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, fedha zinazotolewa na wafadhili ni sehemu ya fedha za Serikali zinazotengwa ili kutekeleza shughuli mbalimbali zikiwemo zile za taasisi mbalimbali chini ya Wizara ya Afya. Kila Taasisi hutengewa fedha kulingana na kiwango kilichopo na kwa kufuata vipaumbele vya Sekta ya Afya. Fedha zilizotolewa kupitia Mfuko wa *Basket Fund* hazikuhamishwa bali ni katika utaratibu wa kuzitengea taasisi mbalimbali zilizo chini ya Wizara ya Afya kama ilivyo kwa fedha za Serikali zinazopelekwa katika taasisi hizo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuwatumia Wakaguzi *Price-Water-House Coopers* katika kutathmini matumizi ya fedha za *Basket,* utaratibu huu ulikubaliwa kwa pamoja kati ya Wizara, Wafadhili wa Mfuko na Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Serikali ili pande zote ziweze kuridhika na matumizi ya fedha chini ya utaratibu huu. Hata hivyo, katika fedha zilizotajwa hapo juu, Halmashauri zote nchini ikiwepo Halmashauri ya Karatu, hazihusiki na mgawo huo kwani kiasi hicho kilitolewa kwa taasisi zinazopata fedha kutoka Fungu 52 tu yaani taasisi zilizo chini ya Wizara ya Afya.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Willbrod P. Slaa, Mbunge wa Karatu kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, hadi kufikia tarehe 30 Desemba, 2003 jumla ya Sh.15,086,013,939/= zilikwishapelekwa kwa Taasisi chini ya Wizara ya Afya na kiasi cha Sh.17,116,926,945/= zilishapelekwa kwa Halmashauri za Wilaya ikiwemo Wilaya ya Karatu.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Karatu imeanza rasmi kupata fedha za *Basket* katika awamu ya tatu kuanzia Januari, 2003. Katika kipindi cha kuanzia Januari hadi Desemba, 2003, Wilaya ya Karatu ilipata jumla ya Sh.80,317,125/=. Katika kipindi cha

kuanzia Januari hadi Desemba, 2004, Wilaya Karatu inategemea kupata kiasi cha Sh.99,316,166/= kwa ajili ya kutekeleza majukumu mbalimbali yaliyo chini ya Sekta ya Afya.

Mheshimiwa Spika, kwa utaratibu tuliojiwekea, hakuna fedha ambayo haijatolewa maelezo kuhusu matumizi. Kila Halmashauri kupitia vikao vilivyowekwa kwa taratibu, hupitia taarifa ya utekelezaji kwa kila robo kabla ya kuruhusu fedha nyingine kutolewa. Kwa mantiki hiyo, fedha iliyotolewa katika kipindi cha 2002 ilitolewa maelezo ya matumizi kwa wahusika wakiwemo wafadhili katika vikao mbalimbali.

(b) Mheshimiwa Spika, tangu kuanzishwa kwa utaratibu huu wa *Basket Fund,* kumekuwa na mafanikio makubwa katika utoaji wa huduma za afya katika ngazi mbalimbali. Utaratibu huu umechangia kwa kiasi kikubwa upatikanaji wa dawa, vifaa vya hospitali, ununuzi wa magari kwa ajili ya ukaguzi wa shughuli za afya Wilayani na vitendea kazi ambavyo hapo awali vilikuwa havipatikani kutokana na ukosefu wa fedha. Licha ya mafanikio hayo, palikuwepo na matatizo ya kiutekelezaji hasa kuwepo na miongozo mbalimbali. Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa pamoja na wafadhili, imefanya mapatio na kuoanisha miongozo hiyo na kuwa na mwongozo mmoja ambao utatumika badala ya kuwa na mlolongo wa miongozo.

(c) Mheshimiwa Spika, suala la kujadili taarifa ya ukaguzi lipo chini ya Halmashauri za Wilaya. Ni jukumu la Watendaji wa Wilaya pamoja na Baraza la Madiwani, kupanga kikao cha kujadili taarifa ya ukaguzi kwani nakala ya taarifa hiyo hupelekwa kila Wilaya.

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie nafasi hii kuzikumbusha Halmashauri za Wilaya kuwa taarifa za ukaguzi ni mojawapo ya taarifa ambazo Halmashauri za Wilaya zinalazimika kuzijadili ikiwa ni pamoja na mipango ya utekelezaji na taarifa za kila robo mwaka za Halmashauri.

**MHE. DR. WILLBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niulize swali moja la nyongeza. Nampongeza sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri lakini pamoja na hayo, nina swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa taarifa nyingi tunazozipata ni kuwa vipaumbele vya fedha za *Basket Fund* vinapangwa na wafadhili pamoja na Wizara na Vikao vya Kanda na vipaumbele hivyo haviwekwi na Halmashauri husika na hivyo vipaumbele vingine kama ukarabati wa Zahanati hauhusishwi na mpango huu. Je, kwanza kauli hiyo ni kweli na pili kama ni kweli Wizara inafanya nini kusaidia vipaumbele vya Wilaya ndio vichukuliwe kuliko vile vilivyowekwa na wahisani wenyewe?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba vipaumbele hujadiliwa kati ya Wafadhili na Wizara. Mara zote Wizara huweka vipaumbele vile ambavyo tunapata kutoka kwenye Wilaya za nchi yetu. Kwa maana hiyo basi, kwa upande wa Wizara vipaumbele ni vile ambavyo tunavipata kutoka Wilayani.

Mheshimiwa Spika, ukweli wa kwamba ukarabati hauhusishwi sio sahihi kuna asilimia katika *Basket Fund* ambayo inaruhusiwa kutumika katika ukarabati wa Zahanati.

Na. 23

**Ugonjwa wa Kisukari**

**MHE. MCHANDE SALIM MCHANDE** aliuliza:-

Kwa kuwa Ugonjwa wa Kisukari umekuwa ni tishio hapa Tanzania na duniani pote; na kwa kuwa Watanzania walio wengi wanaugua ugonjwa huo:-

(a) Je, ugonjwa huo husababishwa na nini?

(b) Je, ugonjwa huo kinga yake ni nini?

(c) Je, Tanzania kuna wagonjwa wangapi wa Kisukari?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Afya, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mchande Salim Mchande, Mbunge wa Konde, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, chanzo cha Ugonjwa wa Kisukari mpaka sasa hakijulikani ingawa ugonjwa huu huonekana kurithiwa katika ukoo kwa kiwango cha asilimia 40.

Mheshimiwa Spika, kuna aina mbili za Ugonjwa wa Kisukari: Aina ya kwanza ni ugonjwa unaojitokeza mtu akiwa na umri chini ya miaka 30 *(Type I Diabetes Mellitus).* Inafikiriwa kuwa ugonjwa huu hutokana na kuharibika kwa sehemu ya mwili inayoitwa kongosho *(pancreas),* ambayo hutoa homoni ya *insulin* inayohitajika ili mwili uweze kutumia sukari vizuri. Uharibifu huu unaweza kutokana na virusi, lakini mara nyingi sababu haijulikani. Wagonjwa wa aina hii huhitaji dawa ya sindano ya *insulin* maisha yao yote.

Aina ya pili ni *(Type II Diabetes Mellitus).* Ugonjwa unajitokeza kwa mtu akiwa na umri wa miaka zaidi ya 30. Wagonjwa hawa huwa na kongosho zisizotoa homoni ya *insulin* au misuli yao imepoteza uwezo wa kutumia *insulin* iliyopo. Mara nyingi sababu haijulikani lakini huweza kusababishwa na virusi, unywaji wa pombe uliokithiri ambao unasababisha athari kwa kongosho. Wagonjwa wa aina hii wanatibiwa kwa dawa za vidonge au kwa kufuata masharti ya chakula, mazoezi na kupunguza unene kama umezidi.

(b) Mheshimiwa Spika, hakuna kinga kamili ya Ugonjwa wa Kisukari kwa sababu chanzo chake bado hakieleweki vizuri. Hata hivyo, unene au kutofanya mazoezi

vinachangia kuwepo kwa aina ya pili ya Ugonjwa wa Kisukari na kunaweza kuepukika kwa kufanya mazoezi na kupunguza unene.

(c) Mheshimiwa Spika, utafiti uliofanyika Tanzania mwishoni mwa miaka ya 80 ulionyesha takwimu zifuatazo:-

| **Kundi la watu** | **Walio na ugonjwa wa Kisukari** |
|---|---|
| Watanzania wanaoishi vijijini | 1% |
| Watanzania wanaoishi mijini | 3-5% |
| Mapadri na Masista Watanzania | 6% |
| Wabunge Watanzania | 8% |
| Wananchi wenye asili ya Kiasia | 12% (K*icheko)* |

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa fursa hii. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina swali moja la nyongeza. Kwa kuwa moja katika jambo linalohitajika kwa wagonjwa hawa ni kupata hiyo dawa ya *insulin* na wengi wa wagonjwa hawa ni wanyonge, je, Serikali ina mpango gani wa kuwasaidia wale wasiojiweza kupata hiyo dawa?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, Sera ya Uchangiaji wa Huduma za Afya ni Sera ambayo imepitishwa na Serikali na hatuna budi kuifuata. Suala lililokuwepo hapa ni suala la misamaha kwa wasiojiweza. Nataka nilihakikishie Bunge lako Tukufu kwamba, hospitali zimepewa maelekezo ya kutoa huduma za afya bila malipo kwa wale watakaothibitika kwamba hawana uwezo wa kulipia.

**MHE. HAROUB SAID MASOUD:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina swali moja la nyongeza. Kwa kuwa maradhi ya kisukari husababisha maradhi mengine katika kiwiliwili cha binadamu, je, kwa yule mgonjwa wa kisukari ambaye meno yake hung'oka ovyo ni kinga gani itaweza kumzuia katika maradhi hayo mengine?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, tatizo kubwa la Ugonjwa wa Kisukari ni madhara yanayotokea baada ya muda mrefu kwa sukari kutoweza kuiweka katika kiwango kinachotakiwa yaani tatizo kubwa la kisukari ni *complications* zinazofuata. Bahati mbaya sana ugonjwa huu unaathiri maeneo karibu yote ya mwili. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, ningependa tu nitaje machache kwamba, Kisukari kinaweza kusababisha ugonjwa wa macho yaani macho kutoweza kuona, kinaweza kusababisha ugonjwa wa moyo, kinaweza kusababisha matatizo ya figo, kinaweza kusababisha kupoteza nguvu za kiume na kama Mheshimiwa Haroub anavyosema vile vile kupoteza meno. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, sasa jambo kubwa hapa ni kuhakikisha kwamba, tunai-*control* hiyo sukari. Kwa hiyo, ningependa kutoa wito kwa wote ambao wana ugonjwa

huu wahakikishe kwamba sukari yao wanaiweka katika kiwango kinachotakiwa ili kuondoa *complications* hizo nilizozitaja.

Na. 24

**Kuweka Dhamana ya Mali/Fedha Mahakamani**

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED** aliuliza:-

Kwa kuwa kwa utaratibu wa kisheria raia wenye mashauri yao Mahakamani wakati mwingine hutakiwa na Mahakama dhamana ya mali isiyoondosheka au fedha taslimu:-

(a) Je, katika kipindi cha mwaka 1995 hadi leo hii, dhamana ya fedha taslimu iliyowekwa kwa ajili ya mashauri mbalimbali kwa kila mwaka ni kiasi gani?

(b) Je, ni utaratibu gani unaotumika baada ya shauri kumalizika na mhusika kutakiwa arudishiwe fedha zake na apate haki yake?

(c) Je, kwa kawaida, huchukua muda gani mpaka dhamana hiyo irudishwe kwa mwenyewe?

**WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ndesamburo ... *(Kicheko)*

**SPIKA:** Hapana! *(Kicheko)*

**WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mbunge wa Kuteuliwa, lenye vipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Utaratibu unaotumika kwa sasa wa kuhifadhi kumbukumbu za dhamana ya fedha taslimu ni kwa kila Mahakama kutunza kumbukumbu zake katika daftari la dhamana ya fedha taslimu. Kwa mantiki hiyo, unahitajika muda wa kutosha ili kuweza kupata takwimu hizo na kuziainisha kutoka Mahakama zote nchini, ukizingatia kuwa kuna jumla ya Mahakama za Mwanzo 1,105 nchini, Mahakama 88 za Wilaya, Mahakama 22 za Hakimu Mkazi na Mahakama 11 za Mahakama Kuu.

(b) Kuhusu utaratibu unaoutumika baada ya shauri kumalizika ili mhusika arudishiwe fedha zake, mhusika anatakiwa kuwasilisha nakala halisi ya risiti aliyopewa wakati alipolipa fedha hizo kwa Mtunza Fedha wa Mahakama husika. Kwa sababu, Mtunza Fedha huandaa hati ya malipo akiambatanisha nakala halisi ya risiti na nakala ya Amri ya Mahakama inayoamuaru Mhusika kurudishiwa fedha hizo hapo itakapobidi

kufanya hivyo. Hati hiyo ya malipo huwasilishwa Hazina Ndogo kwa malipo baada ya kuwekwa saini na Hakimu wa Wilaya Mfawidhi, Hakimu Mkazi Mfawadhi au Msajili wa Wilaya kutegemea na Mahakama iliyopokea fedha hizo.

(c) Muda unaomchukua mhusika kutoka kuwasilisha nakala halisi ya risiti hadi kupata hundi yake unastahili kuwa siku thelathini kama fedha hizo zimewekwa kwenye hesabu za Hazina Ndogo ya Mkoa husika na miezi mitatu kama fedha hizo zimewekwa kwenye hesabu za Makao Makuu ya Mahakama?

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza yafyatayo:-

(a) Kwa kuwa Waziri ameshindwa kujibu swali (a) kama nilivyouliza, je, kwa nini akafanya haraka kulijibu wakati hakuwa tayari kulijibu?

(b) Kwa kuwa tatizo moja la wanaoweka dhamana yao Mahakamani ni kupotea kwa nyaraka na kumbukumbu za dhamana hizo, je, Serikali itakuwa tayari kuwapa riba kutokana na kuchelewa kulipwa malipo yao wale wanaodai haki zao Mahakamani?

**WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA:** Mheshimiwa Spika, katika jibu langu la msingi nilisema sababu ambayo imenifanya kutokuweza kujibu swali hilo ni kuwa kwanza, swali hili tumelipata wiki mbili zilizopita. Kwa hiyo, kuweza kukusanya takwimu hizi zote kutoka Mahakama mbalimbali inachukua muda mrefu. Lakini kama unafanya utafiti wa aina fulani kwa maana ya kutaka kujua hizi takwimu, basi naomba tuwasiliane ili tuweze kuzitafuta. Pili, si sahihi kwamba nyaraka kweli zinapotea, kama una ushahidi basi nitakuwa tayari kuuchukua ushahidi huo, lakini niseme tu kwamba, sasa hivi kwa wale ambao wanaweka dhamana na wakati mwingi siyo dhamana ya fedha ni dhamana ya hati. Kwa hiyo, suala la pesa kupotea kwa kweli siyo sahihi.

Na. 25

**Mashauri Ambayo Hayajaamuliwa**

**MHE. PHILLEMON NDESAMBURO** aliuliza:-

Kwa kuwa yapo mashauri mengi ambayo yamechukua miaka mingi bila kutolewa maamuzi wala kusikilizwa na kwa kuwa mashauri mengi yanapoachwa bila kutolewa uamuzi kwa wakati unaofaa kunawafanya wananchi kukosa haki zao lakini vile vile wanakosa imani na vyombo vyao vya dola yaani Bunge, Mahakama na Serikali:-

(a) Je, Serikali haioni kuwa kuna haja ya kuweka muda maalum kwa yale mashauri yote yanayohusu masuala ya wananchi, kwa mfano, muda uwe chini ya miezi sita, yawe yameshatolewa uamuzi?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kuwa kesi zinasikilizwa na kuamuliwa upesi iwezekanavyo ili wahusika waweze kupata haki zao?

**WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ndesamburo, Mbunge wa Moshi Mjini, lenye vipengele (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, mashauri yanapochukua muda mrefu bila kutolewa maamuzi wala kusikilizwa kwa wakati unaofaa kunawafanya wananchi kukosa haki zao. Zipo sababu za msingi zinazochangia mashauri ya Madai na Jinai kutokumalizika upesi iwezekanavyo ili wahusika waweze kupata haki zao. Sababu hizo ni pamoja na uhaba wa Mahakama za ngazi zote, uhaba wa Mahakimu wa ngazi zote na Majaji, urasimu wa kisheria na ufinyu wa Bajeti.

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikichukua hatua na kuandaa mipango mbalimbali ili kukabiliana na tatizo la ucheleweshaji wa upatikanaji wa haki. Mipango hiyo ni pamoja na kuanzisha Kamati za Kusukuma Mashauri, kuhimiza ukamilishaji mapema wa upelelezi wa mashauri ya jinai, kuajiri Mahakimu na Majaji zaidi na kuongeza bajeti ya Idara ya Mahakama na usikilizaji wa mashauri ya madai kwa njia ya usuluhishi. Hatua nyingine iliyochukuliwa na Serikali ili kukabiliana na tatizo la ucheleweshaji wa maamuzi au usikilizwaji wa mashauri ni pamoja na kuanzishwa kwa Mikataba ya Huduma kwa Wateja ambapo vyombo vinavyohusika na haki kama vile, Mahakama, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Polisi, wamejiwekea vipindi maalum ambavyo ndani yake wanapaswa kuwa wameshughulikia mambo yanayofikishwa kwao na kuyatolea maamuzi ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa Serikali pia inaiangalia upya Sheria ya Mwenendo wa Mashauri ya Jinai ili kuondokana na urasimu wa kisheria usio wa lazima na kuweka muda maalum kisheria wa kutoa hukumu baada ya kusikiliza pande zote mbili kwenye shauri husika. Lakini kutokana na *legal technicalities* katika Sheria za Mienendo ya Mashauri ya Madai na Jinai, inakuwa vigumu kuweka muda maalum ambao mashauri yote yanatakiwa yawe yameshatolewa maamuzi.

**MHE. PHILLEMON NDESAMBURO:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri lakini ame-*generalize* kufanya kesi zote za jinai na za *civil* lakini katika swali langu kimsingi nilitaka kujua zile kesi ambazo zina maslahi ya wananchi, ambazo si nyingi sana, zinaweza kuwa kama zile za Wabunge, zinaweza kuwa kama za Valambia, ambaye kesi ilichukua muda mrefu sana mpaka tukaja kulipa mabilioni sasa yanadaiwa. Kwa hiyo, ninachosema mimi ni kwamba, Waziri hajanijibu swali langu la msingi.

**SPIKA:** Kama hivyo ndivyo, basi bora swali litafutiwe muda mwingine baadaye ili liweze kujibiwa kikamilifu zaidi.

*(Hapa Mheshimiwa Dr. Willbrod P. Slaa alisimama kwa ajili ya kuuliza swali la nyongeza)*

**SPIKA:** Sasa Mheshimiwa Dr. Willbrod P. Slaa, swali limeahirishwa, kwa hiyo hakuna nyongeza. Tunaendelea na maswali mengine, swali kwa Wizara ya Kilimo na Chakula, Mheshimiwa Jacob Shibiliti.

Na. 26

**Mradi wa Umwagiliaji - Mbarika**

**MHE. JACOB D. SHIBILITI** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali imeonyesha nia ya kuufufua mradi wa umwagiliaji ulioko Mbarika ambao uliachwa na Waisraeli miaka mingi iliyopita na kwa kuwa Serikali inategemea kuanza na hekta 50 kwanza:-

(a) Je, ni kiasi gani cha fedha kimetumika hadi sasa katika hatua za awali za kuufufua mradi huo?

(b) Je, mradi huo utakamilika lini na utagharimu fedha kiasi gani?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Jacob Dalali Shibiliti, Mbunge wa Misungwi, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Katika hatua za awali za kufufua mradi wa kilimo cha umwagiliaji maji mashambani ulioko Mbarika, shilingi 19,951,875/= zimetumika katika utekelezaji wa kazi zifuatazo: Uchimbaji wa mtaro wenye urefu wa mita 250, ujenzi wa nyumba ya pampu, ujenzi wa kivuko cha ng'ombe, ununuzi na usimikaji wa pampu na ununuzi wa mabomba ya kusambaza maji mashambani pamoja na upimaji wa eneo la shamba na uchunguzi wa udongo.

(b) Mradi wa kilimo cha umwagiliaji maji mashambani wa Mbarika unatarajiwa kukamilika Aprili, 2004. Ukamilishaji wa mradi huo utahusisha kazi zifuatazo: Ununuzi na ufungaji wa viunganishi vya mabomba *(Pipe Fittings)* kati ya pampu ya maji na bomba kuu la kuchukua maji, ununuzi na utandazaji wa mabomba ya mfumo wa umwagiliaji kwa njia ya kunyunyizia maji mashambani *(Sprinkler System),* kufundisha wakulima juu ya uendeshaji wa pampu ya maji na mfumo wa mabomba ya kunyunyizia maji mashambani, kubadilisha mfumo wa umwagiliaji maji mashambani kwenye baadhi ya maeneo ya shamba kutoka umwagiliaji kwa njia ya kunyunyizia na kuweka mfumo wa mifereji na kuongeza bomba linaloingia Ziwani kutokana na kubadilika kwa kina cha Ziwa kunakosababishwa na upepo.

Mradi huo utakapokamilika, utamwagilia hekta 50 na utakuwa umegharimu shilingi milioni thelathini.

**MHE. JACOB D. SHIBILITI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Pamoja na majibu ya Naibu Waziri, ningependa niulize maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa Naibu Waziri amekiri kwamba ni milioni 19 ambazo zimetumika lakini wananchi wa Mbarika wamekuwa na wasiwasi wa shughuli hii jinsi ambavyo imekuwa ikiendeshwa. Je, Waziri atakubaliana na mimi kwamba, kwa vile mradi huu utazinduliwa mwezi huu yuko tayari kuja tukashirikiana naye na akajionea kwa macho? *(Makofi)*

La pili, kwa vile mradi huu ulikuwepo na sehemu nyingine ya Jimbo la Busega sehemu ya Kalemela, je, sehemu hiyo ya Kalemela Magu umefikia hatua gani? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Spika, wasiwasi wa kuendesha shughuli hizi katika swali haukuonyeshwa, sasa nitaushughulikia nikitoka hapa. *(Kicheko)*

La pili, mradi huu wa Kalemela haukuulizwa, nao nitaufuatilia. *(Kicheko/Makofi)*

Na. 27

**Vyama vya Ushirika Nchini**

**MHE. LYDIA T. BOMA** aliuliza:-

Kwa kuwa baada ya Vyama vya Ushirika kukosa uwezo wa kununua mazao tumeshuhudia wafanyabiashara wakinunua mazao ya wakulima hasa ya biashara kama vile korosho huko Mtwara na kwa kuwa ununuzi huo hufanywa chini ya taratibu za soko huria ambapo baadhi ya wafanyabiashara hukwepa kulipa ushuru kwa Vijiji vinavyohusika na hata kwa Halmashauri:-

(a) Je, Serikali inajua kuwa taratibu za soko huria ni tatizo na kama inajua hivyo inachukua hatua zipi za haraka za kukomesha tatizo hilo?

(b) Je, katika karne hii ya 21 nchini Tanzania kuna Vyama vya Ushirika vingapi ambavyo vinahudumia wakulima wake vizuri?

(c) Na kama vipo, je, fedha za kuendeshea biashara ya kununulia mazao vinapata wapi?

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Lydia Boma, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nisikubaliane na Mheshimiwa Mbunge kwamba, mfumo wa soko huru ulianzishwa kwa kuwa Vyama vya Ushirika

vilikosa uwezo wa kununua mazao ya wakulima bali mfumo huo ulianzishwa kufuatia mfumo mzima wa uchumi wa soko ambao Tanzania ilikuwa imeamua kuufuata. Pamoja na hivyo Serikali inajua ya kwamba, katika utekelezaji wa mfumo huo yamejitokeza matatizo kadhaa yanayosababishwa na baadhi ya wanunuzi binafsi kukiuka taratibu zilizowekwa kama vile kuwapunja wakulima kwa kutumia vipimo visivyo rasmi, kutonunua mazao kwenye vituo rasmi vilivyopangwa, kuharibu ubora wa mazao kwa kununua mazao mabichi au machafu pamoja na kukwepa kulipa ushuru kwa mamlaka husika kama vile Vijiji na Halmashauri za Wilaya. Ili kukabiliana na matatizo hayo, Serikali imekuwa ikichukua hatua mbalimbali ikiwa ni pamoja na hizi zifuatazo:-

- Kurekebisha sheria, kanuni na taratibu za ununuzi wa mazao kwa lengo la kuondoa mapungufu yaliyokuwa yamejitokeza;

- Kuimarisha usimamizi wa utekelezaji wa sheria, kanuni na taratibu hizo kwa kuzishirikisha Halmashauri za Wilaya husika;

- Kuhakikisha kuwa ununuzi wa mazao unafanyika kwenye vituo rasmi vilivyotengwa vikiwemo Vyama vya Msingi vya Ushirika;

- Kuhamasisha uanzishwaji wa Vyama vya Ushirika na kuviimarisha viwe imara kwa ajili ya kukabiliana na ushindani katika soko huru; na

- Kupunguza idadi na viwango vya ushuru wa mazao na kodi zilizokuwa zikitozwa na Halmashauri za Wilaya kwa lengo la kupunguza ukwepaji wa kodi na kuwaondolea kero wakulima kwa mfano viwango vya ushuru vilivyopunguzwa ni kutozidi asilimia tano ya bei ya mkulima.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikihimiza uanzishwaji wa Vyama vya Ushirika vya Mazao ili viwahudumie wakulima vizuri. Hadi kufikia tarehe 31 Desemba, 2003 idadi ya Vyama vya Ushirika vya Mazao vilivyoandikishwa kisheria Tanzania Bara vilikuwa 2,416 vikiwemo Vyama 2,371 vya Ushirika vya Msingi na Vyama Vikuu 45. Katika msimu wa 2001/2002 hadi 2003/2004, Vyama Vikuu vya Ushirika kumi vilifanya kazi ya kukusanya mazao ya wakulima kupitia Vyama vyao vya Msingi. Aidha, vipo Vyama vya Ushirika vya Msingi vinavyotoa huduma moja kwa moja kwa wakulima na wanachama wake. Vyama hivi ni pamoja na Vyama vitano vya Mkoa wa Mtwara ambavyo ni Lukuledi, Nakopi, Nangoo, Nanganga na Mpowora. Vyama vingine vitano vya Msingi vipo katika Wilaya ya Mbinga Mkoani Ruvuma ambavyo ni Malindiko, Pilikano, Kimuli, Luwati na Mahenge vinavyohudumia wakulima wa Vyama vingine 50 na katika Mkoa wa Kigoma kuna Chama cha Msingi kimoja cha Kanyovu kinachohudumia Vyama vingine vya msingi vinane.

(c) Mheshimiwa Spika, Vyama vya Ushirika vinapata fedha za kuendeshea biashara ya ununuzi wa mazao kutokana na mikopo ya mabenki baada ya Vyama husika kukidhi masharti yaliyowekwa. Hadi sasa Benki za *CRDB, Exim* na *Kilimanjaro Cooperative Bank (KCB),* zimefanya kazi nzuri ya kukopesha Vyama. Sambamba na hilo, Serikali imeweka utaratibu wa *Export Credit Guarantee Scheme (ECGS)* wa kutoa

dhamana kwa asasi za fedha zitakazokuwa tayari kukopesha Vyama vya Ushirika na Wafanyabiashara binafsi, fedha za kununulia mazao ya wakulima. Chini ya utaratibu huo wa *ECGS,* Benki ya *CRDB* msimu wa 2002/2003, iliidhinisha mikopo ya jumla ya shilingi 11.260bn/= kwa Vyama Vikuu tisa vilivyokidhi masharti ya mikopo. Aidha, Vyama vya Msingi vya Wilaya ya Mbinga Mkoani Ruvuma vya Malindiko, Pilikano, Kimuli, Luwaita na Mahenge pia vilipata mikopo ya jumla ya shilingi 1.69bn/= kutoka katika benki hiyo. Katika msimu huu wa 2003/2004, *CRDB* imeidhinisha mikopo ya shilingi 13.3bn/= kwa Vyama Vikuu vya Ushirika vya *ACU, KNCU, KCU, KDCU, ISAYULA, MBOCU, SHIRECU, NCU, BCU* na *KACU.* Pia Vyama vya Ushirika vya Msingi nilivyokwishavitaja vimeidhinishiwa na benki hiyo mikopo ya jumla ya shilingi 2.2bn/=.

Wizara yangu inaendelea kuwahamasisha wananchi kujiunga kwa wingi kwenye Vyama vya Ushirika, kuongeza mitaji (hisa), kuimarisha uongozi, kuajiri watendaji wenye sifa zinazotakiwa na waadilifu ili viweze kufanya biashara kwa faida na kuweza kuhimili ushindani katika soko huru.

**MHE. LYDIA T. BOMA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri, nina swali moja la nyongeza. Kwa kuwa soko huria ni tatizo ambalo linadhoofisha Vyama vya Ushirika. Je, Serikali inachukua hatua gani za uhakika ili kuimarisha Ushirika kwa vitendo badala ya maneno mazuri? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, anachosema Mheshimiwa Mbunge ni kweli kwamba, katika hizi vurugu zinazofanywa na baadhi ya wafanyabiashara binafsi kusema kweli zinavuruga hata utaratibu wa Vyama vya Ushirika, kwa hiyo, kuonekana kama vinadhoofika. Lakini kama nilivyoeleza katika jibu la msingi kwamba, hatua ambazo tumekwishaanza kuzichukua ni pamoja na kuviimarisha hivi Vyama katika hatua mbalimbali. Kwa mfano, hivi sasa tumetunga hii Sheria Mpya ya Ushirika ambayo imetoa maelekezo ya waziwazi ya kuhakikisha kwamba, wanachama wenyewe wanaanzisha Vyama vyao vya Msingi kwa matakwa yao na vile vile suala zima la kuwaelimisha wanachama ili waweze kuvisimamia Vyama vyao wenyewe. Lakini vile vile Serikali sasa hivi inaandaa utaratibu wa mageuzi katika ushirika *(Cooperative Reforms),* ambayo nia yake ni kuimarisha ushirika nchini.

**MHE. ABDILLAHI O. NAMKULALA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwa kuwa wanunuzi wa korosho wanapokwenda kununua korosho wanakwenda na bei ndogo na wakulima hulazimika kuchukua bei ile kwa sababu hawana pa kukimbilia. Je, Serikali ina mkakati wa karibu wa kuhakikisha Vyama vya Msingi vina uwezo wa kununua korosho ili kushindana na wanunuzi hawa wanaoleta bei ndogo kwa msimu wa mwaka huu? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, nimesema hapa kwamba, katika utaratibu wa soko huria baadhi ya wafanyabiashara binafsi wanakiuka taratibu zilizowekwa ikiwa ni pamoja na hilo la kuwapunja wakulima kuwapa bei ndogo. Sasa nilichosema katika jibu la msingi vile vile na hata katika jibu la nyongeza hapa nimesema kwamba, Serikali sasa hivi inaimarisha Vyama vya Ushirika ili

viweze kusimamia mazao hayo ya wakulima ikiwemo na korosho. Vile vile nimetoa maelezo hapa kwamba, Vyama vya Msingi vitano vya Mtwara vimeshaanza kufanya kazi hii nzuri. Kwa hiyo, nataka niseme tu kwamba, hiyo kazi ya kusimamia ununuzi wa mazao kupitia Vyama vya Ushirika Serikali inajizatiti na ndicho tunachofanya hivi sasa.

Na. 28

**Mkutano wa Wafadhili Uliofanyika Mwaka 1996**

**MHE. BEATUS R. MAGAYANE** aliuliza:-

Kwa kuwa mwaka 1996 uliitishwa Mkutano wa Wafadhili *(Donors Conference)* kwa lengo la kuchangia maendeleo ya Kigoma kwa kutambua kule kuathirika kwa Mkoa huo kwa sababu ya wakimbizi:-

(a) Je, ni kiasi gani cha fedha kilitumika kuandaa mkutano huo?

(b) Je, ni kiasi gani halisi kilitolewa na kila mchangiaji ikilinganishwa na ahadi zilizokuwa zimetolewa na kila mchangiaji?

(c) Je, fedha hizo au misaada hiyo ilitumika vipi na ni nani alitoa vipaumbele vya matumizi hayo?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Beatus Magayane, Mbunge wa Buyungu, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, mnamo mwaka 1996, Ofisi ya Waziri Mkuu ikishirikiana na Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa *(UNDP),* iliandaa mkutano wa wafadhili kwa ajili ya kuchangia maendeleo ya Mkoa wa Kigoma kutokana na athari zilizotokana na wakimbizi. Mkutano huo ulifanyika tarehe 12 Februari, 1996. Pamoja na kuwa Serikali kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu, ilishiriki kuandaa mkutano huo, gharama zote ziligharamiwa na *UNDP.* Kwa hiyo, *UNDP* ndio wanafahamu kiwango cha fedha kilichotumika katika maandalizi ya mkutano huo.

(b) Mheshimiwa Spika, kiasi cha fedha kilichotolewa na kila mfadhili ni kama ifuatavyo: Denmark waliahidi kuchangia shilingi 500m/= za Tanzania, walitoa shilingi 76.7m/= ambayo ni sawasawa na asilimia kumi na tano ya ahadi yao, Finland waliahidi Dola za Kimarekani 650,000, lakini hawakuchangia yaani ilikuwa ni *zero percent,* Ireland waliahidi dola za Kimarekani 258.020, walitoa dola za Kimarekani 199,000, sawasawa na asilimia sabini na saba ya ahadi yao, Japan waliahidi Dola za Kimarekani 187,970 na walitoa zote yaani *hundred percent, UNDP* waliahidi dola za Kimarekani 2.02m, walitoa dola 856,983 ambayo ni asilimia 34 ya kile walichoahidi, *European Union* waliahidi *Euro* 7m na walitoa zote, *hundred percent*, *USAID* waliahidi Dola za Kimarekani milioni mbili na walitoa zote, Austria waliahidi kutoa Shilingi za Tanzania

410m/= na walitoa zote, Ujerumani waliahidi Dola za Kimarekani 2m na walitoa zote na Shirika la Afya Duniani waliahidi kutoa Dola za Kimarekani laki moja na walitoa zote. *(Makofi)*

(c) Mheshimiwa Spika, fedha zilizochangwa zilitumika kwa shughuli mbalimbali Mkoani Kigoma kama ifuatavyo: Kuhuisha mazingira, ukarabati wa shule za msingi, ukarabati wa vituo vya afya, kuimarisha utendaji *(Capacity Building),* uanzishwaji wa miradi ya kuondoa umaskini na ukarabati wa barabara ya Nyakanazi - Kigoma. Aidha, matumizi mengi ya fedha hizo ni pamoja na ukarabati wa maeneo korofi ya barabara ya Nyakanazi - Kigoma, Miradi ya Maendeleo Vijijini katika Wilaya ya Kasulu, ukarabati wa barabara ya Kibirizi hadi Gungu, uhuishaji mazingira ndani ya makambi na maeneo jirani, ununuzi wa magari kwa ajili ya Taasisi za Serikali zilizohusika na utawala wa wakimbizi pamoja na utunzaji na usambazaji wa madawa muhimu.

Mheshimiwa Spika, aidha, miradi hiyo ilitekelezwa kutokana na vipaumbele vilivyopendekezwa na viongozi wa Mkoa wa Kigoma na Wilaya husika kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu.

**MHE. BEATUS R. MAGAYANE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru na namshukuru Naibu Waziri kwa majibu aliyoyatoa, lakini nina maswali mawili madogo ya nyongeza. Kwa kuwa kumekuwa na tabia kwa watu na taasisi zikiwemo za Kimataifa kama tulivyosikia, kutoa ahadi ambazo baadaye hawazitekelezi. Je, Serikali inajifunza nini inapokuwa inapanga mipango yake inapokuwa inategemea watu wa kutoka nje wanaotoa ahadi zisizotekelezeka? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili, kwa kuwa lengo la kutafuta pesa hizi lilikuwa ni kukarabati miundombinu ya maji, madarasa na zahanati katika Vijiji mbalimbali kwa mfano, vya Lumashi, Kiga, Kasuka, Kasongati, Kaselamahindwa na Bukiriro katika Jimbo la Buyungu na hizo pesa hazikufika. Je, Serikali inasema nini, kwa nini hazikuweza kupelekwa huko ambako awali zilikuwa zimekusudiwa kwenda? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, la kwanza, ni kweli kama nilivyosema katika jibu langu la msingi, kuna baadhi ya wafadhili huwa wanatoa ahadi halafu hawatekelezi. Sasa mwuliza swali anasema katika hali hii Serikali inasemaje? Kwanza, mtu akitoa ahadi ni hiari yake, anatoa ahadi kwa hiari, kwa hiyo, ana hiari ya kukutimizia ama kutokutimizia na huwezi kumpeleka Mahakamani kwa sababu ni msaada. Lakini kubwa tulilojifunza ni suala ambalo Rais wetu, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, amekuwa akilisisitiza la kujitegemea na siyo Rais Mkapa tu hata Marais waliopita, mfano, Baba wa Taifa, amelisemea sana suala la kujitegemea na kwa kweli ndiyo jawabu kubwa kabisa kuliko kutegemea ahadi za wahisani na ambazo wakati mwingine hawazitekelezi.

Mheshimiwa Spika, la pili, amesema kuna baadhi ya Vijiji fedha hizi hazikufika. Sasa kama nilivyojibu katika jibu langu la msingi kwamba, waliokuwa wanapanga matumizi ya fedha hizi siyo sisi Wizara ya Mambo ya Ndani, zilikuwa zinapangwa na

Mkoa wa Kigoma na Wilaya zinazohusika nadhani ni pamoja naye na kama siyo yeye ni Mbunge mwenzake aliyekuwepo wakati huo, kupitia Halmashauri, ndiyo walikuwa wanapanga. Sasa kama hazikufika kwa kweli ni bahati mbaya sana, lakini kwa bahati Mkoa wa Kigoma umepata mradi mwingine unaofadhiliwa na Denmark wenye shilingi 8.9bn/=, karibu bilioni tisa. Fedha hizi moja ya maeneo ambayo zimeruhusiwa kutumika ni katika miradi ya maji. Kwa hiyo, sasa namwomba Mheshimiwa Mbunge, kama nafasi ile iliponyoka sasa nafasi hii ya pili isiponyoke, ashirikiane na Halmashauri na Viongozi wa Mkoa ili Vijiji hivyo vipate miradi ya maji.

Na. 29

**Mzozo wa Ardhi Kijiji cha Ngalole na Gereza la Namajani**

**MHE. RAYNALD A. MROPE** aliuliza:-

Kwa kuwa kutokana na kuzuka kwa mzozo wa ardhi kati ya Kijiji cha Ngalole, Kata ya Namajani Wilaya ya Masasi na Gereza la Kilimo la Namajani na kwa kuwa ng'ombe wa Magereza wanaleta uharibifu mkubwa katika mashamba ya wananchi:-

(a) Je, Serikali inatoa kauli gani kuhusu hali mbaya ya mgogoro huo ambao unaweza kutishia amani katika eneo hili endapo suluhisho la haraka halitapatikana?

(b) Je, kwa nini Gereza la Namajani hawataki kuzingatia mipaka halisi ya Kijiji cha Ngalole ambayo inatambulika kisheria ili kuepusha mgongano na kiini cha mzozo huo?

(c) Je, Serikali itafidia Kaya sita za Kijiji cha Ngalole ambazo zimeathirika kutokana na mazao yao kuharibiwa na ng'ombe wa Gereza hilo?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Raynald Mrope, Mbunge wa Masasi, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, miaka ya nyuma kulikuwa na mzozo wa kugombea ardhi kati ya Gereza la Namajani na wanavijiji wanaopakana kikiwemo Kijiji cha Ngalole. Katika jitihada za kumaliza mzozo huo, tarehe 12 Desemba, 1998 Mkuu wa Wilaya ya Masasi aliitisha kikao cha pamoja kati ya Uongozi wa Magereza na Viongozi wa Vijiji vinavyopakana na Gereza ambavyo ni Amani, Chiroro, Ngalole, Mjiwale na Namatutwe. Baada ya kikao hicho muafaka wa mipaka ya Gereza na Vijiji hivyo ulipatikana. Hata hivyo, pamoja na muafaka huo, wanakijiji wachache wa Ngalole hawakuridhika, hivyo waliendeleza msuguano.

Katika jitihada za kumaliza mzozo tarehe 23 Februari, 2002, Mkuu wa Wilaya ya Masasi aliitisha kikao kingine kilichojumuisha Viongozi na Watendaji mbalimbali wa Kijiji cha Ngalole, ambao baada ya kujadili kwa kina walikubaliana kwamba, uamuzi wa

awali wa mwaka 1998 ulikuwa sahihi na hivyo mipaka ya Gereza ikabaki kama ilivyokubaliwa 1998.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa hivi mgogoro wa ardhi kati ya Gereza la Namajani na Vijiji inavyopakana navyo umekwisha. Gereza linaendelea kuheshimu mipaka ya ardhi yake na kuepusha mzozo na uhasama unaoweza kutokea kati yake na Vijiji inavyopakana navyo.

Aidha, Serikali haina taarifa yoyote ya uharibifu wa mazao ya kaya sita za Kijiji cha Ngalole uliofanywa na ng'ombe wa Magereza na iwapo utapatikana uthibitisho wa taarifa za uharibifu huo, Serikali haitasita kulishughulikia tatizo hilo ipasavyo.

**MHE. RAYNALD A. MROPE:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Ninamshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa majibu yake. Lakini nataka kuuliza kwamba kwa nini Magereza mara kwa mara haiwatendei haki wananchi, mimi nina ushahidi wa kulisha ng'ombe wa magereza katika mashamba ya wananchi kwa sababu eti wao wanalima katika maeneo yao?

La pili, ni kwa nini mizozo mingi ya ardhi inayotokea katika nchi hii ni katika maeneo ya Magereza hasa kwa mfano, wenzetu wa Musoma na kadhalika na mara nyingi mizozo hii inakuwa ya kibabe, hivi Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba Magereza wanaishi kwa usalama na wenzao katika sehemu zile?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, kwanza kama Mheshimiwa Mbunge anao uthibitisho wa ng'ombe wa Magereza kuvuka mipaka ya Magereza na kwenda kula mazao ya wananchi kwa kweli atuletee. Kwa sababu ni makosa kwa ng'ombe wa Magereza kuvuka katika eneo lao na kwenda vijijini kwenda kula mazao. Kama uthibitisho upo naomba atuletee ili tuweze kulishughulikia tatizo hilo.

La pili, kuhusu mizozo kati ya Magereza na wanavijiji, ni kweli mizozo hii imekuwepo hapa na pale. Japo Mheshimiwa Mbunge anasema imekuwa ya kibabe lakini siyo ya kibabe, kila inapotokea tunaishughulikia mpaka tunapata muafaka kama ilivyotokea kule Masasi, mzozo ule ulishughulikiwa vizuri na *DC* na kwingineko kote ambapo mizozo hii imetokea kwa kweli imeshughulikiwa vizuri, kistaarabu na kiungwana bila kuwa na ubabe. Lakini ili kumaliza hii mizozo sasa tumeamua kwamba maeneo ya Magereza yote nchini sasa yatapimwa, mipaka itawekwa rasmi na watapata hati ili utaratibu wa sasa wa maeneo ya Magereza kuvamiwavamiwa uweze kukomeshwa na mizozo itakuwa imekwisha.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali yamekwisha na muda wa maswali pia umekwisha. Kuna matangazo mawili tu kabla hatujaendelea ya vikao. Tangazo la kwanza, Kamati ya Fedha na Uchumi, Mwenyekiti wa Kamati hiyo anawatangazia

Wajumbe wake kuwa leo saa tano kutafanyika kikao cha Kamati yake katika Ukumbi Namba 227.

*Chief Whip* wa Upinzani, anawatangazia Waheshimiwa Wabunge wote wa Upinzani kwamba, leo mchana baada ya kuahirisha Bunge ile saa saba kutakuwa na Mkutano wa Waheshimiwa Wabunge wote wa Upinzani kwenye ofisi zilizopo katika ghorofa ya pili. Mwisho wa matangazo. Tunaendelea na *Order Paper.*

## MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

### Muswada wa Sheria ya Ajira na Mahusiano katika Kazi wa Mwaka 2003 *(The Employment and Labour Relations Bill, 2003)*

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**MHE. SOPHIA M. SIMBA - MWENYEKITI WA KAMATI YA MAENDELEO YA JAMII:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii kutoa maoni ya Kamati ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii kuhusu Muswada wa Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini ya 2003 *(The Employment and Labour Relations Bill 2003).*

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kuchukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Balozi Getrude Ibengwe Mongella, kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Kwanza wa Bunge la Afrika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kabla sijawasilisha maoni ya Kamati yangu juu ya Muswada wa Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini *(The Employment and Labour Relations Bill, 2003),* kwa mujibu wa Kanuni Namba 70(2), Kanuni za Bunge, Toleo la 2004, napenda nieleze kwa kifupi hatua iliyotangulia kabla ya Kamati kufikiria Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipata fursa ya kuhudhuria Semina iliyoandaliwa na Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo, kwa kushirikiana na Shirika la Kazi la Dunia *(ILO).* Semina hiyo ilifanyika Morogoro tarehe 30 - 31 Oktoba, 2003. Semina hiyo ilihudhuriwa pia na wadau mbalimbali ambao waliweza kutoa maoni yao ambayo mengi yamezingatiwa na Serikali. Napenda kuipongeza Serikali kwa utaratibu huu wa kuwashirikisha Kamati pamoja na wadau mapema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha, chini ya utaratibu wa *Public Hearing,* unaowezesha watu mbalimbali kuhudhuria Vikao vya Kamati za Bunge na kutoa maoni yao, tarehe 6 - 7 Aprili, 2004 Kamati yangu ilikutana na kupokea maoni ya wadau mbalimbali wa Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, wadau walioshiriki katika Muswada huu ni wawakilishi kutoka *TUCTA, ILO, DOLASED, TALGWU, TPAWU, CHODAWU, RAAWU, TASU, TUICO, TAMCO, CUT, SUNY/PACT, TUGHE, TRAWU, COTWU, ATE, LHRC, NSSF, University of Dar es Salaam* na *TLS.*

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu inawapongeza wadau hao kwa umakini waliouonyesha katika kuchambua Muswada huu kwani maoni yao kwa kiasi kikubwa yameisaidia Kamati katika kukamilisha kazi hii.

Mheshimiwa Spika, nikianza na maoni ya jumla kuhusu Muswada huu, Kamati yangu inaunga mkono na inakubaliana na Serikali kuwa Muswada huu umeletwa kwa wakati muafaka kabisa kwa sababu unalenga kurekebisha Sheria ya Ajira iliyopo sasa ambayo imeonekana kuwa na mapungufu mengi.

Mheshimiwa Spika, lingine la jumla ni kwamba, Kamati inashauri kuwa masuala ya msaada wa matibabu na maziko kwa mfanyakazi yaendelee kutolewa kama Sheria ya zamani inavyosema.

Mheshimiwa Spika, katika sehemu ya tatu ya Muswada kifungu cha 14(1) Kamati iliona kuwa tafsiri ya neno lililotumika kuonyesha aina za mikataba, yaani *"forms"* lifutwe na badala yake liwekwe *"types."*

Kamati yangu imekubaliana na Serikali kuwa kifungu cha 22(1) kinachomzungumzia mwajiri kutomtaka mfanyakazi kufanya kazi wakati wa siku za mapumziko mpaka mfanyakazi awe ameridhika mwenyewe kufanya hivyo kiondolewe. Hii ni kutokana na unyeti wa baadhi ya kazi.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 37(3)(d) kinachozungumzia sababu ambazo hazitakiwi kuchukuliwa kama sababu ya kumfukuza mfanyakazi, Kamati ilishauri kuwa katika sababu mbili zilizotolewa iongezwe ya tatu itakayosomeka kwa misingi ya ulemavu *(Related to Disability).* Aidha, katika kifungu hicho hicho cha 37 ili kumtendea haki mfanyakazi na ili asiadhibiwe mara mbili kiongezwe kifungu cha (5) kitakachosomeka: *"No disciplinary action in form of penalty, termination or dismissal shall lie for an employee who has been charged with criminal offence which is substantially the same until final determination by the Court and any appeal thereof."*

Mheshimiwa Spika, katika kifungu cha 38(c)(v) Kamati inashauri liongezeke neno *"or redundacy"* pale mwishoni mwa neno *"retrenchments."*

Mheshimiwa Spika, katika kifungu cha 54(c) mstari wa pili, Kamati inashauri yaongezwe maneno *"to form a confederation."*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa sehemu ya tano ya Muswada, Kamati inashauri kuwa katika kifungu cha 60(3) maneno ya mstari wa mwisho ambayo yanasomeka: *"where the employees the union represents are employed"* yaondolewe. Aidha, katika kifungu cha 61(3) mstari wa pili, baada ya maneno *"sub-section two",* Kamati inashauri yaongezwe maneno *"and without reasonable ground."*

Mheshimiwa Spika, katika sehemu ya tano, Kamati inatoa maoni ya jumla kuwa neno *"most representative"* liondolewe na badala yake litumike neno *"Registered Trade Union."*

Aidha, katika kifungu cha 102(5) katika mstari wa pili, Kamati inashauri neno *"Industrial Court"* liondolewe badala yake liwekwe neno *High Court.*

Mheshimiwa Spika, kama nilivyotamka awali, ushauri wetu kwa kiasi kikubwa umezingatiwa na Serikali. Ni matumaini yangu kuwa yale ambayo sikuyagusia, Wajumbe wa Kamati hii na Waheshimiwa Wabunge watachangia watakapopata fursa.

Mheshimiwa Spika, mwisho napenda nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuwasilisha maoni ya Kamati. Pia napenda kuchukua fursa kumshukuru Mheshimiwa Prof. Alhaji Juma Kapuya, Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo, Naibu Waziri, Mheshimiwa Mudhihir Mudhihir, Katibu Mkuu wa Wizara, Bwana Abubakar Rajab, Kamishna wa Kazi, Bibi Regina Rweyemamu, Wawakilishi kutoka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu na Wataalam wote walioshirikiana nao kwa maelezo ya kina na ufafanuzi waliotoa mbele ya Kamati.

Aidha, nawashukuru wadau wote waliotoa maoni yao mbele ya Kamati, ambayo yamesaidia sana kuboresha Muswada huu. Kwa namna ya kipekee, nawashukuru sana Wajumbe wa Kamati yangu kwa kushiriki kikamilifu katika vikao na kutoa michango ya kina ambayo imewezesha Muswada huu kuwa katika sura ionekanayo sasa tofauti na ile ilivyokuwa awali. Naomba kuwatambua kwa kutaja majina kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Sophia Simba, Mwenyekiti, Mheshimiwa Haroub Said Masoud, Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Teddy Kasella-Bantu, Mheshimiwa Zuhura Shamis Abdallah, Mheshimiwa Jina Khatib Haji, Mheshimiwa Mwanaidi Hassan Makame, Mheshimiwa Yussuf Kombo Juma, Mheshimiwa Kijakazi Khamis Ali, Mheshimiwa Mchande Salim Mchande, Mheshimiwa Omar Mohammed Mwenda, Mheshimiwa Yahya Kassim Issa, Mheshimiwa Khalifa Mohammed Issa, Mheshimiwa Ramadhani Nyonje Pandu, Mheshimiwa Bakari Muhema Mbonde, Mheshimiwa Janeth Edward Mashele, Mheshimiwa Cynthia Hilda Ngoye, Mheshimiwa Kisyeri Chambiri na Mheshimiwa Ponsiano Nyami.

Aidha, napenda kumpongeza Katibu wa Kamati hii, Bibi Angelina Sanga, kwa kuihudumia vyema Kamati na kutayarisha maoni kwa wakati muafaka.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii na naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MHE. KHALIFA MOHAMMED ISSA - MSEMAJI MKUU WA UPINZANI KWA WIZARA YA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa kuniita ili niweze kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani, kuhusu Muswada wa Sheria ya *Employment and Labour Relations Bill, 2003* kwa mujibu wa Kanuni za Bunge kifungu cha 43(5)(b)(c) Toleo la 2003.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kutanguliza kusema kwamba, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, hatutapinga kupitishwa kwa Muswada huo wa Sheria. Lakini kutokupinga huku haina maana kuwa Muswada huu hauna mapungufu, ni kutokana na mapungufu ambayo Kambi ya Upinzani imebaini, hivyo inatoa maoni na mapendekezo ili kuuboresha Muswada huu ambao walipa kodi wakubwa wa Taifa hili unawahusu ili uweze kukidhi haja na matarajio yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 15(1)(b) ambapo mwajiriwa anapoanza kazi anatakiwa kutoa maelezo binafsi kwa maandishi, kati ya hayo ni *place of recruitment.* Mara zote taarifa za kwanza ndizo zitumikazo kwenye malipo wakati Mkataba unapositishwa, hivyo basi kuondoa mtafaruku na kupunguza uwezekano wa watu wengi wasio na ajira kujaa mijini ni bora neno *"place of domicile"* litumike badala ya *"place of rectruitment"* kama ikitokea usitishwaji wa ajira mtu arudishwe kule alikozaliwa badala ya anuani ya pale alipoombea kazi.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 40(3) cha Muswada huu wa Sheria pale mwajiri anapoamriwa na Mahakama kumrudisha mfanyakazi kazini na yeye kukataa. Sheria inasema alipwe mafao ya miezi 12, kitu ambacho ni kidogo mno na inatakiwa apewe kitu cha kumshtua kuhusu sheria. Hivyo, mafao ya mwaka mmoja ni madogo mno kiasi cha kuweza kuleta matatizo. Kwa hiyo, sisi tunapendekeza mafao ya kuanzia miezi 18 ni muafaka zaidi badala ya miezi 12 kama ilivyo ndani ya Muswada.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 42(1) kinachosema ninanukuu: *"For the purposes of this Section Severance pay mean amount at least equal to 7 days basic wage for each completed year of continuous service with that employer up to a maximum of ten years".* Kwa maoni ya Kambi, kipengele hiki kwa kiasi fulani hakimpi haki mtumishi ambaye amemtumikia mwajiri wake kwa muda mrefu kama miaka 20. Sasa Muswada unasisitiza kuwa malipo yafanyike kwa kiwango cha juu cha miaka 10, hii inampa mwanya mwajiri kulipa *at the minimum* ambayo ataona kwake ina manufaa. Tunamshauri Mheshimiwa Waziri kifungu hiki cha Sheria kifanyiwe marekebisho.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 42(2)(b), kipindi cha miezi 12 kwenye ajira ndipo mwajiriwa apate haki ya *"Severance Pay".* Maana yake kipindi cha uangalizi *(Probation Period).* Kati ya hiyo miezi 12 hakimo. Lakini ili sheria hii iwe wazi, kama mwajiri amesitisha mkataba na mwajiriwa, na ikiwa jumla ya miezi yake ya uangalizi na ajira halisi imetimia mwaka ni bora apigiwe hesabu ya mwaka na watoe miezi ya kipindi cha uangalizi na miezi iliyobaki alipwe *"Severance Pay".*

Kwa misingi hii sheria itakuwa haina ubaguzi kwenye waajiriwa. Kambi ya Upinzani inamwomba Mheshimiwa Waziri na Bunge kwa ujumla kabla ya kupitisha Muswada huu kuwa Sheria, mambo haya yafanyiwe kazi kwa manufaa ya Watanzania wote kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 42(3)(b) mfanyakazi mwajiriwa kukataliwa kulipwa *severance pay* kwa sababu ya kukataa kazi kwa mwajiri mwingine *(any other*

*employer),* Kambi ya Upinzani inaliona hili kama kumnyima mwajiriwa haki ya uhuru wa kuchagua. Kitendo cha Mwajiriwa kutumia haki yake ya msingi ya wapi afanye kazi na katika mazingira yapi, hakiwezi kumsababishia yeye kunyimwa haki yake ya kisheria, kwa misingi kuwa uhamisho wa kutoka kwa mwajiri mmoja kwenda kwa mwingine ni hiari ya mwajiriwa na siyo lazima. Hivyo, kama mwajiriwa hataki cha msingi ni kumpa mafao yake yote ya kisheria na kuacha ajira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hali ya kawaida mtu hawezi kubadilishwa kama bidhaa toka sehemu moja kwenda nyingine kwa maslahi ya mtu mwingine bila ya kukubaliana na mikataba mipya kati yake na huyo mwajiri mpya na hiyo ni hiari na sio lazima. Hivyo, kama sheria itaendelea kusomeka kama ilivyo, basi tunashauri maneno *"any other employer"*, yafutwe kwenye kifungu hiki cha Sheria.

Mheshimiwa Spika kifungu cha 72(2)(d) na (e) kinachosema michango ya wanachama na wasiokuwa wanachama wa Chama cha Wafanyakazi iwekwe kwenye akaunti mbili tofauti, lakini zote zikiwa chini ya Chama cha Wafanyakazi. Kwanza, ninadhani kulingana na Sheria hii basi kila sehemu ambayo kuna idadi ya uwiano wa robo tatu kwa robo moja kufunguliwe akaunti hizo. Sasa ni akaunti ngapi zitafunguliwa nchi nzima? Halafu kitu kingine kuna fedha za wasio wanachama zitumike pale tu ambapo zitashughulikia masuala ya ustawi na marupurupu ya ajira kwa wafanyakazi ndani ya sehemu hiyo ya kazi, mfano, kama ni *TBL* basi iwe ni *TBL* pekee na yasihusishwe matatizo ya aina hiyo na *Serengeti Breweries* au *Cocacola* au Bandari.

Kwa kuanzia Vyama vya Wafanyakazi huwa vimegawanyika kutokana na Sekta husika na matatizo huwa yanashughulikiwa kisekta vilevile, kwa hiyo, kuleta suala la kila tatizo la kila sehemu au Shirika/Kampuni kutaka lishughulikiwe tatizo lake kivyakevyake, hii ni mbinu ya kukigawa Chama na kudhoofisha utendaji wake na kuleta malumbano miongoni mwa wanachama yasiyokuwa ya lazima.

Kambi ya Upinzani inashauri na kusisitiza kuwa akaunti mbili kama kifungu 72(2)(d) kinavyosema, kiangaliwe upya na kifungu cha (e) kinachosisitiza *"in that workplace"* kiondolewe vinginevyo mwajiri anaweza kukataa kuidhinisha makato ya wale wasio wanachama kwa kudai kuwa wafanyakazi wake hawana manung'uniko na malalamiko kulingana na maslahi yao na utendaji wake kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili nichangie kwenye Muswada huu mpya wa Kazi ambao umeletwa hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, kwanza, niipongeze Serikali kwa kuona umuhimu wa kuleta Muswada huu mpya ili kufuta ile Miswada ya zamani ambayo ilishapitwa na wakati. Muswada mpya ni kama zawadi kwa wafanyakazi wetu ambao ndiyo walipa kodi, kodi inayoendesha Serikali hii, hupiga kura nyakati za uchaguzi na wafanyakazi ndiyo wanaolinda amani hapa kwetu.

Mheshimiwa Spika, kufuatana na mabadiliko ya uchumi, sasa hivi inaonyesha mfanyakazi anaelemewa sana na matatizo kuliko mwajiri, kwa hiyo sheria hii itasaidia kuondoa tofauti hizo.

Mheshimiwa Spika, tatizo moja tulilonalo sasa hivi wafanyakazi wengi walikuwa wanafanyakazi bila Mikataba ya Kazi. Mimi nina imani kabisa kwamba, sheria hii imezingatia hayo yote na hii imeonyeshwa na utafiti uliofanywa ni zaidi ya asilimia 40 ya wafanyakazi wanafanya kazi bila Mikataba na hasa kwenye haya Mashirika ambayo yameingia kwenye Migodi, Mahoteli ya Kitalii, Kampuni za Uwindaji, kampuni za kusafirisha utalii na zingine nyingi.

Mheshimiwa Spika, inasikitisha sana kuona kwamba wawekezaji hawa wengi wao wanatokea Afrika ya Kusini, lakini kule Afrika Kusini Vyama vya Wafanyakazi vina nguvu sana, wanatetea sana maslahi yao. Kwa hiyo na mimi ningeviomba Vyama vya Wafanyakazi hapa chini kwetu viendelee kutetea zaidi maslahi ya wafanyakazi wote.

Mheshimiwa Spika, naomba izingatiwe kwamba, wafanyakazi ni sehemu ya Jimbo la sisi wanasiasa, lakini mpaka sasa wafanyakazi wetu bado hawaridhiki na haya wanayotendewa na mpaka sasa wanauliza Serikali mbona imewasahau? Kwa hiyo, mimi naiomba Serikali kupitia hii sheria mpya iliyoletwa Bungeni na ambayo nina uhakika tutaipitisha, iwakumbuke wafanyakazi wake. Wafanyakazi wako Serikalini, wapo kwenye viwanda na wapo katika maeneo mbalimbali hata wale wa majumbani ni wafanyakazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wafanyakazi wana haki ya kudai maslahi yao kwa njia nyingi. Kwa njia ya mazungumzo ya ana kwa ana, kwa njia ya kuandika, hata wanapoandamana au wanapogoma, kwa kweli wanakuwa wanadai haki yao. Kwa hiyo, mimi ningeiomba Serikali mambo haya yanapotokea, isiwakate mshahara kwa sababu ni njia ya kudai maslahi yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sheria hii baada ya kuisoma nimeona kwamba itatoa tofauti zilizopo. Sasa hivi kama Mashirika ya kigeni kwanza mengi yanaajiri watu kutoka nje na wakati Watanzania wapo, inaajiri hata walinzi wanatoka nje kuja kulinda hapa, watu wetu wanabaki hawana kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tuna wasomi wengi sana hapa nchini ambao wakitoka hapa wakienda nchi za nje wanagombaniwa, lakini hapa hawapati ajira kwenye haya makampuni ya kigeni na hata wakipata ajira wanalipwa tofauti na wale waliotoka nje na wengine wanakuwa hata hawana elimu ya kutosha kama hawa waliopo hapa kwetu. Kwa hiyo, mimi naiomba sana Serikali izingatie hayo. Sasa hivi Tanzania watu wetu wengi sana wako nje baada ya kutokuridhika na maslahi yaliyoko hapa au baada ya kutokuajiriwa na haya makampuni ya kigeni ambayo yapo mengi sana. Kwa hiyo, mimi naiomba Serikali iweke masharti ya kutoa ajira kwa wataalam wetu na hata hawa walinzi na watu wengine. Kwa sababu sasa hivi kwa upande wa walinzi kuna Kampuni nyingi

sana za ulinzi na zinafanya vizuri na nyingine zinamilikiwa na watu kutoka nje. Kwa hiyo, hizo Kampuni zikipewa nafasi ya kushiriki kwenye migodi na kwenye kampuni zingine, Watanzania wengi watapata ajira.

Mheshimiwa Spika, mimi naomba kupitia sheria hii, maslahi ya watumishi wetu yarekebishwe. Sasa hivi tupo kwenye dunia ya utandawazi, tuko kwenye soko huria, kwa hiyo, wafanyakazi wetu wanapofanya kazi wafikiriwe kulipwa viwango vinavyolingana na kazi wanazofanya. Wafanyakazi wengi wanafanya kazi zaidi ya saa zinazotakiwa. Kuna wengine wanafanya mpaka usiku lakini hawalipwi *over time.* Kwa hiyo, mimi nitashukuru sana kama Serikali itazingatia hilo.

Mheshimiwa Spika, Wizara yetu ya Kazi inaongozwa na watu mahiri. Mheshimiwa Waziri Kapuya, ameshiriki kwenye migogoro mingi ya kwenye Mabenki na mambo mengine, sasa hebu huo ufanisi anaoufanya uwasaidie na wafanyakazi walioko Serikalini na kwenye sekta binafsi. Sasa hivi Serikali inaongeza kima cha chini lakini kule kwingine hawaongezi. Kwa hiyo, mimi nashukuru sana kuleta hii sheria kwa wakati unaotakiwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo na mimi naunga mkono hoja mia kwa mia. Nashukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili nichangie mawazo katika Muswada huu wa *Employment and Labour Relations Bill.*

Mheshimiwa Spika, napenda niwapongeze Mheshimiwa Waziri, Wizara yake na Kamati ambayo imechambua Muswada huu, kwa kazi nzuri ambayo wameifanya. Kwa kweli Muswada huu umekuja wakati muafaka ili kubadilisha hali ya ajira iliyokuwepo katika uchumi hodhi na sasa kurekebisha ajira katika soko huria, ikilenga kwamba sasa waajiri watakuwa ni wawekezaji wa nje au hata wakiwa wawekezaji wa ndani lakini ni watu ambao wanafikiria sana faida na maslahi yao kwenye soko. Lakini pia ajira hii ni vyema ikaangaliwa na kudhibitiwa vizuri ili kuzuia ukoloni usije ukanyemelea nchi kupitia kwenye ajira hii. Kwa hiyo, Muswada huu lazima uwe na *safeguards* ili uweze kuwalinda waajiriwa wa Tanzania na kuilinda Tanzania jinsi tunavyokwenda kwenye soko hili huria.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi nitaongelea kitu kimoja tu kuhusu ile sehemu ya (ii) ya Muswada huu inayohusu *Fundamental Rights and Protections* na nitaongea kitu kidogo kabisa *sub-part (c)* sehemu ya 7(4)b katika eneo la ubaguzi. Kila nchi inapokubali uwekezaji inataka pamoja na kuwekeza, wananchi wake wapate kazi. Kwa hiyo, hatuwezi kuwa na sheria ambayo inasema hatutabagua wananchi wa nchi za nje katika kutoa kazi.

Ni lazima kama nchi tulinde kazi ambazo zinapatikana nchini kwetu kama vile kuku anavyolinda watoto wake. Haiwezekani kuwaachia bomba la ajira, eti mtu wa nchi yoyote tu anaweza kupewa kazi, haiwezekani. Kwa hiyo, katika *discrimination* sehemu

ya 7, sehemu ndogo ya 4(b) ile lazima ifutwe. Lazima tuwalete wageni kufanya kazi hapa kama wageni hao wanahitajika. Kama utaalamu wao unahitajika. Lakini sio kila mtu ana haki ya kupewa kazi Tanzania. *(Makofi)*

Pili, kuna sehemu ya 7(c) inayosema: *"discriminations on the grounds of tribe or place of origin".* Mimi ningependa tuseme *tribe or place of origin in Tanzania. It must be very specific.* Maana yake mtu mwingine mwenye *tribe* yake anatoka *Republic* ya kigeni huko nje. Hatuwezi kumjali, tuna kazi naye gani, katika sheria hii. Kwa mfano, kama wale walinzi waliosemwa hapa kutoka Nepal. *It is absolutely absurd* kwamba, tunaweza kuleta mlinzi wa bunduki alinde kitu hapa Tanzania kutoka Nepal. *It is unacceptable and it is something we cannot accept.* Haiwezekani.

Si suala tu kwamba tupewe maelezo, ni suala la *visa* hizi za kazi zifutwe. Haiwezekani tuwe na mlinzi wa bunduki anatoka Nepal, anakuja kulinda hapa Tanzania. Tuna askari ambao wanastaafu hawana kazi ukiwakuta kule nyumbani hali zao mbaya. Tutachukuaje Kanali wa Jeshi wa Nepal aje hapa kulinda, anafuata nini Kanali wa Jeshi la Nepal, ana maslahi gani Tanzania. Kwa hiyo, lazima hii (c) iseme: *"tribe or place of origin in the United Republic of Tanzania."*

Mheshimiwa Spika, katika sehemu hii pia namba (e) kuna kitu kinaitwa *National Extraction.* Sasa kina maana gani kama mtu tunayemtaja ni Mtanzania na tumesema hatubagui rangi, kabila na *race;* sasa hii *national extraction* inatoka wapi na mtu huyu ni Mtanzania? Kwa hiyo, hili lazima tufute maana hili ni *loop holes* ambayo inafanya *messengers* kutoka *South Africa* waletwe kufanya kazi ya u-*messenger* kwenye Mabenki hapa Tanzania. Hili la kwanza.

Mheshimiwa Spika, lakini katika suala la wageni kuja kufanya kazi Tanzania, kwa kweli tumekuwa hatuna *safeguards*, hatuna sifa zinazofanya watu huko nje wasije kufanya kazi hapa. Mimi nimefanya kazi nchini Kenya, Malawi na Zambia. Nimekuwa nasimamia wafanyakazi wa Shirika la *ICRAF* katika nchi 21 na kwa wale watu ambao nimewasimamia mimi hakukuwa na urahisi wa kupata kazi kama inavyokuwa hapa. Lazima uombe na kuna utaratibu uliowekwa ambao ni wazi kabisa wa kuajiri *experts* kutoka nje. Sasa hapa inakuwaje mlinzi au korokoroni anawezaje kupata *work permit* Tanzania. Apewe nafasi awe anafanya kazi Tanzania!

Huko nje zamani tulikuwa tunaheshimiwa sana. Tanzania kwa sababu nchi yetu ni nchi ambayo ina utaratibu, ni nchi mahiri na nchi ambayo ina heshima zake. Siku hizi wanasema Tanzania haina mwenyewe, kwani tumekwenda wapi. Mtu yeyote anaweza kutoka huko ugenini akaja akapewa kazi.

Kuna visingizio vidogo vidogo, kwanza wanasema watu wetu hawajui Kiingereza. Cha pili, wanasema wahitimu wetu katika vyuo vyetu ambavyo vinatoa wataalamu au *professionals,* hawajui kutumia kompyuta. La tatu, wanasema elimu yetu ya ufundi ni dhaifu hata Masekretari wetu wanasema hawafaulu Mtihani wa *Pitman.* Hivi kweli tutakaa tu tunaajiri Kaburu kutoka *South Africa* awe Sekretari, tunaajiri Mwalimu wa Kihindi kutoka Pakistan kuja kufundisha uraia au *Civics* hapa Tanzania,

tunaajiri *fitter and tunner* wa Australia kuja kufanya kazi ya ufundi kwenye madini yetu, tunaajiri wa *FTC* kutoka Australia kuja kufanya kazi Tanzania, watoto wetu watafanya kazi wapi?

Kwa hiyo, pamoja na kusisitiza katika mabadiliko haya ambayo nimeyasema, kwanza, Serikali lazima ihakikishe kazi zote ambazo zinatokea nchini Tanzania zinatangazwa katika magazeti ya Tanzania. Maana ilivyo sasa kuna *technicians* wameajiriwa hivi karibuni kwa mfano, *Kahama Gold Mines* ajira hizo hazikutangazwa hapa Tanzania. Sasa kama haikutangazwa wanapewaje *work permit. How did they get a visa. How do we bring Tunner and Fitters from Australia and give them jobs in Tanzania.* Hivi hakuna *Fitter and Tunners* wa *Dar es Salaam Institute of Technology?* Mimi naamini kabisa wapo. Kwa hiyo, Serikali lazima ihakikishe, kazi zote zinazotokea Tanzania zinatangazwa kwenye magazeti yetu. Mtu yeyote asipewe kazi kutoka nje kama kazi hiyo haikutangazwa kwenye magazeti ya Tanzania.

Pili, ni vizuri Serikali ikajua watu hawa wanaotoka nje na *qualifications* hizo wanapewa mshahara shilingi ngapi. Lazima Serikali ijue kwamba ni thamani gani ya mshahara huo inatumika Tanzania. Mimi nitoe mfano nchini Kenya wanatafuta *data* mpaka wanajua kwamba wewe unakodisha nyumba ya nani na unalipa kodi shilingi ngapi. Kwa hiyo, wanajua kabisa kwamba, *at least one thousand dollars* ya mshahara wako inakwenda kwenye nyumba ya Mkenya. Sasa na kwetu tunazidhibiti namna gani.

Hawa wawekezaji wakija wanapewa kiwanja cha kujenga kiwanda lakini wasipewe kiwanja cha kujenga nyumba kwa sababu Watanzania nyumba zao nani atakaa? Lazima nyumba za Watanzania zipate watu wa kukaa na watu wa kukaa ni hawa wawekezaji au wafanyakazi wao. Ni vizuri na sisi tukaamka, lazima tufundishe watoto wetu Kiingereza hicho wanachosema hatujui. Tufundishe kwa nguvu kabisa ili watoto wetu wajue Kiingereza hicho wanachosema hatujui.

Vile vile nchi yetu imekuwa na vishule shule huku mjini vinafundisha kompyuta. Kila mtoto anayemaliza *form four* anasema nakwenda kujifunza kompyuta na vishule hivi havikusajiliwa au havitoi elimu yenye ubora tunaohitaji. Ni lazima tuhakikishe kwamba, shule zetu zinafundisha kompyuta kule shuleni na tuwe na mtaala ambao utawafanya wawe *competitive* kwenye soko la ajira.

Tatu, katika *professional training* ni lazima tuhakikishe kwamba, tunafikia viwango vya taaluma wanazotaka waajiri. Kwa mfano, katika *technician training* basi tu-*match* hizo *Standards* zetu na *City and Guilts of London.* Tuhakikishe kwamba, kila digrii na *profession training programme* inakuwa na *professional training* katika *computing* na *information technology* ili vijana wetu waweze kuwa *competitive.*

Ninachotaka kusema hapa na kumalizia ni kwamba, katika Wizara hii na Wizara zingine tutakapokuja hapa wakati wa Bajeti, tuone ni hatua gani ambazo zimechukuliwa katika kutekeleza hili ili sisi tusiwe tu eti nchi yetu ni nchi nzuri sana ya uwekezaji, lakini sio nchi nzuri ambayo inaweza kutoa ajira kwa watu wake. Nchi gani ina wawekezaji wengi na watoto wake wako barabarani hawana kazi? *This is a contradiction* ambayo

haiwezi kuwa *acceptable.* Pia nilikuwa nataka nishauri kwamba, wakati umefika kwa Watanzania kwenda nje sasa kwa wingi na Serikali isaidie kufanya hili kwenda kuleta teknolojia mpya. Kusoma katika Vyuo Vikuu vingi vya nje ambavyo vinajulikana wazi vina teknolojia nzuri ili waweze kuleta teknolojia mpya na katika ajira waweze kuwa *competitive.*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, ninapenda niseme kwamba, sina tatizo jingine na Muswada huu na naunga mkono hoja hii. Lakini katika maeneo haya ambayo nimesisitiza, tuchukue hatua thabiti kabisa za kurekebisha mapungufu. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia.

Mheshimiwa Spika, nadhani ninawashukuru Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo na wenzake kwa kuleta Muswada huu. Ni jana tu nilipobadilisha mawazo kwa sababu ule wa kwanza ambao nilikuwa nao kwa kweli ulikuwa na mapungufu mengi. Lakini nadhani kama alivyoeleza jana Mheshimiwa Waziri, baada ya kukutana na wadau mbalimbali, kuna mambo ambayo wameyarekebisha. Kimsingi hii ilitokana kwamba, suala la mwajiri na mwajiriwa na hasa katika mazingira ya nchi maskini kama Tanzania na kwa kuzingatia historia ya mapambano ya wafanyakazi ya kudai haki zao, basi Muswada huu kwa marekebisho ambayo yamefanyika, ndiyo maana nasema ninawashukuruni sana waandaji kwa sababu umetoa nafasi kwa wafanyakazi pengine kuweza kushinikiza ili haki zao ziweze kutolewa.

Kwa sababu tunaelewa kama si vuguvugu la nadharia ya Marx na Engeles na tishio la wafanyakazi kujitwalia madaraka katika nchi za Kibepari, basi nina uhakika Marekani na kwingineko katika nchi za Kibepari, wasingeweza kurekebisha angalau kuweka *incentives* na posho na vitu vingine ili kujenga sasa mazingira mazuri ambayo ilikuwa inaondoa ile vuguvugu na hamasa ya watu kujichukulia madaraka ya kiutawala katika nchi hizo.

Mheshimiwa Spika, lakini nikirudi katika Muswada wenyewe ukurasa wa 58, alipokuwa anazungumza *basic wages,* anafanya *definition* pale, sikuona *basic salary* ame-*define* lakini sikuangalia hiyo. Lakini pale chini ni *section 4* halafu anaendelea pale anazungumza *basic salary* halafu anaenda *does not include allowances whether or not based on the employee's basic wages, pay for overtime worked in terms of section 19(5)* na yale mengine yanayofuata. Uzoefu unaonyesha kwamba, tulipokuwa wakati mwingine tunazunguka huko, yanapoulizwa maswali kuhusu posho mbalimbali ama za *over time* au za mazingira magumu, kuna majibu ya Serikali kwamba, aah posho zile zilijumuishwa katika mshahara kwa lengo la kufanya uwe mkubwa na ili ku-*calculate* yale malipo yako na marupurupu yako unapostaafu. Lakini kwa mujibu wa hii ilivyowekwa, nadhani sasa wakati umefika kwamba watu watakuwa na haki sasa ya kudai hivyo vitu viwe vimetenganishwa. Kwa hiyo, unaliona hili kwamba wanapoliweka sasa wakumbuke kwamba kuna watu wataweza kudai hizo haki zao.

Mheshimiwa Spika, katika *sub-part (c)* anazungumzia *discrimination, section 5 sub-section 6(b)* anasema: *"it is not discrimination",* halafu anaeleza pale kwamba, mtu kumwajiri kwa kuzingatia *inherent characteristic* sasa *inherent* ni kwa mujibu wa nani? Maana tunavyoelewa inaweza kuwa *inherent because of the attitude we have according to the culture we had.* Sasa kama una utamaduni fulani wa kujua kwamba utamaduni fulani inaweza kusomewa na watu fulani na kazi fulani inaweza kufanywa na watu fulani labda ni ya u-*engineer* na kazi nyingine.

Sasa ukishaiweka hapa kwenye sheria na unasema sio *discrimination,* bado inaturudisha kule kule kwa sababu itakuwa ina-*contradict* ile nyingine. Kwa hiyo, sikuweza kujua ni *criteria* zipi zinatumika kuonyesha kwamba nadhani *to be more specific* ni *sub-part (c)* kama nilivyosema *section 7 sub-section 6(b).* Anasema: *"to distinguish, exclude or prefer any person on the basis of an inherent requirement of a job".*

Sasa hiyo ndiyo ipi? Maana yake tuna mazoea yetu ya kifikra sasa kwa sababu haiwezi kueleweka mtu utakwenda kumwuliza kwamba, wewe mbona ulifanya hivi atakuambia mimi nadhani kama hii anayefaa huyu. Pengine katika Muswada huu ameonyesha mtu aweze kutoa *policy* yake na utaratibu mzima wa kuweza kuhakikisha kwamba, anaajiri kufuatana na *reasons za gender.* Sasa hii nadhani wangeanzia kule vyuoni. Maana kuna vyuo vingine unakwenda chuo cha ufundi unakuta kuna wanafunzi kama 300 hivi halafu wasichana ni 30. Sasa huyu naye anaambiwa alete *policy,* sasa sijui *policy* anai-*cover* vipi?

Mheshimiwa Spika, tulitaka katika sheria hii pengine wangeangalia mahitaji ambayo mwajiri anapaswa kufanya akishirikiana na watu wa Mashirika ya *NSSF, PPF* na wengine. Maana imekuwa sasa ni tatizo mtu ameajiriwa na hasa Serikali kwa sababu na yenyewe imetajwa kwenye sheria kama ni mwajiri. Mwalimu ameajiriwa mwaka 1969 au 1970 akapewa nyaraka akahamishiwa Rukwa, akapelekwa Morogoro, Dar es Salaam, Kagera na kuzungushwa huku na nyumba alizokuwa anaishi vyeti vyake vinapotea. Sasa Serikali ambayo ilimwajiri imekaa pale haina hata nyaraka moja, akikaribia wakati wa kustaafu wanaanza kumsumbua kwamba wewe lete barua hii, wewe lete barua hii, wakati katika zama kama hizi, Serikali inapaswa kuwa na *database* ya kwamba mwajiriwa huyu aliajiriwa hapa na kwa kweli kama anakaribia kustaafu miaka miwili iliyobaki unampa taarifa na vitu vyake vyote vinakuwa pale kuliko huu usumbufu ambao tunaupata. Sasa hii haiko *clear* katika sheria hii.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa naangalia *section 5, sub-section 4(b),* inayohusu ajira kwa watoto. Yeye ameweka kana kwamba si vibaya anasema: *"that places at risk the child's well-being, education, physical or mental health or spiritual, moral or social development."* Sasa ninavyoelewa silisemi hili kisiasa na sitegemei nitajibiwa kisiasa, maana kuajiri kuna maana nyingi.

Kuna kuajiri kwa kulipa ujira kidogo na kuajiri kwa kumpa mtu ahadi. Sasa tunaweza kufika mahali kwa sheria hii ukiacha yale mambo ya dini ambapo sasa akizaliwa pale atakwenda pale. Lakini katika vyama vya siasa kama *CUF, TLP, UDP*

ama CCM, watawachukua vijana wanawaita chipukizi halafu wanawapa mafunzo ya Kijeshi na kuwafanya wawe watiifu kwa chama chao.

Mimi nadhani *in one sense or another, this is to corrupt their mental and social development.* Kwa sababu hawana *choice* sasa wewe unapowaita pale unawaambia hivi unawafananisha na nguo zile unakuwa umewanyima haki yao kwa kweli kwa sababu unawapa matumaini kwamba, ukimaliza utakuwa wewe kijana wetu na nini. Kwa hiyo, malipo yale ambayo ni *indirect* ni ile ahadi uliyompa sasa kwa sheria hii ikibaki hapa tutakuja kujikuta watu kwa kweli wanawachukua vijana halafu wanawaharibu ile akili yao katika masuala ya itikadi na masuala mengine ya nchi. Kwa hiyo, mtaniwia radhi kwa sababu sitaji chama chochote, najua kila chama kitakuwa na chipukizi, lakini nadhani tungewawekea masharti.

Mheshimiwa Spika, katika sheria hii inaonyesha kwamba, waajiriwa au chama chao kikikutana ili kupitisha maazimio pengine ya kufanya mgomo ili kumshinikiza mwajiri aweze kuwapa maslahi yaliyo bora, katika mkutano wao ili uweze kuwa halali na maamuzi yale lazima kuwe na *Labour Officer* kama *internal organization.* Sasa *Labour Officer* watu wanapanga mpango wao na *Labour Officer* ndiye aje na sehemu zingine *Labour Officers* wanakuwa ni wachache, sasa hii ni kuweka urasimu na kwa kweli ni kuweka masharti ambayo pengine yatachelewesha kile kilichokusudiwa. Tungeomba kama wanakutana wana mambo ya kusema wayaseme kwa mujibu wa sheria hii na kama wana kitu cha kushinikiza waweze kushinikiza. Kwa sababu tuna uhakika sheria inachokitaka hapa ni kwamba, unachokiomba sio lazima upewe hicho kwa sababu mwisho tunadhani mtakaa kwenye meza, mnafanya *dialogue,* halafu mwisho wake wanakubaliana.

Kwa hiyo, hii *requirement* inayotaka kuwe na *Labour Officer,* nadhani ni kitu ambacho kinachelewesha utaratibu huo.

Mheshimiwa Spika, utaniwia radhi kama nitavunja kanuni lakini nitakuwa sijaivunja kwa sababu katika *briefing* na shughuli zitakazokuwepo kwa Bunge hili, kutakuwepo vile vile na Muswada unaohusu *The Government Student's Loans Board.* Sasa kwa sababu vitu vyote hivi vinatoka Serikalini, ni vyema kungelikuwepo na uoanishaji wa baadhi ya mambo. Kwa sababu ile ipo na tulishagawiwa sisi Waheshimiwa Wabunge, kuna mahali itafika kwamba kwenye sheria za kazi wewe mwajiri utakuwa *responsible* kwa haya.

Sasa kama ingelikuwa vizuri wakawa wamezisoma kwa pamoja angalau wakaweka ili kurekebisha na kuoanisha hiyo hali kwamba wewe utakapomwajiri mtu ambaye amemaliza au amemaliza kama mimi nilivyomaliza, nikichukua mkopo wa Serikali na mwajiri atatakiwa kulipa kama ofisi yako itakavyotakiwa kulipa mkopo wangu niliochukua lakini kwa utaratibu ambao tutakubaliana, nitalipa. Kwa hiyo, nadhani na yenyewe wangeweka wakaona utaratibu huo unakwendaje ili kuweza kurahisisha shughuli hizo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuyasema hayo, nadhani watafanya marekebisho kidogo, napenda kusema kwamba, ninaunga mkono hoja na kwamba natumaini watafanya marekebisho kwa kadri mjadala unavyokwenda. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. LEONARD N. DEREFA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi nichangie kwenye hoja iliyo mbele yetu. Kwanza, napenda nitumie nafasi hii kuwapa pole Watanzania na Mheshimiwa Rais wetu, kwa kuunguliwa na Ikulu. Poleni sana na ninaamini kabisa kwamba, Mwenyezi Mungu, atatuwezesha kujua chanzo hasa cha ajali hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwanza napenda niseme kwamba, naunga mkono hoja hii na sheria hii imeletwa kweli kwa wakati wake na ninaamini kabisa kwamba, itatatua migogoro mbalimbali ambayo imekuwepo hasa katika sekta mbalimbali.

Hapa ningependa nisemee masuala ya watumishi wa hospitali. Hapo nyuma utakuta kwamba, watumishi wa hospitali walikuwa hawana chombo ambacho kinaweza kuwasaidia kama vile walimu wakiwa na ile CWT.

Utaona kabisa kwamba, mishahara ya watumishi wa hospitali imekuwa duni kwa muda mrefu sana. Mara nyingi tunapowatembelea wanalalamika na kwa bahati mbaya utakuta kwamba, hawana chombo ambacho kinawasaidia. Pamoja na kwamba kuna *TUGHE*, lakini utakuta kwamba, baadhi ya watendaji hao walikuwa hawaruhusiwi kutokana na sheria zetu hasa zinazohusu migomo.

Lakini ninaamini kabisa kwamba, watumishi hawa wa sekta ya afya na wenyewe sasa hivi watajiweka sawa ili wawe na chombo kitakachosaidia katika kuboresha maslahi yao. Napenda niipongeze sana Wizara kwa kazi hii nzuri na ninaamini kabisa kwamba, mara watakapopewa hii nafasi hawawezi kuwa na matatizo kama ilivyokuwa nyuma.

Maana yake zamani walikuwa madaktari wanapokuwa wanataka kuona kwamba matatizo yao ya mapato yanakuwa mabovu ili wayaboreshe, wengi walikuwa wanachukuliwa hatua. Wapo madaktari waliowahi kuchukuliwa hatua kwamba wakaagizwa wasiajiriwe mahali popote. Ninaamini kabisa kwamba, sheria hii itawasaidia katika kuboresha maslahi yao.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa naomba vile vile niongelee suala la huduma mbalimbali kwa watumishi wa Serikali hasa walimu. Katika Jimbo langu la Shinyanga Mjini, walimu kwa kawaida tumekuwa na matatizo makubwa sana hasa wanapopata maafa, wanapofiwa ama wanapokufa wenyewe.

Kuna wakati mwingine unakuta kwamba, Halmashauri inakuwa haina fedha zile za kutosha katika kuwahudumia.

Sasa, mara nyingine katika ajira zao walikuwa wanatakiwa kwamba mtu akifa lazima arudishwe kwao, lakini wakati mwingine ilikuwa inakuwa kazi ngumu sana na ndiyo maana katika Halmashauri utakuta wametumia fedha za mifuko mbalimbali

ambazo hazikutarajiwa kutumika katika suala la kuwahudumia walimu. Naomba Wizara mbalimbali zinazohusika kama inawezekana waweze kuwa wanaweka *deposit* ambayo inasaidia katika kuwahudumia walimu hasa wanapopata matatizo mbalimbali kutokana na mapato ya *council* zetu sasa hivi kutokuwa mazuri

Mheshimiwa Spika, vile vile napenda nitumie nafasi hii kuiuliza Wizara hii ingawaje suala hili halihusu hapa, lakini napenda nijue kuhusu suala la kiwanja chetu cha michezo. Kwa bahati nzuri mwaka jana tuliambiwa kwamba Serikali imetenga shilingi bilioni 60 na leo tuko katika mwezi wa nne, ni karibu miezi 10 imepita na kazi hii bado haijaanza. Ningependa wakati Waziri anajumuisha tupate majibu sahihi ni kitu gani kimekwamisha kazi hii yeye kama Askari wa Mwamvuli kuna tatizo gani katika hili kwa sababu fedha zipo halafu na kazi haifanyiki. Tungependa tutumie nafasi hii katika kuuliza hili tatizo ili tuelezwe vizuri.

Mheshimiwa Spika, pia, ningependa kueleza kwamba sheria hii ni nzuri sana itatusaidia katika kupunguza mapungufu mbalimbali. Vile vile, ningependa kueleza kwamba kuna matatizo ambayo yamekuwepo, mishahara ambayo hailingani *(discriminatory salaries)* kati ya baadhi ya idara mbalimbali za Serikali. Kwa mfano, siku moja nilikuwa kwenye mkutano, daktari kwa mfano aliniambia kwamba mshahara wake ni mdogo zaidi kuliko *watchman* wa *TRA.*

Mheshimiwa Spika, masuala ya namna hii, *discrimination* za namna hii katika kupunguza matatizo ni vyema zikatolewa. Kutokana na kwamba sasa hivi Serikali inaboresha mapato yake ni vema kukawepo na utaratibu mzuri wa kuhakikisha kabisa kwamba mishahara inaoanishwa na inalingana.

Ukitazama taaluma ya udaktari, mtu amesoma labda miaka 10 ana *degree* mbili, halafu *watchman* wa *TRA* labda aliishia darasa la saba, lakini kwa ile tofauti ya mishahara kwa kweli hatuwatendei haki watendaji wetu wa Serikali hii na watendaji wetu wa idara mbalimbali kwa sababu kwa kazi hii inatakiwa mishahara lazima ifanane. Ninaamini kabisa kwamba huwezi ukasema mkono ni afadhali zaidi labda kuliko mguu, ukiumwa mkono unaweza ukaathirika vile vile.

Mheshimiwa Spika, nafikiri kwamba katika kuboresha sheria hii ni vyema sasa hivi tukaona kwamba *segregative salaries* lazima ziwekewe utaratibu wa kuboreshwa zaidi ili kusudi Watanzania kutokana na fani mbalimbali na kutokana na kazi zao lazima walipwe mishahara ambayo inalingana. Mfano mimi wakati nilipokuwa nasoma shule, nilikuwa nasoma na baadhi ya watu ambao sasa hivi wengine ni madaktari, hata kiakili nafikiri wale ambao ni madaktari walikuwa kwa kweli wananizidi hata kwa *marks.* Naomba tuzidi kuboresha hali hii na tuweke hali nzuri ili kusudi watu waweze kuridhika.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni kuhusu *discrimination* katika ajira za migodi. Jambo hili mwenzangu Mheshimiwa Msindai ameliongelea. Ukitazama malalamiko ambayo wanayo watumishi wetu wa Tanzania kuhusiana na wawekezaji hasa kwenye migodi na wawekezaji mbalimbali, utakuta kwamba kwa kweli hatuwatendei

haki na ni vema Wizara hii isimamie vizuri sheria zetu ambazo tunazitunga ili kila Mtanzania apate huduma nzuri anazostahili kama mtumishi na hatimaye aweze kuboresha huduma mbalimbali katika nchi yetu.

Baada ya kusema hayo ningependa kuongelea kuhusu madaktari. Katika upande wa madaktari kumekuwepo na malalamiko kwa mfano utakuta sehemu nyingine hawalipwi stahili zao kama *on call allowance.* Mfano katika jimbo langu la Shinyanga madaktari wanalalamika kwamba hawajalipwa *on call allowances* kwa muda mrefu na wanapoomba walipwe fedha hizo, fedha hazipatikani kama Serikali ilivyoahidi.

Mheshimiwa Spika, katika jimbo langu kuna wafanyakazi hapo nyuma walifanya kazi za kupambana na kipindupindu na bado hawajalipwa stahili zao. Mimi kama Mbunge nimejaribu kuiandikia Wizara inayohusika, lakini kwa bahati mbaya sipati majibu na mpaka sasa hivi watumishi hao bado wanadai fedha hizo. Kwa hiyo, napenda nitumie nafasi hii kusema kwamba Wizara zinazohusika hasa Wizara ya Afya, wahakikishe pamoja na kuboresha stahili mbalimbali kama *on call allowance* pamoja na *allowances* zinazotakiwa walipwe hasa kwenye zile *special duties* kama vile kipindipindu, stahili hizi vile vile zinatakiwa zilipwe.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, napenda kusema tena kwamba naunga mkono hoja na ninapenda niipongeze Wizara kwa kuleta sheria hii na ambayo ninaamini kabisa itaboresha utumishi wa Watanzania. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. AGGREY D. J. MWANRI:** Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii kukushukuru sana kwa kunipa fursa ya kutoa mchango wangu katika Muswada huu ambao umeletwa na Mheshimiwa Kapuya.

Mheshimiwa Spika, kwanza ninachopongeza hapa ni namna ambavyo wadau mbalimbali wamehusishwa katika jambo hili. Hotuba ya Mheshimiwa Kapuya nimeitafuta mpaka nikaipata pamoja na kwamba ilikuwa haijaingia kwenye *Hansard,* nikaiangalia na ametuelekeza vizuri kwa kweli kuonyesha, pia kwenye redio na kwenye *TV* nilimfuatilia.

Mheshimiwa Spika, mimi nikiri kwamba hotuba hiyo haikuja kwenye Kamati yangu, niko kwenye *PAC* kwa hiyo sikuiona, lakini nilimfuatilia kwa karibu kwa sababu jambo linalozungumzwa hapa ni *central* kwa nchi yetu na kwa mimi mwanachama wa Chama cha Mapinduzi ni muhimu sana. Chama chetu kinasema ni cha wakulima na wafanyakazi na leo tunazungumza habari ya maslahi ya wafanyakazi. Kwa hiyo, kunyamaza kimya siwezi kunyamaza kwa sababu najua hapa ndipo mahali pake, ndicho kinachotupa sisi hadhi na nafasi ya kuendesha nchi na kuongoza.

Mheshimiwa Spika, kinachozungumzwa hapa kwa kifupi ni *relation of production,* inazungumzwa *the political economy of capitalism and the political economy of socialism*. Hii maana yake siyo *politics* na *economics to put together,* aah, unazungumzia mahusiano ya uzalishaji mali katika maeneo yanayohusika*.* *(Makofi)*

Nchi hii katika katiba inatamka wazi wazi kwamba ni nchi ya kijamaa, lakini katika *policies* zake na mambo yake imeainisha, imefika mahali tukasema kwamba tunafuata pia mwelekeo wa kibepari. Hakuna nchi ya kibepari hapa, hakuna! Ubepari haujengwi hivi, kama unafikiri hapa tunajenga ubepari, hapa haujengwi hivi, wala ujamaa haujengwi hivi, sisi tuna mwelekeo tu unaokwenda hivi. Lakini ni vizuri tukaelewana humu ndani kwamba kama unazo sheria, kama unazo kanuni, kama unazo taratibu unasema sasa mimi naondoka kutoka kwenye mfumo wenye mwelekeo wa kijamaa ninakwenda kwenye mfumo wenye mwelekeo wa kibepari, huwezi ukabakia na taratibu zile zile itakuwa ni *contradiction.* Utasema hivi: "Mimi niko kwenye mwendo wa kujenga nchi ya kijamaa nikiweka mwelekeo wa kibepari, lakini ndani yake ni lazima niweke taratibu ambazo zitawafanya wawekezaji waje wawekeze katika nchi yangu." Ndicho kinachozungumzwa hapa.

Ni vizuri tukaiona *contradiction* iliyopo katika mfumo wa kibepari. *Basic contradiction* iliyoko katika mfumo wa kibepari ni kati ya *labour* na *capital.* Katika *capitalism* kazi ni kujenga kitu kinachoitwa faida kibao wala siyo faida, kwa kiingereza wanaitwa *super profit.* Kwa hiyo, ukiisha-*accommodate* umeukubali huu mfumo umesema unauchukua unakwenda nao.

Ukisema unaleta sasa mwelekeo, unaleta taratibu, ni lazima ujue kwamba mtu huyu anakuja kuwekeza hapa, kazi yake *paramount* ni kujenga kitu kinachoitwa faida kibao. Kwa hiyo, akiwapunja wafanyakazi ndiyo anatengeneza faida kibao. Asipowalipa *night allowances* zao ndiyo atatengeneza faida, kinacholetwa hapa ni kitu kinachoitwa *constant capital* anaileta *variable capital.*

*Constant capital* ndiyo ile inayobaki, ndiyo wakoloni walipotutawala, sitaki kwenda kwenye historia yake. Kinacholetwa hapa ni *variable capital. Variable capital* ndiyo inayolipa *wages,* ndiyo inayolipa mishahara, kwa hiyo ukiibana hivi kama unalipa kidogo maana yake utajenga kitu kinachoitwa faida kibao.

Mheshimiwa Spika na Mheshimiwa Waziri, mimi sina tatizo kabisa na Muswada huu, lakini kuna haja ya kutahadharisha. Kule nyuma kama kukiwa na kesi imetokea katika eneo la kazi mlikuwa mnakutana pale katika eneo la kazi na kuna Chama cha Wafanyakazi pale kitasimamia, mkishindwana pale mtakwenda kwenye *Labour Office* au Baraza la Usuluhishi na hivi vyombo sasa hivi vyote vimeondoka. Tutakuwa tunakwenda sasa mwisho mpaka kwenye mahakama na Waziri anaondoka, atatengeneza kanuni tu.

Sasa, tunawaambia nini Wafanyakazi wa Tanzania? Wenzetu wanakuja hapa wanakuja na *experts* wao, anakuja na l*awyer,* anakuja na watu watakaozungumza kwa niaba ya kampuni, wafanyakazi wetu ni hawa wanaolima mihogo, wanaolima maharage. Wafanyakazi wa kwetu hapa katika mazingira ya kwetu hatuwezi kuwaita wafanyakazi wanaitwa *semi-pro-talent.* Wala matajiri wa hapa kwetu hatuwezi kuwaita matajiri, wanaitwa matajiri uchwara, kule wanaitwa *bourgeoisie,* hapa kwetu tunaitwa *the pet bourgeoisie. (Makofi/Kicheko)*

Kwa hiyo, unapata mazingira hapa na ile *militancy* unayoiona ya *industrial society,* ile ya akina *Tepter String* kule hapa hakuna. Kuna mtu hapa ambaye analima mchicha, analima maharage anaondoka anakwenda nyumbani kwake. Ukimwambia leta maandamano anaweza akakwambia mimi sili kwako, wewe kama unataka kuandamana, kwa sababu ana kitu cha ku-*loose* huko, analima maharage, analima mahindi. Kwa hiyo, hata ile *militancy* inayozungumzwa hapa ni lazima uangalie.

Mheshimiwa Spika, mimi sina ugomvi, Mheshimiwa Kapuya mimi sina ugomvi kabisa na Muswada huu kwa sababu huu ni *contemporary* unakwenda na hali halisi, lakini wakati huo huo tukijua unafanya nini katika mazingira haya yaani wafanyakazi wetu, vyama vyetu vya wafanyakazi vimejiungaungaje pale? Mfumo wa kibepari ulichofanya cha kwanza ni kuzalisha kundi kubwa la watu wasiokuwa na kazi. Cha pili, bidhaa nyingi ambazo hazina soko na tatu kukosekana kwa kitu kinachoitwa malighafi. *The swimming pool of the unemployed,* unasema hawa wataandamana, watafanya vurugu.

Mheshimiwa Spika, *discipline* katika mfumo wa kibepari inatokana na mfumo wenyewe, wako watu mia mbili wamekaa nje, sisi tuko humu ndani tutafanya kazi kwa nidhamu kufuatana na tajiri anavyosema, siyo kama tunavyotaka, kwa sababu ukileta maneno maneno atachukuliwa mwingine ataletwa hapa halafu unaambiwa *out,* unakwenda. Katika mazingira ya namna hiyo kuna kitu kinachoitwa *the cut throat competition,* ni lazima tutahadharishe.

Ndiyo tumeukubali, mimi nasema kwamba Chama changu Chama cha Mapinduzi kinatamka kwamba kutakuwa na mfumo huu wenye mwelekeo wa soko huria na mambo haya. Lakini wakati huo huo hata wanaotusikiliza kule nje kwa juu wale wajamaa wamekaa mle ndani lakini wanajua *the basic contradiction* ambayo ina-*image* katika mazingira. Hilo moja.

La pili, ambalo linakuwa *addressed* hapa ni tabia ya ubaguzi. Ninampongeza sana Mheshimiwa Waziri. Hapa kinachozungumzwa ni kwamba yapo makampuni yatakuja katika Tanzania yana *payroll* mbili, tatu. Hawa wenye akili hii watalipwa kwa *payroll* hii na hawa wenye akili hii watalipwa kwa *payroll* hii. Wakija watu wa *labour* wanataka kuchunguza tutawaonyesha hii *payroll,* ndicho kinachozungumzwa hapa. Kwa maana ya Muswada huu wa leo tunaoupitisha hapa huo mwanya hautakuwepo.

Jambo hili nalizungumza si kwamba silifahamu, nimefanya *comparative analysis* ku-*compare performance* katika *Public Enterprise* na *Private Enterprise* (Mashirika ya Umma na Mashirika yale ya Watu Binafsi). Unamwuliza *payrol*l hivi anakuonyesha hivi, unakwenda kuwauliza wale eti nyie mnalipwa hivi anakwambia sisi hatulipwi hivyo. Wenye asili fulani, sitaki kutaja hapa kwa maana sisi tunajenga umoja, muafaka na nini, sitaki kutaja hapa wenye asili gani, lakini lipo linafanyika katika nchi yetu, wanakaa wanakuangalia namna hii, amekuja huyu Mswahili basi huyu tutamweka kwenye *payroll* hii, leo linazungumzwa hili kwamba hatutakuwa tunaendelea.

Mheshimiwa Spika, suala la tatu ni la Dr. Asha-Rose Migiro. Nimekaa pale Arusha watoto wanaajiriwa kule Mererani wanaitwa chokoraa, wako kibao. Wamejaa

mitaani kule wanachukuliwa wanapelekwa Mererani, wanapelekwa wapi, nisitaje migodi ya watu nisije nikaonekana kama napiga watu vita, lakini tunajua kwamba yanafanyika katika madini, katika mashamba ya miwa, katika mashamba ya mihogo, katika mashamba ya pamba na katika mashamba ya kahawa wanafanya. Wanaajiriwa watoto wadogo wenye umri mdogo miaka 14 kwenda chini, ndiyo inayotamkwa hapa. Muswada huu unaweka mazingira yatakayozuia watoto hawa wasiajiriwe.

Mheshimiwa Spika, leo nimekuja na miwani kabisa, pale katika ukurasa wa 57 *subsection 2* unasema hivi: *"This Act shall apply to all employees including those in the public services of the Government of Tanzania Mainland , but shall not apply to members, whether temporally or permanent in services of :-*

(i) *The Tanzania Peoples Defence Force;*
(ii) *The Police Force;*
(iii) *The Prisons Service or*
(iv) *The National Service."*

Sasa nenda ukurasa wa 58 ile *subsection 3* unasema: *"The provisions of section 5, 6 and 7 shall apply to members of the forces and services referred to in subsection (1),* hii niliyoisoma hapa. Mimi sijakuelewa kwa sababu umesema hii haita-*apply* halafu sasa una-apply.

Mheshimiwa Waziri, ningependa wakati utakapokuwa unajibu ukatuambia kwamba unasema nini, kwa sababu hii umei-*rule out* hapa, umesema kwamba haita-*apply,* sasa umerudi huku mbele unasema kwamba ita-*apply* tena. Kwa hiyo, nina tatizo moja hapa nalipata.

La pili, ukurasa huo huo wa 58 unasema: *"In this act unless the context requires otherwise..."* unazungumzia *arbitrator,* unasema: *" Arbitrator appointed under section 19 of the labour Institutions Act, 2004"* ipi? Haipo. *I know* inakuja, lakini hapa unai-*sight* na hapa tunapitisha jambo la kisheria.

Labda maoni yangu ni kwamba, ungezungumzia *Arbitration Ordinance* ambayo ina-e*xist,* lakini hiyo ukii-*quote* hapa haipo, hatujai-*enforce,* haijapita hiyo, hatujaipitisha hapa. Kwa hiyo, napenda kuuliza kwamba wakati unapozungumzia hii *Labour Institutions Act, 2004* Mheshimiwa Waziri ana-*refer to what?*

Mheshimiwa Spika, mwisho, wakati atakapokuwa anajibu nafikiri atatujibu, napenda nirudie tena kusema kwamba sina tatizo na Muswada huu, lakini nina tahadhari hizo ambazo nimeziweka mbele ya hili Baraza.

Iko haja ya kuangalia vizuri na kujua kwamba wenzetu kama wanakuja kule walikuwa wanasema kwamba *okay* hatuwezi kuwekeza mpaka uondoe sheria hii, mpaka uondoe mfumo huu, ni nini kinachomtisha? Anajua kwamba sitaweza kutengeneza kitu kinachoitwa faida kibao kwa maana ya sheria zilivyo sasa hivi. Leo tunapitisha hivi,

tunataka tuone pia kanuni zinatengenezwa ambazo zitasimamia maslahi ya wananchi wa Tanzania ambao ni wafanyakazi na wakulima wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema maneno hayo, kwa niaba ya wananchi wa Siha naomba kuunga mkono Muswada huu. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. ROSEMARY H. K. NYERERE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja hii. Kwanza kabisa ningependa kutoa pongezi zangu kwa Mheshimiwa Getrude Mongella, kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Bunge la Afrika na pia ningependa kutoa pongezi zangu kwa Mheshimiwa Arcado Ntagazwa, kwa kuwa Rais sasa sijui kama nitakosea sana, lakini Rais wa Baraza la *UNEP*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi hizo, ningependa kutoa pongezi kwa Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo kwa kutuletea Muswada huu ambao umekuja katika wakati muafaka na kuwapongeza Mwenyekiti wa Kamati husika, Mheshimiwa Sophia Simba kwa mchango wake na pia kwa upande wa Upinzani ambao wametoa mchango mzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kabla sijasahau ningependa kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja, ila ningependa tuangalie maeneo machache madogo madogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa ningependa tuangalie sehemu ambayo ameitaja pia msemaji aliyepita, nayo ni sehemu ya kwanza. Utakuta kwenye Muswada huu sehemu ya kwanza *section* ya nne inataja mara nyingi *Labour Institutions Act, 2004.*

Imetajwa katika maelezo ya neno *arbitrator,* katika maelezo ya neno *Commission, Council, Essential Services Committee, Labour Commissioner, Labour Court, Mediator, Registrar.* Kila mara inarudia *Labour Institutions Act* ya mwaka 2004, hiyo *act* haipo, kuna *bill* inayokuja mbele yetu wala hatujaijadili, tutai-*discuss* baada ya ku- *discuss* *bill* hii.

Mheshimiwa Spika, hicho kitu kilitokea tena mwaka jana wakati tuna-*discuss* sikumbuki ilikuwa ni *bill* gani, lakini Mheshimiwa Mkono ali-*raise issue* kama hiyo, kwamba tunataja act kwa kitu ambacho hakipo. Nafikiria kwamba ingekuwa busara tujifunze kwa makosa yaliyopita siyo kila mara kusema sisi ni binadamu tumekosea, sisi ni binadamu tunakosea, basi. Nadhani ni vizuri, hasa makosa kama yametokea basi tusiyarudie hasa kama siyo ya zamani sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo ningependa kulizungumzia ambalo pia Mheshimiwa Maghembe amelitaja ni kuhusu vibali vya kazi ambavyo wanapewa watu kutoka nchi za nje.

Labda sielewi sheria vizuri, lakini ninavyoelewa kwa uelewa wangu mdogo ni kwamba *works permit* zinatolewa kwa watu ambao taaluma ile hatunayo nchini, siyo kwa

watu ambao taaluma ile tunayo nchini. Mfano tukiangalia kwenye *Mining Industry,* inaeleweka kwamba hatuna *technological capacity* ya kuchimba migodi, hatuna uwezo huo sasa hivi.

Kwa hiyo, inaeleweka tukisema kwamba tutawaomba wawekezaji kutoka nje watusaidie kuchimba migodi kwa sababu hatuna vifaa hivyo, hatuna taaluma hiyo, hiyo inaeleweka tunaweza tukaikubali.

Lakini tunaposema sasa kwamba na wale wanaokuja kuchimba migodi basi wapikiwe chakula cha kutoka kwa mtu wa nje siyo vizuri, kupika chakula tunaweza, taaluma ya kupika chakula tunayo taaluma ya kusafisha ofisi tunayo, tunaweza. Kwa hiyo, nafikiria kwamba ingekuwa ni muhimu tunapotoa *work permit* tuangalieni taaluma gani ipo na taaluma gani haipo. Binafsi naona kwamba siyo sawa sawa ku-*subcontract* kampuni kutoka nje kuja kupika chai.

Hii imetokea katika *Financial Institution* hapa Tanzania, huko Dar es Salaam kuna kampuni ya nje inayopika chai, inayotoa chai. Chai tunaweza kupika, vitafunio tunaweza kutoa, tuna uwezo huo. Tuna uwezo wa kufagia ofisi, hata mimi nina uwezo huo baada ya mkono wangu kupona, huo uwezo upo. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika *employment* ukiangalia kwamba watoto wetu wengi hawana kazi tuwafikirie kwanza raia wa nchi yetu, siyo raia wa nchi nyingine, tufikirie kwanza raia wa nchi yetu kwamba wao wapewe nafasi ya kwanza hasa ukifikiria kwamba katika nchi hii hakuna kuwalipa watu ambao wako *unemployed* kulinganisha na nchi zingine.

Mheshimiwa Spika, nchi ambazo zimeendelea watu ambao hawana kazi wanapata visenti kidogo, lakini nchi yetu hatupati visenti kidogo, kama huna kazi, huna kazi. Kwa hiyo, ni lazima tufikirie wananchi wetu kwanza kabla ya mwananchi yeyote mwingine. Wale hawana kazi wanakuja kutafuta kazi huku, basi tutawapa kazi ambazo wanaziweza na ambazo sisi hatuziwezi, siyo ambazo sisi pia tunaziweza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kuendeleza hapo hapo, mfano katika hospitali utakuta anakuja daktari ambaye ni *TX* kutoka nje na daktari ambaye yuko hapa hapa Tanzania, taaluma zao ni sawa sawa, lakini na ninaamini kwamba hata huyu aliyeletwa kutoka nje sidhani kwamba tumepungukiwa kiasi cha kumwita kutoka nje.

Sawa taaluma zao ziko sawa sawa, labda tuna upungufu wa madaktari basi, lakini tofauti ya mishahara isiwe kubwa kiasi hicho wakati mingine inafika zaidi ya mara 15.

Daktari bingwa wa Kitanzania katika taaluma fulani mshahara wa *counterpart* wake kutoka nje katika hospitali hiyo hiyo, katika fani hiyo hiyo mwenzake analipwa zaidi ya mara 15. Hizo hela, mshahara wa yule *Foreign Medical Doctor* ukilipa miezi miwili tu unaweza kumsomesha bingwa mwingine, shilingi milioni 22 kwa mwezi. Miezi miwili tu mshahara wake tunaweza tukapata bingwa mwingine, hivi ni vitu vya kuangalia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunatafuta nesi kutoka nje wakati tuna manesi hapa nchini. Kipato anachokipata kulinganisha na *counter part* wake tofauti ni kubwa sana, bora kukaa nae basi kwa siku mbili, tatu kuchukua ule mshahara wake kwenda kumsomesha mtu nje apate taaluma kama ya kwake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama kawaida maneno yangu siyo mengi sana, baada ya haya maneno machache sasa ningependa kuongezea *point.* *Point* hii ni ya kumalizia kwa kusema kweli. Kuna kitu kimoja hapa kidogo ambacho ningependa kuelekezwa, sijakielewa vizuri ni katika ukurasa wa 63, *section* ya sita (c).

Mheshimiwa Spika, kwanza nianze na Kifungu cha 6 (1): *"Any person who may procures, demands or imposes forced labour commits an offence.* Hapa *'may'* iondolewe kwa sababu *it doesn't make sense at all.*

Halafu *subsection 2 (c),* nikimalizia hapo anasema kwamba: *"...or placed at, the disposal of private persons.* Kuna sheria ambayo inazungumzia kwamba watu wenye makosa madogo madogo, wafungwa wenye makosa madogo madogo wanaweza wakafanya kazi katika *community* katika *disposal* ya *private person.* Naomba nipate maelezo kama hapa hakuna *contradiction* na inamaanisha nini, sielewi vizuri hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, basi maneno yangu ni hayo machache na ningependa kusema tu kwamba naunga mkono hoja hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. MARGARETH AGNESS MKANGA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja tuliyonayo sasa hivi. Kabla sijaanza kuzungumzia undani wa machache niliyonayo kuhusu Muswada huu kwanza nitoe pongezi kwa Bunge letu kuwapata Marais wawili katika taasisi mbili tumepata Rais wa kwanza wa Bunge la Afrika Mheshimiwa Mama Getrude Mongella mwalimu wangu na pia tumempata Rais mwingine kwenye ngazi ya Kimataifa kabisa sijui ndiyo hiyo *UNIT* aliyoisema mwenzangu lakini mimi nasema Baraza la Mazingira la Dunia Mheshimiwa Arcado Ntagazwa kama nimekosea mtanisahihisha.

Mheshimiwa Spika, yote haya kwangu mimi yanathibitisha kwamba nchi yetu ina watu wenye uwezo ndiyo maana hata inashangaza kwamba hata ajira ndogo ndogo eti tunawapata watu kutoka nje, hali sisi wenyewe tumo na tunaweza kufanya kazi na ndiyo maana wamechaguliwa hawa wana uwezo mkubwa ambao Tanzania kwa kweli wananchi wake wanao uwezo katika sehemu mbalimbali. *(Makofi)*

Pili, nitoe pongezi kwa waandaaji wa Muswada huu ambao ni Mheshimiwa Waziri Alhaj Profesa Kapuya, Naibu Waziri wake Mheshimiwa Mudhihir M. Mudhihir, Katibu Mkuu na watendaji na wadau wote ambao walishiriki kutuandalia Muswada huu. Nikiri kwamba Muswada huu nadhani hauna matatizo sana kwa sababu katika Muswada nyeti kama huu ningetegemea pale kwenye *gallery* wadau wengine wa kuja kutusaidia

kuchochea wangekuwa wengi au vipeperushi kule kwenye *pigeonhole* vingekuwa vingi, lakini sijashuhudia.

Kwa hiyo, hii ina maana kwamba wananchi na wadau wengi wameshirikishwa wameweza kutoa mawazo yao na basi Serikali imeweza kuyachukua yale yaliyo mengi hilo ni pongezi. Mambo kama haya yaendelee kama Mwenyekiti wa Kamati alivyosema kwamba ukishirikisha wengi kazi inakuwa rahisi na wanaona kile kitu ni kitu chao siyo kitu cha Serikali kwa sababu wote mmeshiriki. Kwa hiyo, hilo nipongezi sana.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu nilivyousoma jumla jumla naona kwa kiasi kikubwa unakidhi haja ya mahitaji ya kazi katika ulimwengu huu wa utandawazi. Lakini pia kuna machache ambayo ndiyo maana Wabunge, tupo kuweza kusisitiza au kuyarekebisha au kuyakaziakazia. Muswada huu umekidhi haja kwa sababu umeweza kuoanisha sheria mbalimbali za nyuma zilizojikalia kila mmoja kivyake huyu anasema hivi, huyu anasema hivi kiasi kwamba sheria saba za nyuma zimefutwa kabisa na mbili zimefanyiwa marekebisho zile sehemu ambazo zilitakiwa ili pawe na Muswada unaoeleweka.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuyazungumzia hayo kwa ujumla ningeomba sehemu ya pili ibara ya saba ukurasa 63 mpaka 64 unaozungumzia suala la kukomesha ubaguzi katika sehemu za kazi na kazi. Ubaguzi huo umefafanuliwa vipengele tangu *"A"* mpaka *"O"*. Mimi binafsi nimefarijika sana na uchambuzi huu kwa hivyo vipengele *"A"* mpaka *"O"* kwamba mwajiri yeyote sasa haruhusiwi hata kidogo kuwabagua wafanyakazi wake katika kipengele kimojawapo kati ya hayo.

Lakini mimi *concern* yangu sana ni pongezi kwamba kipengele *"J"* kama sijakosea kimesema kabisa hakuna ubaguzi hasa katika hali ya ulemavu. Nadhani ni mara ya kwanza sheria imeweka wazi jambo hili kwamba sasa hakuna ubaguzi wa ajira wa kazi hata kwa watu wenye ulemavu.

Kwa nini nilipongeza hili, mimi ni mmojawapo bahati nzuri mimi sikubaguliwa lakini watu wenye ulemavu wengi kabisa kwa muda mrefu wamejiona kwamba hawawezi kupata ajira hata wale wenye taalum zinazostahili kutokana na suala hilo kwamba mwajiri akiangalia anasema eh! Naye huyu wa nini atapandaje huko ghorofani?

Kwa hiyo, kwa muda mrefu wamejiona kwamba wanatengwa katika kupata ajira kwa misingi ya ulemavu wao.

Sasa kwa Muswada huu hilo halimo kwa hiyo, naamini kabisa kwamba uwezekano wa kubaguliwa wa aina hiyo hautakuwepo na kwamba Muswada umezingatia sana *convention* ya 150 ya Shirika la Kazi la Dunia *article* namba 4 inayosisitiza usawa wa wafanyakazi kuwa na usawa wa wafanyakazi, kati ya wafanyakazi wenye ulemavu na wafanyakazi wasiyo na ulemavu.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo hapa ningeomba kutoa ushauri kwa Serikali na hata kwenye Muswada huu sijui mtaweka kwenye kanuni sina uhakika. Ili hili kuweza

kuzingatiwa na waajiri mbalimbali ikiwa ni Serikali au waajiri binafsi ambao wanakuja na wataendelea kuwepo ni kwamba ihakikishwe basi kwamba waajiri hawa wanaweka mazingira muafaka kwa wafanyakazi wenye ulemavu katika sehemu zao za kazi, kinyume chake itakuwa ni maneno ya kuremba lakini utekelezaji hautakuwepo katika kundi hili.

Mheshimiwa Spika, jingine ambalo naomba nishauri ni kwamba pamoja na kwamba hii sheria tutaipitisha bado hisia za jamii kwa watu wenye ulemavu hazijawa na mwelekeo mzuri sana. Nishauri tu kwamba waajiri watakaoweza kuwaajiri watu wenye ulemavu wale ambao wana taaluma hizo zinazostahili waweze basi kutoa motisha kwa sababu kwa kufanya hivyo wametekeleza jukumu la kuwawezesha watu wenye ulemavu kuweza kupata ajira kama watu wengine kwa hiyo, labda wapewe motisha na hiyo itasaidia na wengine kuona kwamba kuna stahili na uhalali wa kuajiri watu kama hawa.

Niseme kama nilivyosema siku za nyuma, watu wenye ulemavu kama mtu ana ujuzi wa suala huwa wanafanya kazi vizuri siyo wategaji hawawezi kuondoka ovyo wanakuwa makini wakijua kwamba hapa hapa ndiyo chakula changu, ndiyo mlo wangu, tofauti na wengine wanaweza wakatokatoka kwenda kunywa chai na kadhalika kumbe masaa yanakwenda. Kwa hiyo, hilo naomba nilisisitizie hapo.

Muswada umenifurahisha kwa sababu umetoa uhuru kwa waajiri na waajiriwa kuweza kuunda vyama vyao na wao wakaweza kujadiliana na kuelekezana masuala mbalimbali na hii inasaidia kuleta utulivu katika mahali pa kazi, hii inasaidia kuongeza tija kama Mheshimiwa Waziri, alivyotuelekeza katika maelezo yake ya mwanzo.

Mheshimiwa Spika, ukurasa 71 *section 19* kipengele cha pili kimezungumzia siku za kufanya kazi kwamba zitakuwa ni sita au masaa 45. Sasa mimi nimetatizwa kidogo hapo pa siku 6, siku 6 tunaihesabu tangu Jumatatu mpaka Jumamosi na kama Jumamosi sasa itakuwa siku ya kazi. Je, tunafuta ile ya kwamba wafanyakazi Jumamosi angalau mkalimelime mkaangalie michicha?

Kwa hilo labda ningependa nipate ufafanuzi hapo kwamba hivi Jumamosi sasa itakuwa ni siku ya kazi au hizi siku 6 tunazihesabu kutoka siku gani?

Mheshimiwa Spika, nimefurahishwa pia katika Muswada huu kuona kwamba suala la wafanyakazi kukatwa mishahara bila ridhaa yao kwa Muswada huu na hasa sheria itakapopita hilo nalo limekwisha kwa sababu imekuwa kero. Mimi nilikuwa mwalimu ilikuwa kero unakuta mwisho wa mwezi shilingi 20,000 zimekatwa, ukiuliza unaambiwa aa! Wizara itatueleza baada ya, kwa kweli ilikuwa ni kero na nadhani siyo walimu tu ni kila mahali kulikuwa na mchezo huu. Mishahara ya watu inakatwa tu bila taarifa, taarifa unakuja kupewa baada ya kukatwa mshahara, siyo kabla ya kupata mshahara.

Kwa hiyo, hili nimeona nalo litawasaidia wafanyakazi wawe na amani wajue hela yao inakwendaje pamoja na kwamba wataambiwa yale makato wanayotarajia kukatwa

wataelezwa wataelewa, sidhani kama itaweza kuwa mgogoro, ilikuwa na mgogoro kwa sababu ilikuwa inafanyika kabla ya taarifa na maelekezo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo mimi niseme kwa ujumla Muswada huu ni mzuri umezingatia masuala yote ya wafanyakazi na waajiri. Ila tuweze kurekebisha na kufuatilia yale ambayo yanapaswa kufuatiliwa kwa mfano wakaguzi hawa wa sehemu za kazi na nini wawe *serious* na yale makosa makosa yasionewe haya kuweza kuyarekebisha ili tuweze kuendelea kuwa na sehemu za kazi zenye utulivu na amani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naunga tena mkono hoja niliyoyasisitiza yazingatiwe ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. LEONARD M. SHANGO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia kidogo katika Muswada huu.

Kwanza kabisa naunga mkono hoja Muswada huu kwa asilimia mia kwa mia. Pili, nampongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu wake, Wizara yake na Kamati ya Bunge iliyofafanua Muswada huu. Pia nachukua nafasi ya peke kabisa kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Getrude Mongella na Mheshimiwa Arcado Ntagazwa kwa nafasi zao za juu walizozipata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi sina mengi ya kuzungumzia katika Muswada huu, lakini nitaomba ufafanuzi katika mambo fulani fulani. Kama tunavyoelewa mwajiri mkubwa kabisa katika nchi hii na siyo nchi hii tu katika nchi nyingi ni Serikali au sekta ya umma.

Sasa huu Muswada unatamka nini kuhusu wafanyakazi katika sekta ya umma? Tunavyoelewa sasa hivi wafanyakazi katika sekta ya umma, ndiyo wanaosota zaidi mishahara midogo, maslahi madogo wanastaafu wanafuatilia maslahi yao wanapata matatizo na wengine wanakufa kabla hawajafaidika. *(Makofi)*

Sasa hii sheria lazima itamke wazi hivi kama siyo kunyanyasa ni nini? Hawa ni wafanyakazi ambao tuseme ni wengi zaidi katika taifa hili katika Serikali kwa sababu wao ndiyo ambao wanaendesha nchi, wanaendesha uchumi. Sasa hii sheria iweke wazi kuwa Serikali/umma kama mwajiri nayo izingatie sheria hii kuwatendea haki wafanyakazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili ningeomba kujua sheria inatamka nini kwa wafanyakazi ambao wana wito? Kuna wafanyakazi wa kawaida ambao wanakwenda kufanya kazi kwa sababu wanataka ajira, kuna wengine ni wito *(professional interest)* na *commitment.* Kwa mfano walimu, waganga na watumishi wengine katika sekta hii. Ni sekta nyeti za kutoa huduma kwa wananchi. Lakini ukitazama hali zao siyo nzuri ukizilinganisha na sekta zingine. *(Makofi)*

Kwa hiyo, sheria hii itoe mwongozo na ielekeze kuwa katika sekta ambayo wafanyakazi wana wito, wana *interest,* wana *commitment* wapewe motisha maalum kwa mfano sasa hivi watu wanaoingia katika walimu ni wale wanaotafuta tu kazi siyo kuwa wana *interest* katika kufundisha kwa sababu walimu ambao wana *interest* wamekwishaondoka wamekwenda mahali ambako kuna maslahi zaidi.

Mfano zaidi katika Wilaya yangu shule nyingi za sekondari na shule za msingi hazina walimu kwa sababu walimu wanakataa kwenda kwenye vituo walikopangiwa kule kwa sababu maslahi ni duni na pili maeneo mengine yanaweza kuwa ni mazingira magumu ya kazi *(hardship work stations).* Sasa unapomlipa mwalimu au mganga anayepelekwa kwenye Mkoa kama wa Singida au Rukwa umtoe Dar es Salaam unategemea nini? Unamlipa posho au maslahi yale yale kama mwenzake ambaye atabaki Dar es Salaam?

Kuna mfano mzuri sana rafiki yangu mmoja alikuwa daktari Moshi akahamishwa kwenda Sumbawanga, alipoondoka akaenda kwenye kituo cha basi akaamua hapo hapo badala ya kwenda Sumbawanga akaenda Mombasa mpaka leo amezeekea Mombasa anatibu kule kwa sababu aliona kuwa hawezi yeye kwenda kwenye eneo ambalo anaona kuwa mazingira ni magumu ya kufanyia kazi. Sasa ndiyo ingekuwa labda Muswada huu uelekezwe kuchora ramani ya mazingira ya vituo vya kazi kusudi mtu anapopelekwa kwa mfano kwenye mahali ambapo panaonekana pagumu apewe motisha maalum, siyo suala la kulipwa au kutoka pale alipotoka ambapo alikuwa amezoea mahali pazuri halafu apelekwe huko maporini.

Sasa kama Muswada huu hautaelekeza maana yake wananchi wetu walio wengi vijijini hawatapata huduma za kutosha kwa sababu wale watalaam ambao wangekwenda kule watakataa kwenda na watapelekewa labda wale watalaam wafanyakazi ambao wanataka kazi tu, hata aende wapi kwa sababu hana sifa ya taaluma ile lakini atakwenda kule kwa sababu atapata mshahara. *(Makofi)*

Sasa mimi ningeomba Muswada huu uwaangalie na uelekeze na utoe tamko kuhusu suala la motisha katika mazingira ya kazi kwa wafanyakazi awe wa umma awe wa makampuni binafsi. Sasa kuna wakati mwingine wafanyakazi wanapelekwa kwenye maeneo magumu ya kufanyia kazi *(hardship work stations)* kwa sababu au anaadhibiwa na *boss* wake, au ni kwa chuki binafsi na *boss* wake. Sasa hii ni kumnyima haki mfanyakazi na kumkandamiza. Sasa sheria hii inasema nini? Kama mtu anapelekwa mahali ambapo anajua ni *hardship* na haelewi na haeleweshwi sasa akiacha kazi au akikataa kwenda anapunguzwa kazi. Sasa akipunguzwa kazi kwa sababu ya kutotii amri ya kuhamishwa itakuwa ni kumnyanyasa na kumnyima haki yake.

Sasa ningeomba hii sheria itazame kwa undani wale wanaochukua sheria mikononi mwao na kuwahamisha wafanyakazi na kuwapeleka kwenye maeneo ambayo wanaona kwamba ni adhabu. Hili linafanyika sana katika Idara za Serikali, Mashirika ya Umma watu ambao msipokubaliana na boss unaweza ukapelekwa mahali ambapo hapaelewi, ukipata adabu kidogo ndiyo utarudishwa labda.

Pia, ningeomba sheria hii pia iangalie suala la migogoro ya wafanyakazi wengi ambapo kwa miaka mingi imeendelea. Sasa sheria hii labda itamke kuwa kama kunakuwa na migogoro kama hii ambao labda iko mahakamani, mahakama ya kawaida au katika mabodi ya usuluhisho basi mahakama kama hii ambayo tunaiunda kwa kupitia sheria hii iangalie kuchukua na kuharakisha kumaliza matatizo ya migogoro hii. Nina mfano mzuri kwa mfano wafanyakazi wa urafiki mpaka leo hawajalipwa wanazungushwa, mwajiri wao yupo na wizara mama ipo. Sasa kwa nini tunawatesa wafanyakazi wa urafiki mpaka leo waliopunguzwa wasipate maslahi yao? Nani atawalinda? Vile vyama vya wafanyakazi ambavyo tunavitamka katika sheria hii vimekuwa hapa katika nchi hii kwa miaka mingi sana, lakini havifanyi kazi ya kutosha kuwalinda wanachama wao. Sasa sheria hii i wajibishe vyama hivi, mashirika haya wafanyakazi kuwa wawatetee wafanyakazi wao. Wafanyakazi kama wa Urafiki wana chama chao ambacho wanakitumia lakini sidhani kama tumepata kufanya kazi vizuri mpaka leo kwa sababu wanasota wale waliopunguzwa.

Kuna pia wafanyakazi wa *UFI,* wafanyakazi wa *Elimu Supplies,* Wafanyakazi wa *Tanganyika Packers,* wote mpaka leo wanasota hawajamaliza kupata maslahi yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi ningeomba katika Muswada/sheria hii iwekwe wazi kuwa kazi fulani fulani ziorodheshwe kama *schedule* namba 5 kuwa hizi kazi ni za Watanzania tu, ziorodheshwe kisheria hapa na zitakuwa zinaongezeka kadri Watanzania wanavyopata ujuzi katika maeneo fulani fulani ambayo sasa wageni wamechukua nafasi. Kwa hiyo, ningeomba orodha hii iwekwe kisheria pia kwa kazi fulani fulani mwajiri yeyote hawezi kumleta mtu kutoka nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa kuna suala la familia, wafanyakazi wanapohamishwa kutoka kituo fulani kwenda mahali fulani, lakini katika kuhamishwa ana familia watoto wanasoma labda mama anafanyakazi au mume anafanyakazi lakini *there is no consideration* anahamishwa tu na kupeleka na hii inakuwa kama ni kuvuruga na kudhoofisha familia ile ambayo inapewa uhamisho. Ningeomba sheria hii itamke waziwazi kuwa unamhamisha mtu angalia maslahi mengine kama yatakuwa yamekidhi. Watoto wanasoma shule sasa kama unapeleka mahali ambapo hakuna hata shule kama shule ya sekondari na bado tegemezi kwa wazazi, sasa watoto watakaa kwa nani? Au mmojawapo katika mama na baba mmojawapo anafanya kazi, akihamishwa kule hatapata mwingine kazi sasa inakuwa pato linakuwa ni la mtu mmoja. Sasa kweli hapo tunaitendea haki familia hiyo? Kwa hiyo, ningeomba hii sheria imulike mambo haya na iweke sawa. *(Makofi)*

Baada ya kusema hayo, tena narudia kusema naunga mkono Muswada huu kwa asilimia mia kwa mia. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. ZAHOR JUMA KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili nami niwe miongoni mwa wachangiaji asubuhi hii.

Mheshimiwa Spika, naomba moja kwa moja katika mchango wangu nijielekeze kwanza kuhusiana na masuala haya yanayohusiana na ajira za wageni. Nimejaribu kupitia hii sheria kwa bahati mbaya sana sikuona sehemu ambayo inaweka taratibu zinazoelekeza wageni watakaokuja Tanzania, taratibu zao za ajira zitakuwa ziko vipi na viwango vyao ambavyo vitawatofautisha kati ya wenyeji na wageni.

Wenzangu waliotangulia kuchangia wamelizungumzia suala hili. Kwa kiasi ninachofahamu kama sikosei sana katika sheria ya uhamiaji kumewekwa taratibu pale nadhani zinazohusiana na vibali vya ajira kwa wageni. Lakini ingekuwa ni vyema kama taratibu hizo zingekuwa chini ya sheria hii hasa kwa kuzingatia kwamba sheria hii ndiyo inayohusika au Wizara hii ndiyo inayohusika na kujua pengine hata zile *categories* za wafanyakazi namna wanavyohitajika katika sekta mbalimbali ndani ya nchi. Kwa hiyo, sehemu moja ya upungufu ambao nimeuona na nahisi kuna haja ya kuufanyia kazi ilikuwa katika masuala yanayohusiana na ajira za wageni.

Mheshimiwa Spika, nikiondoka hapo nielekee katika kifungu kinachohusiana na ajira za watoto, kifungu cha tano. Katika kifungu hiki kimezuia tu kwamba mtoto yeyote chini ya miaka 14 hataruhusiwa kuajiriwa, kwa maana miaka 14 na kuendelea juu hawa wanaruhusiwa kuajiriwa, isipokuwa chini ya miaka 18 hawataruhusiwa kuajiriwa katika zile kazi za hatari.

Nadhani kwa maelezo haya au kwa mwelekeo huu napata mashaka kwamba sasa tunaweza tukaelekea kufungua milango ya ajira za watoto kwa sababu miaka 14, 15, 16 tunaelewa uwezo wao wa maamuzi, uwezo wa kufikiri kwamba bado hawa ni wadogo kulinganisha na mazingira mazima ya suala zima la ajira.

Hivi sasa kuna tatizo kubwa sana la ajira za watoto hasa katika kazi za nyumbani. Usimamizi wa sekta hiyo ni mgumu sana kupata maelezo, masuala ya mikataba na mambo mengine chungu nzima. Sasa tunaposema kwamba labda katika zile kazi ambazo zitakuwa na madhara kwa wao ndizo hizo hawaruhusiwi.

Sasa kugawanya hayo maeneo najua kuna kifungu humu, nadhani kifungu cha 6 katika kifungu hicho hicho cha 5(6) kimeelezea kwamba Waziri ataweka kanuni ambazo zita-*classifies* hizo zinazoitwa *hazardious form of work.* Lakini nadhani bado kuna maeneo yatakuwa yanamwanya bado, tuchukulie mfano, kunyanyua vitu vizito hiyo pia ni kazi ambayo itakuwa na madhara, lakini inaweza ikawa huyu mtoto kutegemea vile vile na namna ya umbo lilivyo na uwezo wake wa maumbile.

Mtoto wa miaka 15 mpaka 17 inaweza ikawa kwa huyu mmoja kunyanyua kilo kumi isiwe kazi hiyo ina madhara kwake yeye, kwa mwingine kazi hiyo ikawa na madhara. Pengine kutofautisha hicho kutahitaji vipimo vya kidaktari kuweza kutofautisha vipi watakuwa na madhara au hayapo hayo madhara. Lakini hapo sasa tumeshafungua milango, ruksa huyo kuajiriwa.

Kwa hiyo, bado mimi naona kwamba kutakuwa kuna mwanya hapa wa hawa watakaoajiriwa hapa kushindwa kuwalinda ipasavyo hiyo moja. Pili, sijui Serikalini,

Serikali imejiandaa kwa kiwango gani, hivi kweli Serikali itakuwa tayari kuajiri watoto wa miaka 16? Kwa maana hiyo sasa itakuwa ni *right* yao kudai na wao wanayo haki ya kuajiriwa Serikalini, pengine ukimwajiri kama karani na kazi zingine ambazo hazina madhara. Kwa mtazamo huu wa hapa huo mwanya upo na sasa watakuwa na *rights* za kudai haki hiyo kwamba na wao wanayo haki ya kuajiriwa.

Sasa hilo nalo tungeliona na kwa maana hiyo, nina wasiwasi na kifungu hiki kwa kiwango gani kitalinda maslahi ya hawa watoto hata hilo eneo tunalosema kwamba labda hiyo ruksa itatolewa iwapo katika kazi za kujifunza, nadhani hiyo pia nayo bado kwa mtazamo huu wa hapa iko *vague.* Nadhani zingelikuwa kwa yale mafunzo zile ambazo ni *registered* tu vinginevyo watawatumia hawa watoto halafu kisingizio kwamba wanajifunza. Kwa hiyo, hilo nalo tungeliangalia katika zile labda *registered, Vocational Training or Schools.*

Nikiondoka hapo niende kifungu cha sita ambacho pia pamoja na madhumuni yake ni kuzuia hiyo *forced labour* lakini bado hiki kifungu mimi nakiona kina wepesi, kimejieleza tu katika ile ibara ndogo ya kwanza kwamba kufanya hivyo litakuwa ni kosa. Anasema hii *forced labour commit an offence,* sawa, lakini sasa ukiangalia huku mbele inavyoendelea na sina hakika kwamba hii *forced labour* imekuwa *defined* humu.

Lakini bado nina wasiwasi na kipengele hiki namna kilivyoendelea huku mbele kwamba kazi zipi zitatofautishwa na hiyo *forced labour* na namna ambavyo tukirudi kundi lile lile la watoto na wale vijana wadogo watakavyolindwa na hilo tatizo la *forced labour* hasa katika mazingira ya kazi za majumbani. *Okay,* hiyo sheria labda itakayofuata baadaye hizo *labour institutions,* kutakuwa na ukaguzi lakini si rahisi kufanya ukaguzi katika nyumba na ukaweza kugundua kwamba pana *forced labour* au hakuna kwa hii kuzingatia masaa ya kazi pale bado pana tatizo. Kwa hiyo, hili nadhani Mheshimiwa Waziri anaweza akatusaidia vipi ataweza kulizingatia suala hilo.

Nikielekea kifungu cha 20, Mheshimiwa Spika, katika kifungu cha 20 nakusudia kuzungumzia kuhusu *night work.* Kwanza hii *night work* sasa hivi nadhani kama sikosei ni saa 2 za usiku ndiyo tuna-*define night* mpaka 12 za asubuhi. Tutakapokuja kuangalia kwa wale wanawake labda tuseme wenye watoto wadogo wanaonyonyesha baada ya kumaliza *maternity leave* amerejea kazini na inategemea sasa hatua ya kutoka sehemu yake ya kazi mpaka nyumbani pengine napo panaweza pakawa na *distance* ya kutumia masaa mawili, kutoka kazini saa 2 kufika nyumbani saa 4 na mazingira ya matunzo ya mtoto mchanga. Nadhani hili suala pia kuna haja tungeliangalia kwa maslahi ya mtoto. Pamoja na kwamba kipengele (b) katika *sub-section two* kimeelezea, *before that if mother, no no* hii nadhani inahusiana na masuala la kujifungua. Kwa hivyo, hapo pia nahisi pana tatizo ambalo linaweza likawa siyo zuri kwa maslahi kwa mtoto.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 31 kinachohusiana na masuala haya ya *annual leave* ndani ya Sheria hii kumeelezwa kuhusiana na siku za mapumziko na *public holidays,* zile zimetambulikana. Zinakubalika kwamba hizo ni *non working days.* Lakini unapo-*count annual leave* unasema, zitahesabika siku 28 zinajumuishwa kila kitu, hiyo *off days, public holidays* zote zinakuwa *ccounted* pamoja. Mimi nadhani hii sio sahihi

na si utaratibu nzuri. Kwa sababu tunazungumzia likizo yule anapumzika siku za kazi. Zile nyingine ni *right* yake hata kama angelikuwepo kazini. Lakini hapa zinafutwa zote zinahesabika moja kwa moja tu, Jumapili, sijui kama kuna *Chrismas,* Pasaka zote zinakuwa *counted* kukamilisha *28 days leave.* Sasa hii nayo nadhani kidogo nalo hilo ni tatizo tungeliangalia kwamba zikawa kama ni *28 days,* au *26 days* lakini zikawa ni *working days* ambazo hizo nadhani ni sahihi zaidi kuzi-*count* kwamba hizo ndiyo zinazostahiki kwa likizo.

Mheshimiwa Spika, nikienda katika kifungu cha 33 pale katika *sub-section 1,* kinachozungumzia *notice shall be supported by medical certificate.* Hapa kidogo sijafahamu iwe *supported* na kitu gani, kwamba huyu mama hapa kwamba ni *pregnant* au anategemea kujifungua ndani ya miezi mitatu au hiyo *medical certificate* iwe ina-*satisfy* kitu gani? Hapa nikikisoma hiki kipengele sipati picha kamili hiyo *medical certificate* hapa inathibitisha kitu gani.

Kwa hivyo hapa nadhani kidogo Mheshimiwa Waziri atatusaidia nini hasa kinachohitajika. Halafu nikienda kifungu kidogo cha 6 hapo katika kifungu hicho hicho cha 33(b) ambacho kinasema *100 days paid maternity leave, if the employee gives birth to more than one child at the same time.* Sasa wanina wasiwasi ya hatari za kuja kutokea ulalamishi tunapotumia hili neno *more than one at the same time.* Wako wengine wanapojifungua hubahatika, akatangulia wa kwanza, akafuata wa pili. Sasa wapowanaopishana mmoja asubuhi mmoja jioni sasa hii itakuwa *the same time or the same day?* Mmoja kazaliwa leo mwingine kesho. Kidogo hapa napata matatizo. *(Kicheko)*

Ningeliomba pengine hili ukatusaidia kutofautisha kati ya *the same time and the same day.* Au siku ya pili, nina wasiwasi wa kutokea matatizo ya waajiri wakakuambia hawa hawakuzaliwa siku moja, walizaliwa siku mbili tofauti, mmoja ilikuwa tarehe moja mwingine tarehe mbili. Pengine huwa kuna tofauti ya masaa pengine 12. Sasa hili nadhani tungeliona pengine labda tukasaidiana hapa ufafanuzi wake uko vipi hasa.

Mheshimiwa Spika, nikienda kifungu cha 44. Nitaanzia pale 42, ni kuhusu *severance pay* inazungumzia nitaanzia mstari wa pili, *about at least to seven days, basic wage for each completed year of continuous service.* Hiki sijui tumechukulia kigezo gani kwa kiasi nilichokifahamu kipengele hicho nikikiunganisha na kile cha 44 kwa maana hiyo mkataba utakaovunjwa tuseme na mwajiri lakini hiyo ni ile ya *unfair termination,* kule mfanyakazi maana yake atakachostahiki kulipwa ni zile *seven days* kwa hesabu niliyofanya *multiplied by number of years of service.*

Sasa hapa napata mashaka, ukichukulia *let say* mshahara uwe laki moja, *seven days,* tuseme tuigawanye *by four* inakuja karibu *twenty five thousand to multiply by number of year of service* kwa mwaka mmoja mfanyakazi huyo maana hapa atakacholipwa na mwajiri wake tuseme ni 25,000 nahisi ni *very small amount*.

Sasa sijui kigezo hapa kilitumika kitu gani ku-*determine* hii *figure* au sijui kama kuna hizo *international conventions* kidogo pia ningeliomba Mheshimiwa Waziri atusaidie ili kuona *balance* aliyoitumia katika kufikiria kitu hicho.

Halafu kunako hivi vyama vya wafanyakazi, na vyama vya waajiri, kwa sheria inavyofafanua kifungu cha 45 zinaruhusika kufanya kazi nadhani katika ule muda wa miezi mitatu kama sikosei kabla ya kupata hata ule usajili ambapo ndani ya kipindi hicho waweze kufanya taratibu za usajili. Suala langu linakuja kwamba iwapo kesi inasimama Mahakamani, chama hakijasajiliwa hili *legality* inakujakuja vipi. Nadhani tunaweza tukapata tatizo, kwa hivyo hili nadhani tungeliangalia tena kuona vipi tutaepuka, pengine akienda kwenye usajili chama hicho kikakataliwa wakati huku mwanzo kimesha-*represent interest* iwe za wafanyakazi au *interest* za waajiri. Pengine kukawa kuna matatizo kunako *constitutions* zao na mambo kama hayo.

Mheshimiwa Spika, muda umeisha, kwa hiyo, mimi nimalizie kusema naunga mkono Muswada huu na ningeomba hayo pia yazingatiwe. Ahsante Mheshimiwa Spika. *(Makofi)*

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwa kukushukuru kunipa nafasi ya mwisho asubuhi hii na mimi kutoa maoni yangu juu ya Muswada ulio mbele yetu. Na vile vile nimpongeze Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri, Katibu Mkuu wake na Watendaji wote wa Wizara hii kwa kazi kubwa walioifanya katika maandalizi ya Muswada huu mpaka kufikia katika hali hii.

Mheshimiwa Spika, niruhusu nimpongeze sana Mheshimiwa Getrude Mongella, kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Bunge la Afrika. Na vile vile nimpongeze Mheshimiwa Arcado Ntagazwa kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Baraza na Mazingira Duniani. *(Makofi)*

Naendelea kuipongeza Serikali kwa kuleta Muswada huu wa kurekebisha Sheria za kazi zilizopo kwani kwa kweli zimepitwa na wakati na nampongeza sana Mheshimiwa Juma Kapuya, kwa maelezo yake aliyoyatoa jana kwamba amewashirikisha wadau wengu katika maandalizi ya Muswada huu, ni jambo la msingi.

Lakini Mheshimiwa Spika, kuwashirikisha au kushirikishwa ni jambo moja, mnapokubali yale waliosema ni jambo lingine. Sasa pamoja na majigambo kwamba amewashirikisha wengi. Lakini watapimwa kwa kiasi gani ameyakubali na kuyazingatia yale ambayo yamesemwa na wadau katika marekebisho na kuboresha Muswada huu. Pengine anaweza akatueleza hapo baadaye.

Mheshimiwa Spika, katika Muswada huu sikusikia chochote kuhusu sheria ya *Work Mans Compensation* ambayo ndiyo imepitwa zaidi na wakati na ambayo mimi binafsi takriban mabunge kadhaa yaliyopita nimeipigia sana kelele kwa sababu kwa kweli hali ilivyo sasa ya kutoa shilingi elfu 84 kwa mtu aliyefariki na kulipa shilingi laki moja na nane kwa *total in capacitation* ni thuluma tena ni thuluma kubwa.

Mheshimiwa Spika, nilitazamia kwamba katika sheria hii kipaumbele kingetolewa katika mambo kama hayo, kulikoni haya ambayo yameletwa ingawa yote ni muhimu. Lakini mimi nilidhani ile sheria ya *Compensation* kwa kweli inahitaji *attention* ya haraka zaidi. Sasa sikusikia chochote.

Sasa kama itakuja baadaye niombe sana Mheshimiwa Spika, iletwe haraka, kwa sababu wafanyakazi wanaisubiri kwa hamu, maafa yameshatokea mengi ya *Railways* hapa na mengine. Basi ni vizuri Serikali ikaharakisha kuuleta Muswada unaohusu *Work Man Compensation and Social Securities* zingine ambazo au wataona inafaa.

Mheshimiwa Spika, vile vile nieleze hisia zangu kwamba marekebisho ya Sheria hizi zimerekebishwa kwa mtazamo wa kumlinda zaidi mwajiri au mwekezaji kuliko mfanyakazi. Huu ndiyo mtazamo wangu na maelezo ya jana ya Mheshimiwa Waziri alipokuwa anawasilisha hoja yake alieleza hivyo.

Mheshimiwa Spika, nia ni kuangalia tunakwenda wapi, tunaangalia vipi, tuko wapi na kadhalika. Serikali lakini inanipa hisia kwamba mwelekeo ni kumlinda zaidi mfanyakazi kwa kisingizio cha kulinda ajira, jambo zuri, lakini *not at the expense* ya wafanyakazi au ya wananchi.

Matazamio yangu ni kwamba Sheria hizi zitamlinda pia mfanyakazi kama ambavyo zinavyotazamiwa kuwalinda wote wawili waangaliwe vizuri zaidi siyo upande mmoja uegemee kama inavyoonekana sasa. Kinachonisikitisha zaidi ni kwamba Serikali imethubutu kupunguza hata yale marupurupu na mafao yaliyopo sasa kwa wafanyakazi ambayo tayari yapo kwa mujibu wa sheria zilizopo, imethubutu kuyapunguza, badala ya kuyaboresha.

Mimi nadhani siku zote *changes is better*, lakini huwezi kufanya *changes* tena wewe ukajipunguzia, ukapunguza yale yaliyopo sasa. Mimi sikubaliani na *concept* hiyo. Lakini hapa ndivyo inavyoonekana, kwa mfano, katika kifungu cha 32(ii) ukurasa wa 79 likizo ya ugonjwa.

Likizo ya ugonjwa kwa sheria za sasa mfanyakazi anapoumwa ukiacha yule ambaye anaumia kazini anatibiwa miezi sita, anapata mshahara kamili na miezi sita anapata nusu mshahara. Ndivyo ilivyo sasa. Lakini katika sheria hii katika Muswada huu, Serikali imethubutu kupunguza hata hilo kwa mgonjwa kitu ambacho mtu hajitakii na kufanya sasa iwe siku 63 kwa mshahara kamili na siku 63 kwa nusu mshahara. Hapo mimi ndiyo kidogo natatizika hapo.

Yaani tumerekebisha sheria ili kuwaonea zaidi wafanyakazi hata katika ugonjwa basi, nani anataka kuugua? Vinginevyo tutaji-*contradict* kwamba hapa anakatazwa mgonjwa wa UKIMWI. Jambo ambalo siku zote hapa tunasema, sijui *stigma,* tuwasaidie watu wa UKIMWI, tutawasaidiaje wakati umeshambana kwenye sheria hii kwamba unamwona yeye ndiyo anachukua muda mrefu kutibiwa mpaka inafika miezi kadhaa. Leo sasa unaweka kifungu cha siku 63 mshahara kamili na siku 63 nusu mshahara.

Mheshimiwa Spika naona hapo kuna kasoro kubwa sana. Niliomba hilo liangaliwe, angalau basi wangesema nusu ya ule muda wa zamani kwa maana ya kwamba walau miezi sita, mshahara kamili na wamemdhamini miezi mitatu mshahara kamili na miezi mitatu ni mshahara hata angalau siku 90. Ndiyo nasema mwelekeo hapa ni kumlinda mwajiri na huyo anayedaiwa mwekezaji kwa kisingizio cha kulinda ajira. Lakini *at the expense* ya wafanyakazi.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo nasema wamethubutu kulipunguza wakati lipo ni kwamba katika kumbukumbu la mfanyakazi yeyote mahala pake pa kazi ni kuwa na *place of domicile* lakini katika Muswada huu limeondolewa kabisa lisionekane katika kumbukumbu za mwajiri. Imeonekana *a place of recruitment.* Katika ukurasa wa 69 kifungu cha 15(1)(b) kwamba katika rekodi aonyeshe tu mtu ameajiriwa wapi lakini siyo kwao.

Hii Mheshimiwa Spika, maana yake ni kwamba mfanyakazi wa Singida, Mwanza, kule Ukerewe na Mafia kule, hawezi akaajiriwa kupitia kule. Sasa hivi unaweza ukaajiriwa ukitokea Mafia, ukaomba kazi, ukawa huna sifa ukaajiriwa.

Lakini kwa sheria ya sasa wewe mtu wa Mafia na mtu wa Ukerewe huwezi kuajiriwa kama sisi wa Singida huwezi kuajiriwa kwa sababu unaonekana unakaa mbali. Tutaanza kuweka kitu cha ubaguzi hapa, wale walio karibu na viwanda na kwa sababu viwanda vingi viko Dar es Salaam basi ndiyo watakaopata kazi. *(Makofi)*

Wale wa mbali hawatapata kazi. Hata wale wa Tabora kule Urambo hawatapata kazi. Mimi nadhani hapa nako kuna kasoro. Mimi nasema sheria nia yake ni kurekebisha ili kuboresha. Lakini haya yaliyopo sasa wakati wafanyakazi wanasafirishwa wao na wake zao mpaka nyumbani kwao unawaondolea.

Sasa ndiyo umeboresha au umeharibu. Hili nalo ni la pili ambalo nilidhani wenzetu hawa kwa kweli katika sheria hii hawakuwatendea haki wavuja jasho wa nchi hii na wameangalia zaidi huyo mwajiri na mwekezaji. Nimeshasema siku zote *change* ya siku zote zinatakiwa zilete mambo mazuri.

Mheshimiwa Spika, katika sheria zilizopo sasa liko tatizo la kutowalipa wafanyakazi pale kiwanda kinapobinafsishwa au kinapofilisika. Sasa nimeangalia katika hali hii sikuona kifungu hasa mahsusi kinachowafaa au kinachowafanya wafanyakazi nao walipwe madeni yao pale ambapo kiwanda kinafilisika. Kwa sheria ya sasa ni kwamba madeni mengine yote yanalipwa, haya ya wafanyakazi kama mishahara na marupurupu mengine ni ya mwisho kabisa kama pesa zitabaki, vinginevyo hawalipwi kitu chochote. Sasa nimwombe Mheshimiwa Waziri anieleze ni wapi kifungu hicho kipo mimi nimeangalia sikuona na ni kifungu 27 basi naomba akirekebishe ili kusudi kwa kweli madeni ya wafanyakazi yaende sambamba na madeni mengine yoyote pale kiwanda kinapofilisika au kiwanda kinapokuwa hakifanyi kazi tena. *(Makofi)*

Katika ukurasa wa 85 kifungu namba 40(3) mimi nasema kifutwe. Kifutwe kabisa kwa sababu kinasema kama Mahakama yameshaamua na msuluhishi kaamua

mfanyakazi arudi kazini anapewa tena mwajiri nafasi ya kufikiria ama arudi au asirudi, kwa nini? Yeye alishamfukuza. Tumekwenda kwenye vyombo vya sheria vimesema mrudishe kazini, halafu tena anaambiwa hebu angalia unaweza au huwezi. Umlipe mishahara ya miezi 12, wapi tunakwenda hiyo. *(Makofi)*

Mimi nasema hicho kifutwe. Na kama ni lazima basi aende Mahakamani tena akaombe kibali, aeleze sababu za msingi na faini pale au nini fidia ile iwe si chini ya miaka miwili kwa ushauri wangu mimi. Ili aone *pinch* watu wengine wanaondolewa kwa sura yake mbaya tu. *(Makofi)*

Inaweza kuwa mimi unene wangu unaweza kuwa kikwazo kazini nikaondolewa tu. Kwa hiyo, naomba isiwe *automatic* lakini vile vile nakubaliana na pendekezo la kuwa kesi za kikazi zishughulikiwe Mahakamani lakini najua taratibu za Mahakama kuna malipo na kadhalika na kadhalika. Ningeomba wafanyakazi hawana kitu, hali zao taabani, duni, hoi, hawana kitu, kama inabidi iende Mahakamani basi ile kwa kweli isihusike na mambo yale sijui ya kujiandikisha na kadhalika na kadhalika. Na nyinginezo ambazo zitakuja huko mbele ya safari.

Mheshimiwa Spika, zile ambazo zinakwenda Mahakama Kuu, Mahakama Kuu sasa ziko *centralized* ni matumaini pia Kanda hizi ambazo zipo zipewe nafasi vile vile za kushughulikia kesi hizi kwa mujibu wa Muswada huu au wa Sheria hii kulikoni ku-*concentrate* Dar es Salaaam peke yake. Makesi ni mengi na *experience* ni kwamba sasa hivi Mahakamani kesi zinakuwa zinachelewa sana hapa Mahakamani.

Mheshimiwa Spika, niombe kuishauri habari ya *definition* ya *contracts* Mheshimiwa Waziri ameeleza hapa kwamba moja ya faida ya Muswada ni kwamba ni sheria rahisi. Sheria rahisi mbona *definition* ya *contract* haipo, hiyo rahisi inatoka wapi?

Mheshimiwa Spika, huyo mfanyakazi anayetoka kule Singida hajui Kiingereza hajui hajui Kiswahili vizuri, na nini atajuaje hiyo rahisi. Kwa hiyo, niombe sana kwamba kwa kweli *definition* ili mfanyakazi ajue wajibu wake ni nini, haki zake ni zipi, ajira yake ipo namna gani na kadhalika. Hiyo ni muhimu sana. *ILO conversion* ndivyo kinavyosema. Sasa tunaziridhia kwa kila siku halafu tunakwenda ku-*control* na haya maana yake nini?

Katika ukurasa wa 78 *Section ya 31* mfanyakazi anayezuiwa na mwajiri wake kwenda likizo wako wengi hasa wakubwa, ananyimwa hapa haki ya kupewa pesa *in lieu* kwa nini?

Wewe mwenyewe umemzuia halafu sheria inamkataza kwamba huyu amezuiwa miaka mitatu, miaka nenda rudi na hutaki kumruhusu. Mpe haki yake na fedha yake aende kwa nini mnanyima? Na sheria sasa imekubali kwamba mtu anaweza kulipwa *cash in lieu* badala ya siku zake zile za likizo.

Pale kwenye uwakilishi kwenye matawi, mwanamke hata pale anapofanya Ofisi ina watu kumi, walau mwanamke mmoja awepo, au pale ambapo sijui kuna watu 15

walau mwanamke mmoja awepo isiwe tu huku mwishoni ambapo mmetaja kuwa kama kuna wafanyakazi 15 mnasema haa! Basi angalau wanawake watano, tokea mwanzo pale kama tawi lina watu watatu basi walau mmoja awe mwanamke. Mimi ndiyo ushauri wangu mimi. *(Makofi)*

Halafu *page 66, clause 6(iii)* naomba ibaki vile vile kama ilivyokuwa mwanzoni. Marekebisho yaliyoletwa yameondoa na imeweka kitu *without resoanable grounds* iondoke. Hapa ndiyo unampa ridhaa mwajiri acheze na sheria. Ni Mtanzania gani ambaye utamwambia nieleze kwa nini leo umechelewa kuja Bungeni. Mheshimiwa Spika akakosa kukuambia.

Mheshimiwa Spika, nitakupa sababu nimechelewa mtoto alikuwa anaumwa, mama yake alikuwa hayupo na mimi nilikuwa nalea na kadhalika. Kwa hiyo, ukimwachia mtu nafasi aeleze kwa nini utapata tu, popote pale. Mtanzania ni fundi sana wa kujieleza. Kwa hiyo, naomba na hili nalo liondolewe.

Halafu kuna *page 82* kwamba mwanamke ambaye alikuwa amechukua *maternity leave* anaweza akawa *terminated* baada ya likizo kumalizika. Hapa nataka maelezo kwa nini. Amechukua *maternity leave* amemaliza vizuri, amerudi kazini lakini kuna kifungu hapa kwenye *page 6(a)4* ambacho kinaweza kumfanya mwanamke huyo asiajiriwe tena kwa kuwa tu alikuwa katika *maternity leave* ningeomba hilo nalo liweze kuangaliwa. *Definition hazards work* ni vizuri itafsiriwe tusimwachie kila mtu.

Ndugu yangu alijaribu kueleza pale, kazi ziko inategemea ameajiriwa kazi gani, sasa *hazards work* bila kuwa na tafsiri yake hapa na tukamwachia kila mwajiri akatafsiri vyake yeye anavyoona huyu mama mja mzito kazi gani ambayo ni nzito ni mbaya kwake nadhani inaweza ikaleta matatizo. Basi kama haitafsiriwi kwenye sheria yenyewe Mheshimiwa Waziri kwa mujibu wa utaratibu ambao ameutoa kwa njia ya *regulation* aweke kwenye kanuni zake za kazi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono na nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge , tutaendelea mchana kwa sababu wakati tunaendelea kuna maombi zaidi yalipokelewa tumebaki na wasemaji hadi sasa watano ambao watapata nafasi mchana. Niwaarifu Waheshimiwa Wabunge kuna wasomaji Watanzania waliopo nje ya nchi ambao wameanza kutumia tovuti yetu wanaitembelea wanaona yaliyomo.

Sasa kuna Mtanzania mmoja yuko Chuo Kikuu cha Dilamogan Uingereza, amegundua kwamba baadhi ya sifa za Waheshimiwa Wabunge tulizoziweka mle siyo sahihi. Kuna wengine wameshajiongezea sifa za elimu hazikuonekana mle. Kuna wengine hawaonekani kabisa.

Kwa hiyo tutazi-*down* zote halafu niwaombe Waheshimiwa Wabunge mtusaidie kuzi-*up date* ziwe sahihi kabisa ili kusudi maelezo ya Mbunge yasionekane yana hitilafu kwa Watanzania. Huyu ni Mtanzania amegundua ametaja na majina kama

Mheshimiwa Monica Mbega, Mheshimiwa Juma Kapuya na ana mashaka na Mheshimiwa Diodorus Kamala, ana mashaka kwamba sifa zilizoko kwenye tovuti yetu hazifanani na hali halisi ya sifa walizo nazo.

Kwa hiyo tutafanya hivyo, tutaomba ushirikiano ili tuwe na taarifa sahihi kwenye *web site* yetu ya Bunge. Baada ya hapo sasa tumefikia muda wa kupumzisha Bunge kwa kipindi cha chakula cha mchana. Hivyo nasitisha shughuli za Bunge hadi saa 11.00 jioni.

*(Saa 06.55 Mchana Bunge lilifungwa Mpaka Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge lilirudia)*

*Hapa Naibu Spika (Mhe. Juma J. Akukweti) Alikalia Kiti*

**MHE. HENRY D. SHEKIFFU:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda kukushukuru na napenda nitoe hongera nyingi kwa wale wenzetu ambao wamepata nyadhifa, Mama Mongella na Ndugu yetu Ntagazwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru Waziri wa Kazi na Maendeleo ya Vijana kwa kuleta Muswada huu ambao kwa kweli kwa imani yangu ni kwamba umechelewa. Ulipaswa kuja kipindi kirefu kilichopita lakini niseme kwamba umekuja pia wakati mzuri kwa sababu mambo mengi yamejitokeza hapa katikati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kwa yale mambo ambayo ninayaona na ambayo yapo katika nyanja ya kazi. Ukiangalia Muswada huu ni Muswada mzuri sana lakini yaliyoandikwa ndani ya Muswada, kuandika Muswada na kutekeleza Muswada ni mambo mawili tofauti. Ninaanza kwa kusema hivi kwa sababu iko Miswada mingi mizuri tu kama huu ulivyo na Miswada ambayo kwa kweli imepata mawazo ya wananchi kama huu ulivyo lakini utekelezaji wake unakuja kuleta matatizo au hautekelezwi kabisa au hautekelezeki.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa swali ambalo baada ya kumpongeza Waziri kwa kuleta Muswada huu na nakiri tangu mwanzo kwamba naunga mkono hoja hii asilimia mia moja, katika ukurasa wa 57 kuna suala linalohusu *discrimination* na katika Aya hiyo Kifungu cha 6 imeelezwa mambo gani ambayo hayatahusika kama *discrimination.* Moja lililotajwa katika Kifungu cha (c) linasema: *"To employ citizens in accordance with a National Employment Promotion Services Act 1999"*.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 1999 mimi nilikuwa Mbunge ilitungwa sheria hii ambayo nimeitaja kwa shangwe na kupigiwa makofi makubwa lakini pengine Waziri wakati wa kujibu angeeleza tumefikia hatua gani katika utekelezaji wa sheria hii? Nauliza hili kwa sababu Wabunge wengi wamelalamika sana kuhusu uhaba wa ajira na watu ambao hawapaswi kuajiriwa katika nchi hii. Ninaamini uko uhusiano kati ya Idara ya Uhamiaji na Wizara ya Kazi na Maendeleo ya Vijana mtu haruhusiwi kuingia katika nchi

hii na kufanya kazi bila hizi Wizara mbili kukaa na kushauriana. Hivi hawa wanaofanya biashara ambazo Watanzania wana uwezo nazo wanapata vibali vya kufanyia kazi wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi nilinunua maua pale Kariakoo kwenye duka la Mchina hakunijua mimi ni nani lakini yeye ndiye aliye na duka naamini hivyo kwa sababu anapanga bei, anaagiza hili na lile hivi hawa wanapata wapi vibali vya kuishi katika nchi hii wafanye biashara ambazo Watanzania wana uwezo nazo?

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria ile ya mwaka 1999 ilikuwa inatoa maelekezo kuitaka Wizara ya Kazi na Maendeleo ya Vijana isimamie ajira zile ambazo hazipaswi kuwa za wageni lakini inaelekea kwa kweli hakuna linalofanyika. Kazi nyingi ambazo zinapaswa kushikwa na Watanzania na ambazo tuna uwezo nazo bado zinaendelea kuchukuliwa na watu wengine na watu hao sio raia.

Mheshimiwa Spika, leo hii sio rahisi kwa mimi kwenda kuanzisha duka Dubai, sio rahisi kwa mimi kwenda kuanzisha duka London, watu wetu kule wanafukuzwa sisi wenzetu tunawakumbatia, hivi tunashindwa hata kuuza rejareja? Basi kwa nini hao wafanyabiashara wa nje wasilete vitu vyao mpaka hapo Bandarini wakawauzia Watanzania na wakachukua jukumu la kuuza katika soko la Tanzania na watu wetu wakapata ajira? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, madhumuni ya sheria hii yameelezwa katika ukurasa wa 52, Kifungu cha 3, *Object: "To promote economic development through economic efficiency, productivity and social justice"*. Hatutawatendea wananchi wetu haki wala lengo hili halitafikiwa kama hatutawatetea.

Mheshimiwa Naibu Spika, siku zote Sheria za Kazi watu wetu bado wanahitaji elimu hata hii tuliyoitunga wanahitaji elimu ni kwa kiasi gani elimu inatolewa ili watu hawa wajue haki zao? Hili ni suala ambalo ni lazima liangaliwe na Serikali na liwekewe mikakati kuhakikisha kwamba kwa kweli linatekelezwa. Kwa hiyo, katika kifungu hiki cha kutekeleza haki, ninaomba sana elimu itolewe ili wananchi wajue haki zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo ningelizungumzia liko katika eneo hilo hilo la discrimination bado ziko tabaka za wananchi katika ajira katika nchi hii na mimi sijui kama Waziri anajua au hajui lakini naamini Waziri anajua. Wako watu wameajiriwa miaka miwili, mitatu anapewa mshahara wa kutwa, hivi inawezekanaje? Naamini sheria inamtaka mwajiri inapofika mtu ameajiriwa kwa zaidi ya miezi mitatu au sita apewe ajira ya kudumu lakini kuna watu wameajiriwa zaidi ya miaka miwili, mitatu anaajiriwa miezi mitatu ikifika anaachishwa siku mbili halafu anakuja tena anaajiriwa kwa ulaghai ili asipate haki zake muhimu za kustaafu baada ya kuacha kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naamini malengo ya sheria ni kuyajibu hayo lakini nazidi kurudia tena ni kiasi gani tunazisimamia sheria hizi ili zitekeleze malengo yake, hilo ndio la msingi. Kwa sababu kutunga sheria bila kuisimamia malengo yake, ukweli uliopo haitasaidia kama hii ya mwaka 1999 ambayo ilikuwa na nia ya kuwasaidia na maeneo ambayo wananchi wameambiwa wawekeze huko na hizi kazi zimetengwa kwa

Watanzania yalitajwa lakini mpaka leo unakuta Mataifa mengine yanafanya kazi ambazo tuna uwezo wa kuzifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo mimi ningeomba na hili kwa kweli itafika mahali kama halitatolewa maamuzi, aah, kwa kutumia Bunge hili, mimi nitaomba kuleta Hoja Binafsi ufanywe uchunguzi kati ya Idara hii ya Uhamiaji na *Labour,* vibali vya watu kukaa hapa nchini kufanya kazi vinatolewaje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hilo kama halitabadilika tutaendelea kuona watu wanafanya kazi ambazo Watanzania wana uwezo, mimi nitaliomba Bunge kwa kweli tukachunguze ni nani anatoa vibali hivi, ni nani anayesimamia kwa sababu najua Wizara ya Mambo ya Ndani haiwezi kutoa kibali bila kwanza kupitia Wizara ya Kazi ili ionekane kwamba kweli huyu anayetaka kuajiriwa hiyo nafasi yake hakuna Mtanzania wa kuijaza, sasa inawezekanaje? Mimi naamini liko jambo hapa na hili jambo la rushwa tusilidharau lipo na tunaomba viongozi mliangalie wenzetu lawama tunazotoa sio za uongo zipo maana mimi nina ushahidi kama ninavyokuambia juzi nimenunua ua kwenye duka la Mchina huyu Mchina kapata wapi kibali cha kukaa hapa nchini na kufanya kazi ukitaka nitakupeleka ukaone.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo nilitaka nizungumze kidogo tu ni katika suala la vikundi hasa suala linalohusu vikundi maalum kama ajira kwa watoto. Ajira kwa watoto ni tatizo kubwa na katika sheria hii imeandikwa kwamba itabidi mtu aliye na miaka 14 asiajiriwe mahali popote kama nimeelewa vizuri kama sikuelewa vizuri basi Waziri atakuja kunisaidia. Lakini vijana wetu wanaofanya kazi majumbani wanafanya kazi wakiwa chini ya umri wa miaka 14, hivi litaweza kutekelezeka hili? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru katika wale ambao wameambiwa wafanye kazi wakiwa na miaka 18 lakini kuna vipingamizi ambavyo vinaeleza kwamba wasifanye kazi aina fulani. Nafikiri na hili ili liweze kutekelezeka ni vizuri pengine tukaangalia ni kazi gani ambazo mtoto chini ya miaka 14 asiajiriwe pengine zingetajwa. Kwa sababu tutaji-*contradict* sisi wenyewe viongozi hapa leo umetunga sheria usiajiri mtoto chini ya miaka 14 lakini ukienda nyumbani huyo ndio mfanyakazi wako wa ndani, kwa hiyo kwa kweli unavunja sheria. Sasa naomba ufafanuzi katika hili limeangaliwa kwa misingi ipi ili kwa kweli lisituchanganye.

Mheshimiwa Naibu Spika, pengine nizungumzie wasiwasi wangu nilionao katika mabadiliko ya mawazo ya Watanzania hasa katika soko la utandawazi wa kazi. Hivi leo tunaingia katika Jumuiya ya Afrika Mashariki, nchi za *SADC* na ni kweli kwamba sasa soko la ajira litakuwa wazi, watu wetu wamejiandaa kiasi gani kuondokana na mawazo ya ukiritimba wa huko nyuma ili waingie katika soko la ajira kwa mashindano yanayokubalika?

Hili ni suala ambalo lazima tuliangalie kwa sababu kama hatutaliangalia kwa uangalifu tutaajiri watu wengi kutoka nchi za nje hasa majirani zetu katika Jumuiya ya

Afrika Mashariki au *SADC* matokeo yake watu wetu watakosa ajira sasa hili katika sheria hii linaangaliwa kwa msingi gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho kabisa, sheria hii haitamki wazi wazi pengo la ajira linalokua siku hadi siku na inatamkwa tu suala la taratibu za ajira lakini ni vipi tutapunguza pengo la ajira la vijana wetu? Kwa mfano hii bomoabomao inayoendelea ni eneo moja ambalo linaondoa ajira sana kwa vijana hivi Serikali haiwezi ikaliwaza hili pamoja na madhumuni yake mazuri kiasi iwezekanavyo lakini unapokosesha vijana ajira kwa maelfu unajenga jeshi ambalo ni la hatari sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vizuri pawepo na mawasiliano kati ya Wizara na Wizara. Wizara ya Ujenzi inavunja nyumba barabarani, Wizara ya Kazi inatafuta kazi kwa vijana wake sasa kwa nini kusiwe na mawasiliano maana pengine watu wangepewa muda wa kutosha kujiandaa hiyo busara ingetumika ingesaidia sana kuliko mnatoa miezi mitatu unawakosesha watu 1000, 2000 hawana ajira wako barabarani na huna njia ya kuwarudisha makwao unaleta janga kubwa sana katika nchi. Ni vizuri sheria zinapotungwa Wizara mkae na taratibu zinapowekwa Wizara zikae kwa pamoja tuwe na mawasiliano ili tujue athari za kila sheria tunapoitunga.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kusema sijafurahishwa sana na sheria ile inayovunja nyumba za watu barabarani pamoja na kwamba niko katika Kamati ya Miundombinu lakini sifurahishwi na tendo lile kwa sababu linakiuka haki za binadamu na linatujengea wimbi baya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, haiwezekani mtu kajenga nyumba yake miaka 25 iliyopita wewe ulikuwepo badala ya kumwambia kwamba bwana usijenge leo unakwenda unaivunja unasema ulijenga ndio umenichokoza kwa msingi upi wewe ulikuwa wapi hukumwambia? Sasa mambo haya ni mazito lakini lazima tuyataje tusiyoyatamka kama Wabunge tutajikuta kwenye matatizo na ni vizuri tuangalie athari zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hivyo, namalizia kwa uchungu sana kwamba hili jeshi tunalolifukuza barabarani hili kwa kuwavunjia nyumba zao litatuletea matatizo, Waziri wa Kazi tusaidie watu hawa wapate kazi tunajenga jeshi litakaloleta janga. Sheria hii ya kuvunja nyumba barabarani ichunguzwe na ikiwezekana ibadilishwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. CHRISTOPHER S. WEGGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi nami nichangie. Ni kweli nimeingia sasa hivi lakini haina tatizo. *(Kicheko)*

**NAIBU SPIKA:** Lakini nilishasoma jina lako kabla haujaingia nilidhani jirani zako wamekuambia, endelea.

**MHE. CHRISTOPHER S. WEGGA:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Spika, kubwa la ajira ni kwamba siku zote tumesema kazi zipo za aina mbili ya kilimo na kazi

za kuajiriwa, tunayoizungumzia ni kazi ya kuajiriwa. Kwa *message* tu ya kawaida hii kazi ya kilimo haitambuliki. Lakini hawa wanaoajiriwa wanapotaka kujitetea pale wanapoonewa Watumishi Wakuu wanasema: "Kama umeona mshahara mdogo basi kalime". Sasa hilo si jambo zuri sana kama hutaki kufanya kazi yangu na mshahara mdogo nenda kalime inaonyesha wazi kwamba kazi ya kulima ndio haina haki ya kudai na vile vile yule anayedai anakatishwa tamaa na maneno haya hawatumii watu hawa wageni, wanatumia hata kwenye Mashirika ya Umma na Serikalini, wanamkatisha tamaa kabisa mtu kwamba wewe kama hutaki basi kalime. Sasa sijui wanakuwa na msingi gani kwamba kulima sio kazi nzuri au kulima ndio haina madai kabisa? Nilitaka niseme hilo kwamba si jambo zuri kabla ya mambo mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kubwa ni ajira juu ya mashirika tunayobinafsisha. Kuna ajira tatu pale ajira ya kwanza ndio hii wanaizungumza wenzangu kwamba wawekezaji wanapokuja wanakuja na ma-*expert* wao wale wana mshahara wa nje huko huko hapa wanapewa posho na chakula na wakati mwingine wanakuwa na kantini yao wanapata chakula bila hata mshahara lakini mishahara yao kule inaanzia milioni nane, milioni kumi.

Sasa nataka nipate tu ufafanuzi kwamba hivi hapa Serikali haikosi mapato yanayotokana na kodi kwa sababu hawa mishahara wanachukulia nje huyu Mtanzania anayechukulia mshahara hapa hata kama anapata laki nane analipa kodi wanapataje kodi yao huyu anayelipiwa huko nje?

Mheshimiwa Naibu Spika, pili kwenye mashirika haya tuliyobinafsisha watu wanafanya kazi kama kibarua kwa muda mrefu yaani sasa mtindo uliokuja ni kwamba wao hawataki tena permanent yaani yule anayefanya kazi kwa mwezi hawana habari naye wanaogopa ajira ambayo itamtaka atoe tiba, makazi na huduma nyingine wanasema hapana sisi tunachotaka sasa wewe tunataka kazi za kila siku za kutwa ndio wengi wako hapo.

Sasa tunaiomba Wizara isaidie kutembelea viwanda hivi ili kuwe na amani sasa hivi hata Wabunge tukifika kwenye viwanda hivi ambavyo tumebinafsisha kubwa tunalolikuta ni kwamba watumishi wetu hawathaminiwi, Watanzania hawa hawathaminiwi kabisa. Kwa hiyo, tunaomba ile mikataba ithaminiwe na Wizara nayo hawa Makamishna watembelee mpaka kwenye viwanda pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, Watumishi wa Mashirika ya Umma na Watumishi wa Serikali tunafahamu ni Idara mbili tofauti Mashirika ya Umma ni kutokana na faida mliyoifanya, mtafanya kazi kutokana na uzalishaji lakini kwenye marupurupu mngetizama kwamba hivi kama tatizo sio wafanyakazi tatizo kwa mfano Shirika la Umma *TANESCO* mwaka huu tatizo ni maji, Bwawa la Mtera halikujaa hivi pale utasema mwaka huu uzalishaji mbaya hampati mafao yenu wao wangekwenda kule wakatengeneze mvua juu? *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ndio kinachozungumzwa kwamba bwana mwaka huu bahati mbaya sana Bwawa la Mtera halikujaa maji, mkataba ilikuwa tuwape mafao lakini

sasa bwawa halikujaa maji na Wizara inakubali kabisa watu wakienda pale katika Chama chao cha Wafanyakazi *TUICO* wanasema hapana, kama kweli maji hayakujaa basi hakuna mafao hapa. Sasa hayo, ningeomba Wizara itazame kwamba jamani kama mkataba ulisema ukifikia miaka mitatu na bahati mbaya mwaka huu mvua haikunyesha ungeongezwa mshahara kutoka 80,000 - 100,000 basi apewe 100,000 hili bwawa la mvua lingoje mvua ikinyesha maji yatajaa. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hilo Mheshimiwa Waziri tunakuomba sana ndivyo wanavyoonewa watu wetu maeneo kama hayo machache tu. Sasa mtu huyu anarudi ananung'unika na lingine ndio hilo wanasema kama unaona mvua haikunyesha basi acha kazi kalime, mvua yeye hatengenezi mvua, huo ni ujeuri. Tunataka wafaidi uwekezaji, Mashirika ya Umma na Serikali wasipishane sana watu hawa. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wenzangu wamezungumzia sana suala la kuumwa. Sasa hivi umekuwa ni mtindo hasa kwenye mashirika haya ya watu binafsi kukiuka sheria, sheria inasema kabisa kuna vifaa vya kupewa kutokana na maeneo unayofanyia kazi kama ni ya hatari.

Mheshimiwa Spika, tumetembelea kiwanda kimoja juzi sitaki kukisema tunamwuliza bwana hizi *gloves* za hawa watu ziko wapi? Anasema sisi tunawapa lakini wenyewe hawataki kuvaa. Sasa tunauliza Wizara huwa mnatembelea sehemu kama zile mbona wenzenu tukitembea tunakuta watu wana matatizo tuache tabia ya kupata majibu tukiwa maofisini tutembee kuangalia watu wetu. Tulisikitika sana siku hiyo watu wana hali mbaya dakika kumi tulizotumia pale, *oxygen* tuliyoivuta pale ni *carbon oxygen...(Kicheko)*

**MBUNGE FULANI:** *Carbon dioxide*. *(Kicheko)*

**MHE. CHRISTOPHER S. WEGGA:** *Carbon dioxide,* samahani. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli ujumbe umefika lakini hali ya hewa ya pale ilikuwa mbaya sana. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya hali hiyo sio pale hata sehemu za machimbo. Kwenye machimbo utakuta watu wapo tu hawana vifaa vyovyote, kila mahali tulipokwenda. Kwa hiyo, hili suala la vitendea kazi, tusaidieni sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli wafanyakazi sasa hivi mishahara ni mizuri lakini nataka nizungumzie suala la viwango. Sasa hivi ni Sh.44,000 kwa Mashirika ya Umma na kwa mashirika ambayo tumebinafsisha lakini kiwango hiki kwa sasa ni kidogo sana Sh.44,000 anapotaka kuitumia mtu yeyote yule ni ndogo sana.

Mheshimiwa Spika, sasa wawekezaji kikubwa walichosimamia ni kwamba huu mshahara umetoka Serikalini na wewe Mbunge unayekuja kutetea sisi hatukuelewi, ndio mshahara wenu. Sasa kumetokea hali halisi kwamba sisi hatutetei sasa tulikuwa tunataka angalau kima cha chini kifikie Sh.100,000 hata ukiweka 150,000 kutokana na hali ilivyo

kama huyo anayesema hapati faida basi afunge hicho kiwanda lakini kumwambia mtu mshahara ni Sh.44,000/= ndio kima cha chini cha Serikali ukampangia matumizi tu hata kama ana watoto tu wa kusomesha hawezi kufanya hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tuende upande wa pili wa shilingi ni wale watumishi wetu wenyewe wale wa ndani bado ni Sh.5,000/=. Nikushukuru sana Mheshimiwa Naibu Spika kama wa kwako amefika Sh.40,000/=, watumishi wa ndani kuanzia sisi hapa Bungeni, watumishi wa ndani mahali popote pale wana mishahara midogo sana tunawasaidiaje hawa?

Mheshimiwa Naibu Spika, wenzangu wamezungumzia sana umri, kwamba wenye umri mdogo wasiajiriwe. Wasiajiriwe wakiwa na umri mdogo sawa, lakini kibaya zaidi ni mshahara kwa watu binafsi hasa wafanyakazi hawa wa ndani, hata kama haiwezekani basi hawa wangekwenda mpaka Sh.30,000 watu wanalipwa 5,000/= na 10,000/= hali hiyo kwa kweli inamfanya, kwa hali hii tunayoisema ataepukana na maradhi kama ni wasichana watafanya kazi ya ngono tu hasa kwenye mabaa. Wale hawako pale kwa ajili ya mshahara, inashindikana mshahara mdogo baadaye mtu anafanya vitendo viovu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia, ahsanteni kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

**MHE. TEDDY L. KASELLA-BANTU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi nami nichangie Muswada ulio hapa mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda kuwapongeza Mheshimiwa Balozi Getrude Mongella kwa kuwa Rais wa Bunge la Afrika. Pili, nampongeza Mheshimiwa Waziri Arcado Ntagazwa kwa kuwa Rais wa Umoja wa Kimataifa katika mambo ya Mazingira, hongera sana. Vile vile, nafurahi kwamba Bunge letu Tukufu limetoa *Speakers* wa Mabunge haya ambayo ni jinsia vile vile kwamba tuna mwanamke anayeweza na tuna mwanaume anayeweza kwa hiyo duniani tunaonekana kwamba sisi tunajali jinsia, ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niingie katika Muswada wenyewe. Kiutaratibu nampongeza kaka yangu Profesa Kapuya kwa utaratibu wake aliofanya kwa ajili ya kuwaweka wadau wote kukaa pamoja katika semina ile iliyofanyika Morogoro na juzi katika *public hearing*. Kwa kweli hii imesaidia sana kuwaweka waajiri na waajiriwa, vyama vyao vya TUGHE na Vyama vingine pamoja na...

*(Hapa mic ilipiga kelele)*

**NAIBU SPIKA:** Endelea!

**MHE. TEDDY L. KASELLA-BANTU:** Naomba dakika zangu ziongezwe kidogo. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na hivyo vikao tulivyokaa pamoja imetusaidia sana kupunguza mambo mengi kwa sababu kulikuwa na watu wanaowakilisha vyama vya waajiri na kulikuwa na watu wanaowakilisha vyama vya wafanyakazi. Kwa hiyo, utaratibu huu ni mzuri umetusaidia kupunguza matatizo mengi ambayo yalikuwepo. Sasa hivi naona kuna mapungufu machache ambayo naomba niyazungumzie.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapungufu ninayotaka niyazungumzie ni kwanza katika masuala ya matibabu. Wafanyakazi wetu ambao ni Watanzania wamezoea kuwa katika mfumo wa Mashirika ya Umma na Serikali ambapo walikuwa wanapata matibabu bure. Unapowaingiza sasa hivi katika *cost sharing* ni lazima twende nao taratibu ili tuweze kupata *production* inayofaa.

Kwa misingi hiyo basi, naomba makampuni au waajiri waweke kipengele hiki cha matibabu ili wafanyakazi wawe na uhakika na afya zao na vilevile mwajiri awe na uhakika na afya za wafanyakazi wake. Kwa kuwa kama mfanyakazi ana uhakika wa afya yake yeye pamoja na familia yake ambao ni kama watoto wanne ambalo nalo ni jambo geni sana kwa Watanzania, tumezoea kuzaa watoto wengi, sasa tunaweka *limit* ya *population* ya watoto wanne.

Kwa hiyo, hilo nalo ni tatizo lakini *at least* mwajiri aweze kutoa matibabu kama ilivyokuwa zamani na kama ni kuchangia basi wafanyakazi wachangie kidogo sana katika Bima ya Afya ili wanapougua waweze kwenda kutibiwa katika hospitali zilizopangwa na mwajiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfanyakazi akiwa anajua kwamba saa yoyote akiugua anakwenda, anapata matibabu, atafanya kazi kama punda, lakini akiwaza kwamba nikiugua au nikiuguza sina pa kupeleka mtoto wangu kutibiwa na wakati mwingine magonjwa yanakuja hana hata senti tano mfukoni mwake hawezi kufanya kazi vizuri. Kwa hiyo, hilo ni tatizo kubwa na katika kupunguza kero za wafanyakazi ili wawe na amani na wawe na afya bora, naomba haya matibabu yaongezwe ili yaweze kumfanya mfanyakazi aweze kufanya kazi kwa uhakika na amani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna wafanyakazi ambao ni wasichana wadogo au ni kina mama vijana ambao na wenyewe wanajifungua wakiwa katika umri huo wakiwa ni wafanyakazi na vile vile wanakuwa na haki ya kuruhusiwa na mwajiri kwenda kunyonyesha watoto wao, wanapewa muda huo. Lakini utakuta mfanyakazi anatoka kwa mfano Kimara, Temeke, Tandika au Salasala, anakuja kufanya kazi Mjini, *City Centre,* sasa unakuta hawezi kurudi nyumbani kuanza kunyonyesha mtoto wake na mtoto huyu ana haki yake ya kunyonya maziwa ya mama yake ambayo ni lishe bora.

Kwa hiyo, nilikuwa nashauri wafanyakazi wapewe angalau chumba kimoja au viwili pale kazini ili watoto hawa wawekwe pale kama *nursery school* au *clinic* ili mama huyu aweze kutoa pendo la kunyonyesha mtoto wake wakati akifanya kazi na hiyo ni haki ya mtoto kunyonya maziwa ya mama yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niende kwenye kifungu namba 40(3) kuhusu sababu za kufukuzwa kama ukiwa mlemavu. Waswahili wanasema hujafa hujaumbika, kuna wengine wanaozaliwa walemavu na kuna wengine wanakuwa walemavu kutokana na matukio yanavyokuwa katikati hapa kwa mfano, anaweza kupata ajali au kama hivi kuna *stroke* na vitu kama hivi. Kwa hiyo, mwajiri asifukuze walemavu kwa sababu ya ulemavu.

Kwa hiyo, naomba hicho kipengele kiongezwe ili walemavu nao wasifukuzwe kwa sababu ya hali halisi iliyowapata wakati huo na siyo kwa sababu zao wenyewe, ni kwa sababu Mwenyezi Mungu amefanya hivyo na kweli methali hii husema hujafa hujaumbika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunatengeneza hizi sheria kwa kuwatayarishia watoto wetu, vilembwe vyetu na wajukuu wetu na sheria huwa inachukua miaka mingi sana mpaka ibadilike. Kwa hiyo, lazima tuwe waangalifu sana, tusitazame sasa hivi, tutazame mbele watoto wetu na vijukuu vyetu vitakuwa namna gani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye masuala ya kufukuzwa ambayo yanaweza kuwa mengi sana kutokana na Watanzania wenyewe tumezoea kufanya kazi chache kwa watu wengi. Kwa mfano, sasa hivi kazi moja inaweza kuwa ya kufanya watu kama kumi, anapewa mtu mmoja. Hili ni tatizo kwa sababu hatujazoea stahili hiyo.

Kwa hiyo, mimi naomba kama itatokea mtu anafukuzwa pengine kwa sababu ya stahili yenyewe ambayo hatujaizoea na pengine kwa sababu ya rushwa au wizi ambao amefanyiwa kama majungu au fitina na akipelekwa Mahakamani anashinda basi iwe *automatically* anarudi kazini, siyo afukuzwe tena kwa sababu atakuwa amepewa adhabu mbili hapa. Alikuwa anapewa nusu mshahara wakati kesi ipo Mahakamani, inapokwisha kama ameshinda basi arudishwe *automatically* kama vile anavyokuja kufukuzwa kama ameshindwa kesi ambapo ni *automatically* anafukuzwa.

Kwa hiyo, vitu hivi viwe pande zote mbili, akishinda arudishwe kazini na akishindwa afukuzwe *automatically.*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie kifungu namba 15(b) kuhusu *recruitment* na naomba iongezwe *domicile,* yaani anapoajiriwa mtu, kwa mfano, kazi nyingi zinatokea Dar es Salaam na watoto wetu wanaomaliza *University* na vyuo wengi wanakimbilia Dar es Salaam kwa ajili ya kutafuta kazi kwa sababu wanaamini kazi zipo nyingi sana huko Dar es Salaam.

Sasa anapokwenda kuomba kazi haandiki anuani kwa mfano ya Nzega, Tabora, Shinyanga, Kigoma au Arusha kwa sababu akiandika anuani ya Kigoma, barua mpaka ifike Kigoma, aitwe kwenye *interview,* atakuta *interview* imeshakwisha, kwa hiyo, anaandika ya Dar es Salaam. Lakini anapoajiriwa, huyu mtu si mtu wa Dar es Salaam pengine pale anakaa kwa rafiki au ndugu ambaye vile vile katika kusaidiana, maisha yanavyokuwa magumu *the extended family* zinaanza kupungua.

Kwa hiyo, huyu anatakiwa aangaliwe alipotoka ili wakati anapokwenda likizo apewe nauli yake mpaka huko alipozaliwa au wazazi wake walipo. Vile vile hii inasaidia wakati anapofukuzwa au anapoacha kazi maslahi yake yaani *final payment* yake kuwa nzito kidogo kuliko akichukuliwa kama ni mtu wa Dar es Salaam na maziko na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niongezee machache ya haraka haraka lakini mengine nitayawasilisha kwa maandishi. Kwa haraka haraka ukitazama kifungu namba 20(b) na Kifungu kidogo (a) kuhusu *maternity leave. Maternity leave* imeandikwa miezi miwili. Lakini miezi miwili hii kuna wengine wanakuwa na matatizo sana wakati wa ujauzito anaweza kuanza *leave* yake akiwa na miezi nane, *by the time* anakuja kujifungua atakuwa amebakiza mwezi mmoja, kwa hiyo, hii haimsaidii mama na mtoto kupumzika na mama kulea mtoto wake vizuri na kuonyesha upendo na lishe bora ya maziwa ya mama.

Kwa hiyo, kwa misingi hiyo naomba iongezwe *maternity leave* yake ianze tarehe ambayo amejifungua, ndiyo ihesabike miezi miwili ili imsaidie mama akae *maternity leave* kwa muda wa miezi miwili *exactly* na vile vile aweze kulea mtoto wake kwa miezi miwili *exactly* kabla hajaanza kumwacha na mayaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie vile vile kifungu kingine kinachohusu *leave* ya ugonjwa *(sick leave).* Katika Sheria hii imeonekana kwamba ziwe siku 120. Mimi naomba ziwe 180 yaani badala ya siku 63 ziwe siku 90 na badala ya siku 63 zinazofuata ambazo unapewa *half daily pay* iwe siku 90 pia, kwa misingi hiyo atakuwa na siku 180.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu bado nina nafasi naomba niongezee kitu kingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie kuhusu *section number 50(a),* hapa kuna mfanyakazi anaposhtaki anatakiwa kutoa *filing fees.* Sasa unavyojua Watanzania wenzetu, wafanyakazi na sisi wenyewe tunajua hali halisi, pesa imekuwa ngumu sana, maisha yamekuwa magumu na wote ni walala hoi, kwa hiyo, unapomwambia mtu aende kufungua kesi halafu alipe *filing fee* ni kama unampa adhabu tena.

Kwa hiyo, naomba basi hii ya *filing fee* iondolewe ili mfanyakazi apate haki ya kushtaki kupata haki yake vilivyo kisheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. HADIJA K. KUSAGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia kidogo katika Muswada huu.

Kwanza na mimi naomba nichukue nafasi hii niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu waliotangulia katika kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge

waliochaguliwa kuwa Marais. Kwanza nimpongeze kwa dhati kabisa Mheshimiwa Mama Getrude Mongella, ambaye amekuwa Rais wa Bunge la Afrika, Mheshimiwa Arcado Ntagazwa naye pia nampongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tunaye Rais wa Chama cha Walimu, dada yangu Mama Margareth Sitta na yeye pia kwa vile nachangia Muswada huu yupo, basi nichukue nafasi hii kumpongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze basi kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, kaka yangu Mheshimiwa Profesa Juma Kapuya, Naibu Waziri, Mheshimiwa Mudhihir Mudhihir, pamoja na watendaji wote wa Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo kwa kuleta Muswada huu. Labda mimi niseme kwamba Muswada huu umekuja muda muafaka, muda ambao kiu ya wafanyakazi ni kubwa sana kwa maana sasa hivi ni kipindi ambacho ni cha ubinafsishaji wa Mashirika mengi tu, kwa hiyo, kumekuwa na migogoro mingi baina ya wafanyakazi na waajiri kutokana na huu ubinafsishaji. Sasa ndiyo maana nimesema kwamba Muswada huu umekuja muda muafaka, muda ambao wafanyakazi na waajiri wapo kwenye matatizo haya ya ubinafsishaji. Kwa hiyo, kuleta Muswada huu kutasaidia kwa kiasi kikubwa kuweza kupunguza migogoro baina ya wafanyakazi na waajiri kwani kila mmoja atakuwa analindwa na sheria ambayo tutaipitisha leo.

Kwa hiyo, nichukue nafasi hii kabla sijaendelea niseme kwamba na mimi naungana na wenzangu kuunga mkono Muswada huu kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuupitisha Muswada huu ama kuunga mkono Muswada huu, lakini yapo matatizo makubwa sana kwa watumiaji wa sheria hii ambayo leo hii tutaipitisha.

Mimi kabla sijawa Mbunge huwa nazungumza mara kwa mara, nimetokea kwenye Vyama vya Wafanyakazi na nichukue nafasi hii kuwapongeza sana kwani inawezekana kabisa ndiyo walioniandaa niweze kusimama vizuri na hasa katika kuomba nafasi ya Ubunge Jimboni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo matatizo makubwa ya utumiaji wa hizi sheria kuanzia huko nyuma kuna matatizo kati ya wafanyakazi wenyewe, yapo matatizo baina ya viongozi wa wafanyakazi, lakini yapo matatizo pia kwa upande wa waajiri. Wizara yetu inafanya utaratibu mzuri kabisa wa kuweza kuziandaa sheria mbalimbali lakini ni vipi walengwa hawa watatu wataweza kuzitumia sheria hizi ili zisiweze kuleta matatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, wakati napitia Muswada huu nilikuwa naangalia kwanza nikawa najiuliza Mheshimiwa Waziri mpaka ameamua kutuletea Muswada huu ili tuweze kuupitisha nini hasa madhumuni yake?

Sasa nikakuta ukurasa wa 48 mpaka 49 Mheshimiwa Waziri ameeleza kwamba nia ya kuuleta Muswada huu anataka kuwepo na mfumo endelevu wa kazi kwa kusimamia utaratibu na masuala ya sheria za kazi. Lakini ameeleza kwamba zitaundwa

taasisi na amezitaja hapa naomba kunukuu kwanza amesema, "Kutaundwa taasisi ya utatu kwa maana ya mwajiri, mfanyakazi na Chama cha Wafanyakazi ambayo itaitwa Baraza la Kazi, Uchumi na Ustawi." Lakini pili, amesema, "Kutaundwa Tume ya Usuluhishi wa Migogoro na kutakuwepo na Kamati ya Huduma Muhimu, kutakuwepo pia Bodi ya Kima cha Chini cha Mishahara na kutakuwepo na Kitengo cha Ukaguzi na pia kutakuwepo Mahakama za Kazi."

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi sina tatizo kabisa na mpangilio huu wa taasisi hizi ambazo zitaundwa. Tatizo langu kubwa ni hili nililolieleza mwanzo kwamba hawa watumiaji wa sheria hii inayoletwa wanao uelewa wa kutosha wa kuitumia sheria hii, hili ndilo tatizo langu. Sasa nilikuwa naangalia pia je, ni kwa kiasi gani Wizara hii ama Waziri ameweza kulitilia maanani ili aweze kufanikisha lengo lake ambalo amelisema ni mfumo endelevu, ni jinsi gani ametilia maanani katika utoaji wa elimu, kwa sababu mimi nafahamu matatizo kama nilivyosema hapo awali kwamba wapo wafanyakazi wetu hawazielewi hizi sheria. Kwa mfano, Mahakama ya Kazi zilikuwepo lakini wafanyakazi hawatambui ni jinsi gani atatokea huko chini na kesi yake mpaka kufikia Mahakama ya Kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili ni tatizo ambalo nimekuwa nikiliona na limekuwa likiwakumba sana viongozi wa Vyama vya Wafanyakazi kiasi sasa hivi viongozi wa Vyama vya Wafanyakazi wanakosa wateja kwa maana hivi anaposhindwa kumtetea mfanyakazi wake siku nyingine mfanyakazi huyo ataamua kweli kujiunga na Chama cha Wafanyakazi akafanye nini? Si itaonekana kwamba hiki Chama hakielewi chochote?

Kwa hiyo, Vyama vya Wafanyakazi vimekuwa na matatizo, vinapoteza wateja wao kutokana na kwamba hakuna elimu ya kutosha kwa viongozi wa wafanyakazi kuanzia ngazi ya matawi, Wilaya, Mikoa, Kanda na hata ngazi ya Taifa.

Kwa hiyo, nilitarajia ama nimwombe basi Mheshimiwa Waziri ili aweze kufanikisha kwa madhumuni hayo ambayo ameyaeleza ukurasa wa 48 mpaka 49, ni vema akatilia mkazo utoaji wa elimu kuweza kuwaelimisha hawa viongozi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ninavyofahamu wafanyakazi na viongozi wa wafanyakazi mara nyingi ni wale wafanyakazi wa kima cha chini. Kwa hiyo, hawana elimu ya kutosha ya kuweza kudai haki zao, lakini pia hawana elimu ya kutosha ya kuweza kuzichambua hizi sheria. Sasa ili tuweze kwenda pamoja basi pamoja na mikakati mizuri ambayo Mheshimiwa Waziri ameiweka ni vema akatilia mkazo suala la elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, huku nyuma mimi nakumbuka kulikuwa na Chuo kinaitwa Chuo cha Wafanyakazi kiko Mbeya, nadhani wenzangu waliowahi kupitia huko watakuwa mashahidi. Chuo hiki miaka ya nyuma kilikuwa kinapata wanafunzi wengi sana lakini sasa hivi chuo hiki hakifanyi kazi vizuri kama ilivyokusudiwa kutokana na huu mfumo tulionao sasa hivi wa ubinafsishaji wa mashirika. Baadhi ya Mashirika ya Umma yanachukuliwa na wenzetu wageni kutoka nje, kwa hiyo, wanapofika pale viongozi wa Vyama vya Wafanyakazi hata kama wangeshauri kwamba wale viongozi wa

Vyama vya Wafanyakazi ngazi hizi za matawi waende wakapewe elimu ili waje wasaidie kiwanda pamoja na wafanyakazi, mwajiri huyu haelewi chochote.

Kwa hiyo, mimi nilikuwa naomba kama suala hili litaanzia huku juu kisha litashuka kwenye Mashirika haya ya Umma ili tutakapokuwa tunafunga nao Mikataba ya kuwakabidhi Mashirika yetu ni vema tukaweka mikakati hii, sharti mojawapo liwe ni kuhakikisha tunawaelimisha viongozi wa Vyama vya Wafanyakazi kuanzia ngazi ya matawi kwenda ngazi ya Wilaya, ngazi ya Mikoa na hata kufikia ngazi ya Taifa. Tukifanya hivi tutakuwa tunaimba wimbo mmoja, lakini bila kuliangalia suala la elimu basi lile lengo ambalo Mheshimiwa Waziri anakusudia itakuwa ni vigumu kulifikia.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo ningependa nilizungumzie wakati najaribu kukipitia kitabu hiki kwa haraka haraka na wenzangu wameliongelea hapa ni kwamba Mheshimiwa Waziri ameeleza kwamba kabla hajauleta Muswada huu amejaribu kushirikisha wadau mbalimbali. Kwa kweli mimi nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa kuweza kuwashirikisha wadau hawa, lakini na mimi niseme tu wasiwasi wangu ni kwamba sina uhakika na hoja zile ambazo wamempa Mheshimiwa Waziri je, ameweza kuzifanyia kazi kabla hajatuletea hapa?

Mheshimiwa Naibu Spika, huo ndio wasiwasi wangu, kwa sababu tunaposema kushirikisha wadau wanaweza wakaleta mapendekezo yao lakini Mheshimiwa Waziri akayapokea na kuyaweka pale na kisha akaleta yale ambayo anayaona yeye yanafaa, sasa je, uhakika kwamba haya waliyochangia ama mawazo yao ameyatilia maanani na kama ameyatilia maanani tulitarajia tuyaone katika kitabu hiki cha leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ninayo taarifa na nina uhakika kabisa Mheshimiwa Waziri kabla hajaleta Muswada huu ni lazima atakuwa amekaa na Chama cha Wafanyakazi nchini Chama kinachoitwa *TUKTA* chini ya Mwenyekiti wake mama Sitta ili kuweza kueleza nia ya kuleta Muswada huu na wao watakuwa wameleta mapendekezo yao.

Sasa mimi bahati nzuri niliweza kupata nakala, lakini nina wasiwasi mkubwa na kwa vile sikuwa na muda kwa hiyo, sikuweza kuchambua ili kuweza kulinganisha je, haya waliyoyaleta kama Chama cha Wafanyakazi nchini ambao ndiyo wametumwa na wafanyakazi wa nchi nzima yameweza kurekebisha vizuri katika Muswada huu kabla hatujaletewa hapa.

Kwa hiyo, nitamwomba sana Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anatoa majibu, ajaribu kunipa uelewa vizuri kama haya yatakuwa yametiliwa maanani. Lakini je, atueleze maana amefumba kwamba ni wadau, lakini aeleze ni wadau gani aliowashirikisha zaidi labda ya viongozi wa Vyama vya Wafanyakazi nchini, ni wadau gani wengine na amechukulia vipi mapendekezo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi niliona niyaseme haya, mengine yamezungumzwa na wenzangu, kwa hiyo, sitapenda kupoteza muda mwingi zaidi. Kwa

hiyo, naomba nirudie tu kwa kusema kwamba naunga mkono Muswada huu kwa asilimia mia moja. Nakushukuruni sana. *(Makofi)*

**MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi ili na mimi nishiriki katika kujadili Muswada huu uliopo mbele yetu na kabla sijaanza kuchangia hoja hii naomba kwanza niwapongeza Mheshimiwa Balozi Getrude Mongella, kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Bunge la Afrika na pia Mheshimiwa Arcado Ntagazwa kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Baraza la Mazingira Duniani. Tunawatakia kheri ili muweze kufanya kazi vizuri katika nyadhifa hizo mlizopata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama mchangiaji aliyemalizia ninayo mambo machache ambayo ningependa kuyazungumzia ili kuweza kuboresha Muswada huu.

Kwanza niwashukuru viongozi wote wa Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo, kuanzia Waziri, Naibu Waziri, Kamishna, Katibu Mkuu pamoja na wafanyakazi wengine kwa jinsi walivyouleta Muswada huu ukiwa na mapendekezo mbalimbali ambayo yatasaidia kuboresha sheria zetu za Tanzania. Kwa kweli ni lazima tukiri kwamba sheria hii au Muswada huu ambao umeletwa mbele yetu kwa kweli umechelewa sana kwa sababu malalamiko ya wafanyakazi wa nchi hii ya Tanzania yamekuwa ni mengi sana na ya muda mrefu, wakilalamikia juu ya sheria hizi zimepitwa na wakati jinsi zinavyopingana, jinsi ambavyo sheria zenyewe hazieleweki vizuri na wafanyakazi wenyewe. Kumbe kuuleta Muswada huu kwa namna moja ni kujaribu kuwasaidia wafanyakazi wa nchi hii ili waweze kuwa na unafuu katika utendaji wa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kama msemaji mmoja aliyetangulia alivyoelezea inaonekana sheria hizi au Muswada huu kwa kiasi kikubwa unawasaidia waajiri au wawekezaji wanaokuja katika nchi hii ili waweze kukubaliana na sheria zetu na ili waweze kufanya kazi ya kuajiri Watanzania. Lakini kama tunavyoelewa wawekezaji wanaokuja katika nchi hii kwa kweli lengo lao kubwa ni kuja kutengeneza faida. Kwa hiyo, wasingependa hata kidogo kuona sheria ambazo zitawabana bana ili washindwe kutengeneza faida kubwa wanayoitaka. Sasa ni lazima tuwe waangalifu sana katika sheria hizi.

Mimi nashukuru kwamba angalau Muswada huu umewekea maanani *ILO Convention* 87 na 98 ya *Freedom of Association* na *Collective Bargaining.* Halafu pia *Convention* namba 100 na 101 ambayo inazungumzia juu ya mshahara halali wa wafanyakazi katika nchi hii na ile ya kuondoa ajira za hatari kwa watoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la ajira katika nchi yetu limekuwa likilalamikiwa sana kwamba kuna ajira ambazo ni za kiubaguzi na Muswada huu umezungumzia, kwa hiyo, nawashukuru sana. Ukiangalia katika ukurasa wa 64 Wizara katika ku-*identify* maeneo ya kuondoa ubaguzi ni pamoja na wagonjwa wa *HIV,* imeongezwa hapa ambayo haikuwepo huko nyuma na ilikuwa inaleta mashaka sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini niseme moja, haya maneno au haya mambo ambayo yameorodheshwa katika kifungu hiki cha nne kuna ubaguzi wa kikabila na *origin* unaweza kuwa mbaya zaidi kuliko ule tunaouzungumzia wa watu kutoka nje wanapokuja kuajiri Watanzania hapa. Hiyo ipo, waajiri kutoka nje hasa hawa wawekezaji, kuna wengine wanapokuja hapa wanakuja na wafanyakazi ambao hawana sifa tofauti na za Watanzania, lakini utakuta kimshahara wanawatenga, Watanzania wanapewa mshahara mdogo na wale kutoka nje pamoja na kwamba pengine hawana elimu au ujuzi zaidi ya Watanzania wanapewa mshahara mkubwa zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa Wizara hii inafanya nini ili kuweza kuhakikisha kwamba inawabana hawa ili waweze kuhakikisha kwamba Watanzania nao wanapata mishahara ambayo inalingana na kazi zao kwa sababu sheria au Muswada huu unazungumza kwamba watu watalipwa mshahara wa haki kutokana na kazi waliyoifanya?

Hivyo, Wizara isipokuwa na watumishi wa kutosha wa kuweza kutembelea sehemu za kazi na kufanya ukaguzi wa mara kwa mara Muswada huu ukipitishwa kuwa sheria, nina uhakika bado kutakuwa na tatizo ambalo wale wanaoajiri kwa ubaguzi wataendelea kufanya hivyo. Na yapo Mashirika au yapo Makampuni ambayo yameishaanzishwa hapa hapa kama wenzangu walivyosema wanatumia kumwajiri mtu kutokana na mahali walipompata *(place of recruitment).* Hii itaendelea kuwatenga watu, lakini pia si kutenga watu kutokana na sehemu walizotoka inawezekana kutokana na *tribe or place of origin* hili likawa ni tatizo kubwa ambalo litatokea katika ajira zetu zinazofanyika hivi sasa.

Hivyo, naomba Wizara iwe na mpango thabiti wa kuweza kufuatilia kwa makini ni jinsi gani watauondoa ubaguzi huo ambao tayari umeshajionyesha waziwazi na wafanyakazi wengi wanalalamikia mpango huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria au Muswada huu nia yake ni kusaidia kulinda ajira ya Watanzania. Sheria hizi zisiposimamiwa zitatoa mwanya kuleta watu kutoka nje ambao watachukua nafasi ambazo na Watanzania wangeweza kuzifanya. Ndiyo maana tunaona kuna ukosefu wa ajira kwa kiasi kikubwa sana katika nchi yetu.

Hivyo, tunaomba sana Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo pamoja na kupitisha sheria hii iandae wafanyakazi wa kutosha katika Wizara hii ambao watazijua sheria hizi ili waweze kuzisimamia kwa karibu kuweza kuwasaidia wafanyakazi wa Tanzania waweze kupata ajira ya kutosha kutokana na nafasi hizi za watu kutoka nje kuja kuwekeza katika nchi yetu.

Kuhusu suala la migogoro ya wafanyakazi. Migogoro ya wafanyakazi inatokea kwa sababu nyingi. Lakini moja ya sababu zinazosababisha migogoro ya wafanyakazi ni kwa wafanyakazi kutoelewa sheria na kanuni zilizowekwa na Serikali. Sasa kwa sababu Mheshimiwa Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo ameleta Muswada huu ambao tuna imani kabisa utapitishwa kuwa sheria inabidi wawepo wafanyakazi watakaofanya kazi kwa makini kuielezea vizuri sheria hii na kuwaelimisha

wafanyakazi juu ya haki na wajibu wao na kuwaelimisha wawekezaji watakaokuja juu ya haki na wajibu wao kwa wafanyakazi ili kuweza kuepusha migogoro inayotokea sehemu za kazi.

Halafu ni kufafanua hizi *terms* zilizotumika katika Muswada huu, *contract of employment,* tunaomba Wizara itoe tafsiri zilizo sahihi kwa sababu kuna *contract* nyingine wanasema ni *oral contract* halafu na nyingine ni *written contract.* Kwa nini *oral contract?*

Kisheria wanasema inaandikwa pale *oral contract,* lakini bado wanaweza kuandikiana Mkataba. Lakini tatizo ni kwamba wale wanaokuwa na uelewa wa sheria wanaweza wakaelewa maana yake nini? Lakini wengi sana ambao wamekuwa wafanyakazi katika Mashirika ya Umma yaliyopita walikuwa hawaelewi jambo hili na mara kwa mara kulikuwa kunatokea migogoro kwenye mambo haya ya *oral contract,* sasa mtoe tafsiri iliyosahihi ili kila mfanyakazi atakayeingia katika Mikataba hii aweze kuelewa anafanya nini anapoingia katika Mikataba hii mbalimbali ambayo imewekwa.

Halafu mikataba mingine wanasema ni ya watoto, mikataba hiyo itakuwa ya namna gani? Naomba sana Wizara izingatie mambo hayo.

Kuhusu suala la kulipia mtu anapopeleka kesi katika Mahakama, hizi fedha ambazo zimewekwa kulipia *filing fees* wenzangu wamelizungumzia. Naiomba Wizara na Mheshimiwa Waziri wafikirie vizuri zaidi kuona ni jinsi watakavyoweza kuwasaidia wafanyakazi wa Tanzania kuhusu suala hili. Kwa sababu si wote wanaokuwa na uwezo wa kuweza kulipia gharama hizo. Sasa itafutwe mbinu itakayosaidia ni jinsi gani ya kuwasaidia hao wafanyakazi ambao watakuwa na kesi zao katika Mahakama.

Kuhusu suala la Makampuni haya ambayo yanafilisika kwa kweli ingekuwa busara kabisa Wizara iangalie ni jinsi gani ya kufikiria kuwalipa kwanza haki wale wafanyakazi kuliko kuanza kufikiria madeni mengine ndiyo yanalipwa, halafu wafanyakazi wanabaki kuhangaika miaka nenda miaka rudi. Kuna kesi nyingi sana ambazo Serikali inaelewa wafanyakazi wa iliyokuwa Afrika Mashariki katika Bandari, Railways na nini? Mpaka leo limekuwa ni tatizo hatuelewi malipo yao yanakwenda namna gani? Kwa sababu Serikali inawachukulia kama walivyo wanaingia katika ajira nyingine, lakini malipo yao ya kule nyuma yameleta migogoro mingi sana.

Sasa Shirika linapofilisika tunaiomba Serikali iingilie kati kuhakikisha kwanza kwamba wafanyakazi wanalipwa kwanza kabla ya kufikiria kulipa madeni mengine, kwa sababu watu ni muhimu sana katika uzalishaji mali. Halafu kuhusu suala la kufungua Akaunti Benki kwa ajili ya wafanyakazi wale ambao hawako kwenye Chama cha Wafanyakazi. Suala hili lisipotiliwa maanani na tukaendelea kufungua Akaunti nyingi kwa ajili ya wafanyakazi wale ambao hawapo katika *Trade Unions* zile zitapunguza nguvu za Vyama vya Wafanyakazi. *(Makofi)*

Mimi nilichokuwa nafikiria ni vizuri akaunti hizi zikafunguliwa katika akaunti zile zile za Vyama vya Wafanyakazi na matatizo yao yanapotokea, basi waweze

kuyashughulikia kama wanavyoshughulikia matatizo mengine kuliko kuwatenga kama ilivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya, mimi naunga mkono hoja na ni matumaini yangu kwamba Wizara itatilia maanani yale ambayo Waheshimiwa Wabunge wamechangia kujaribu kuboresha Muswada huu ili uweze kuwasaidia Watanzania na siyo kuwakomoa wafanyakazi wa nchi hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. STEVEN M. KAHUMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naunga mkono Muswada huu kwa sababu unao mwelekeo wa kuwasaidia watumishi wasiendelee kudhulumiwa kama siyo kumyanyasa kama alivyofanyiwa na anaendelea kufanyiwa Mama Mkemwa na *TRA* na siyo vibaya tukisema na Wizara ya Fedha ambayo licha ya wewe kama Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo ulitoa uamuzi wa kumrejesha *Mrs.* Mkemwa kazini kwake.

Naomba Mheshimiwa Waziri anapohitimisha hoja aelezee jinsi sheria hii itakavyompa uwezo zaidi ya Mawaziri wenzako kuhusu malalamiko ya wafanyakazi na maamuzi ya Wizara yako na wewe mwenyewe binafsi. Naunga mkono hoja.

**MHE. PHILLEMON NDESAMBURO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa nafasi hii. Muswada huu umekuja wakati muafaka kwani utakuwa ni ukombozi wa wafanyakazi, wengi wamenyanyasika katika nchi yao. Pia Muswada unatoa mwongozo mzuri kwa waajiri ili wasiende kinyume na sheria za nchi.

Kuna tatizo moja ambalo litatuletea matatizo mbeleni. Sasa hivi muda si mrefu nchi za Afrika Mashariki, watakuwa na soko moja na Ajira itakuwa *free for all* wanaoishi *East Africa* na siyo hilo tu sio muda mrefu *WTO* na sisi tunatarajia kuwa wanachama na kuwa mwanachama pia utaathiri sheria zetu za uajiri. Dunia inazidi kuwa ndogo na sheria ya ajira kwa nchi itakuwa na utata mkubwa.

Kwa kuwa nchi yetu bado ni ya dunia ya tatu na umaskini bado unatuandama, wawekezaji wanaokuja hapa wana *take advantage* ya umaskini wetu kuingiza katika mikataba wanayo *sign* na sisi kuwa ya uonevu kwani hii mikataba inawapa haki ya kuingiza wafanyakazi kutoka nje na katika mikataba ya namna hii sheria kama hii inashindwa kutekelezwa. Katika mashirika mengi ya namna hii wana wafanyakazi wengi ambao hawastahili kuwepo hapa kwetu. Tunazo sheria nzuri sana kama hii hapa Tanzania, lakini mikataba mingi huwa inatoa mwanya wa kupinda sheria za nchi. Naomba Serikali iwe macho sana hasa wakati wa kuingia mikataba na wawekezaji. Wawekezaji wa ndani, ndiyo hawageuki sheria hizi lakini ni wageni na kama sheria hii itafuatwa na wageni, basi hali ya waajiri na waajiriwa itakuwa inaendeleza uchumi wa nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo Mheshimiwa Naibu Waziri na Watendaji Wakuu kwa maandalizi ya Muswada huu wenye lengo la kurekebisha sheria ya ajira ambayo ilikuwa imepitwa na wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa maoni na mapendekezo katika maeneo yafuatayo:-

Kwanza sehemu ya 19(2)(a) na (b) kwa kuwa sehemu ndogo (a) na (b) zinazungumzia kiwango cha siku za kawaida za kazi na saa za kazi kwa wiki ni muhimu kuweka uzito kwamba siku hizo na saa hizo hazitahusu siku za mapumziko *(Public Holidays)* zinazoangukia siku hizo na saa hizo za kawaida za kazi. kama ilivyo katika sehemu 25 kutofanya hivyo kunaweza kutoa mwanya kwa waajiri wakorofi kupinda sheria.

Pili, sehemu ya 20(1) inayohusu usiku *(night)* kwa kawaida hata kwa matamshi ya mazoea kwa jamii, usiku unaanza saa 1 usiku na hivyo ndivyo inavyotamkwa na wala siyo saa 1 jioni. Hivyo muda muafaka uwe unaanza saa 1 usiku badala ya saa 2 usiku *(after 20 hours)* kama ilivyoandikwa katika Muswada.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia sehemu ya 20(2)(b) Mama anayenyonyesha afanye kazi za kujifungua ni kumnyima haki mtoto mchanga kupata lishe ya Mama wakati wa usiku kwa kawaida Mama ananyonyesha kwa zaidi ya mwaka mmoja lakini mtoto anaanza kupewa chakula laini baada ya miezi sita hivyo badala ya miezi miwili sasa iwe miezi sita.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho naomba Mheshimiwa Waziri atoe tafsiri sahihi katika sehemu ya 42 inayohusu *severance pay.* Tafsiri inaonyesha ni mshahara wa siku saba kwa muda wa miaka halisi ya ajira. Kwa mfano, mshahara wa mfanyakazi ukiwa shilingi 70,000/= kwa mwezi maana yake ni 70,000 ukigawa kwa 30 = 2,333 kwa siku saba ni shilingi 16,221 kwa miaka ya kazi 10 ni sawa na shilingi 16,2210 kama *severance pay* kwa mtumishi huyo aliyefanya kazi kwa miaka 10. Iwapo tafsiri hiyo ni sahihi basi kiwango hicho ni kidogo sana kwa mtumishi huyo inapendekezwa iwe mshahara wa miezi saba kwa muda wa ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho naunga hoja mkono.

**MHE. SEMINDU K. PAWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Waziri ajibu maswali yangu hapa aniridhishe ili niunge mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri apokee pongezi zangu kwa kuzingatia hoja zetu katika kikao cha Februari, 2004 ambapo Muswada huu ulirudishwa?

Kwanza, hivi ni kweli au uvumi usio na ushahidi kuwa Muswada huu umeletwa kwa shinikizo la wawekezaji wageni? Je, hoja 32 za wadau zilizotolewa katika kujadili Muswada huu ngapi zimezingatiwa na kwa maslahi ya nani?

Pili, fidia ya viungo mfanyakazi anapouumia nasikia viwango hutungwa na Kanuni za Wizara, nasikia baadhi ya Wizara ikiwemo Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, je, Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo itasukuma jambo hili kwa kiasi gani ili wanaoumia wasipunjwe?

Tatu, wawekezaji uchwara ambao wanakuja na wafanyakazi wao wa kutoka nchi zao hata kwa kazi za uhudumu, ulinzi, udereva ingawa hapa nchini tunao, je, Muswada huu unazingatiaje nafasi hii ili kutoa fursa kwa Watanzania?

Nne, waajiri wakorofi ambao hunyanyasa wafanyakazi. Je, hatua zimewekwa waondolewe nchini au adhabu kali?

Mwisho, Muswada huu ingawa unapitishwa hivi sasa kwa kujihami hami je, baadae tukiona utekelezaji wake mbovu Bunge hili linaweza kufuta na kuomba maeneo yenye utata?

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali itengeneze sheria nzuri ya kazi ambayo itawapa maisha bora wafanyakazi kwa sababu ndiyo wao wanaoanya kazi zote hapa nchini wao ndiyo walipa kodi ya kuendesha Serikali, wapiga kura nyakati za uchaguzi na wafanyakazi pia ndiyo walinzi wa amani. Kwa hiyo, zawadi kubwa ya kumpa mfanyakazi ni kumtungia sheria nzuri itakayomsaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka sasa mabadiliko ya uchumi yanamwelemea sana mfanyakazi pekee na waajiri wanapeta kwa raha. Inasikitisha sana kuona wawekezaji wanawaajiri wafanyakazi bila Mkataba. Utafiti umefanyika na kubaina ya kwamba 40% ya wafanyakazi hawana mikataba ya kazi kama vile Mgodi, Mahoteli ya Kitalii, Kampuni za Uwindaji, Kampuni za Kusafirisha Watalii na Kampuni ya Gesi ya Songosongo.

Mheshimiwa Naibu Spika, inasikitisha sana kuona kwamba hapa kwetu wawekezaji ambao siwezi kuogopa kusema ya kwamba wengi wao wanatoka Afrika ya Kusini wanawaona wafanyakazi wa Kitanzania tofauti na huko walikotoka kwa sababu ya Vyama vya Wafanyakazi huko *(Trade Union)* huko vina nguvu sana.

Mheshimiwa Spika, ninaomba sana Vyama vya Wafanyakazi hapa kwetu vipate uwezo wa kuwatetea wafanyakazi wanao wanaowawakilisha. Moja ya Jimbo la Mbunge ni wafanyakazi waliopo kwenye eneo analoliwakilisha. Mpaka sasa wafanyakazi wanauliza wameikosea nini Serikali mpaka inasahau umuhimu wao?

Mheshimiwa Naibu Spika, ni lazima Serikali ijue ya kwamba njia moja ya mfanyakazi kudai haki yake ni kugoma. Inashangaza sana pale wafanyakazi wa

kiwanda fulani wakigoma hawalipwi zile siku na Serikali inaunga mkono. Sasa hivi tupo kwenye dunia ya utandawazi ni lazima Serikali iangalie, Serikali za wenzetu wanafanya nini pale wafanyakazi wanapogoma. Ukweli ni kwamba wanalipwa mishahara yao kama kawaida.

Mheshimiwa Naibu Spika, inasikitisha sana kuona hawa wawekezaji hawaajiri wasomi Watanzania wenye sifa ambao wakienda nje wanagombaniwa na kupewa mishahara mikubwa. Inasikitisha kuona hata msomi Mtanzania akiajiriwa anapewa mshahara mdogo kuliko hata mgeni asiyemzidi elimu. Sasa umefika wakati ambapo wageni ni lazima wapewe masharti ya kuwaajiri wasomi wetu.

Nimalizie kwa kusema ya kwamba hivi hata walinzi ni lazima watoke nje kama kutumia Kampuni za Ulinzi si hata hapa zipo tena nyingi zinamilikiwa na wageni? Pia hapa kwetu tunao wapishi, madobi na kadhalika wazuri wengi tu hebu hii sheria mpya iwaangalie na hao.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono marekebisho ya sheria hii mia kwa mia.

**MHE. TEMBE K. NYABURI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naanza kwa kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja, lakini ninayo machache ya kuchangia kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati sheria hii inaandaliwa ni vema ilinde maslahi ya Mtanzania. Mfano nilipata fursa pamoja na Waheshimiwa Wabunge wenzangu wa Mkoa wa Mara kutembelea mgodi wa Nyamongo, Tarime. Pale tulikuta *Geologist* kutoka Canada mwenye sifa sawa kielimu na Watanzania, lakini yeye analipwa mshahara zaidi ya mara tano kuzidi Watanzania wenye sifa kama za Mzungu huyo. *Geologist* wa Tanzania analipwa shilingi 900,000/= na Mcanada huyo analipwa kati ya dola 4,000 mpaka dola 6,000. Sheria itamke na kuwataka waajiri kuwasikiliza waajiriwa pindi wanapokuwa na malalamiko ya msingi. Wajadiliane kuondokana na mizozo sehemu za kazi kwani inaweza kufikia kuvuruga amani na utulivu nchini.

**MHE. KHERI KHATIB AMEIR:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa dhati kabisa naomba kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu wake, Watendaji wa Wizara, Katibu Mkuu na timu yake kwa kuwezesha kuleta Muswada huu mbele ya Bunge lako Tukufu kwa wakati. Ni Muswada tuliokuwa tukiusubiri kwa muda sasa na kuletwa kwake kunaleta faraja kweli kama wawakilishi wa wananchi na wapigakura wote kwa jumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kuwa Muswada umepiga marufuku ajira za watoto ili kutekeleza haki za binadamu, lakini hili lipo hasa katika sehemu za mashamba ya tumbaku, chai na kwenye maeneo ya uchimbaji wa madini. Si hilo tu bali maeneo ya utalii kando kando mwa fukwe na maeneo ya uvuvi suala hili limeshamiri, watoto hawaendi shuleni wanafuatana na watalii pamoja na kupaa samaki.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo ya mijini, miji mikuu kama Dar es Salaam, Mbeya, Arusha na hata Dodoma utawakuta njiani wanatembeza mayai na njugu (karanga) mitaani. Hili ni kosa kubwa na ni janga la Taifa siku za usoni. Kuhusu ajira kwa jumla imekuwa ni tabia hivi sasa ajira/waajiri wengi kutoka nje za nchi kwa visingizio tu vya elimu ya juu. Ninao ushahidi, kuna kiwanda cha Sigara *(TTC)* wameajrii watu kutoka Kenya na *South Africa* na kwingineko katika nafasi ambazo Watanzania wana uwezo nazo. Wanaachwa Watanzania bila ya sababu za msingi pamoja na kuwa kielimu Watanzania wana uwezo au wameelimika zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna kauli ya kuwa kuna Watanzania asilimia 40 hadi 42 walioajiriwa viwandani Tanzania hawana mikataba ya kudumu na wengi wao wanadhalilika na kutumwa bila ya mpango. Kuna wanaoteswa na hata baadhi yao kufukuzwa pale wanapodai au kuuliza juu ya suala hilo la mikataba. Pia, kuna unyanyasaji wa kijinsia na rushwa za wapenzi. Wako wanaokubali au kuacha kazi kwa visingizio endapo endapo watakataa. Kuhusu maslahi, kuna haja ya Wizara ya Utumishi kwa kushirikiana na Wizara yako kuangalia tena suala hili la maslahi na kiwango cha chini cha mishahara ya Wafanyakazi, kiwango kilichopo sasa ni kidogo. Nashauri vile vile Wizara yako iongee na Wizara ya Utumishi juu ya suala la uwekaji wa kumbukumbu ili kuboresha mafao ya Wafanyakazi na stahili zao wakati wanapomaliza muda wao wa ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili tunaliona jepesi kwa sasa kwani halitugusi moja kwa moja, lakini ni zito sana na wala halina mantiki ya wale waliojaribu kuchelewesha mafao yao kwa sababu eti hakuna kumbukumbu. Wewe unamtumiaje mfanyakazi muda wote wakati huna hata kumbukumbu zake za uajiri na mwenendo wake wa kazi? Huu ni uhalifu wa haki za binadamu. Ahsante.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa Wizara hii inafanya nini ili kuweza kuhakikisha kwamba inawabana hawa ili waweze kuhakikisha kwamba Watanzania nao wanapata mishahara ambayo inalingana na kazi zao kwa sababu sheria au Muswada huu unazungumza kwamba watu watalipwa mshahara wa haki kutokana na kazi waliyoifanya?

Hivyo, Wizara isipokuwa na watumishi wa kutosha wa kuweza kutembelea sehemu za kazi na kufanya ukaguzi wa mara kwa mara Muswada huu ukipitishwa kuwa sheria, nina uhakika bado kutakuwa na tatizo ambalo wale wanaoajiri kwa ubaguzi wataendelea kufanya hivyo. Na yapo Mashirika au yapo Makampuni ambayo yameishaanzishwa hapa hapa kama wenzangu walivyosema wanatumia kumwajiri mtu kutokana na mahali walipompata *(place of recruitment).* Hii itaendelea kuwatenga watu, lakini pia si kutenga watu kutokana na sehemu walizotoka inawezekana kutokana na *tribe or place of origin* hili likawa ni tatizo kubwa ambalo litatokea katika ajira zetu zinazofanyika hivi sasa.

Hivyo, naomba Wizara iwe na mpango thabiti wa kuweza kufuatilia kwa makini ni jinsi gani watauondoa ubaguzi huo ambao tayari umeshajionyesha waziwazi na wafanyakazi wengi wanalalamikia mpango huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria au Muswada huu nia yake ni kusaidia kulinda ajira ya Watanzania. Sheria hizi zisiposimamiwa zitatoa mwanya kuleta watu kutoka nje ambao watachukua nafasi ambazo na Watanzania wangeweza kuzifanya. Ndiyo maana tunaona kuna ukosefu wa ajira kwa kiasi kikubwa sana katika nchi yetu.

Hivyo, tunaomba sana Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo pamoja na kupitisha sheria hii iandae wafanyakazi wa kutosha katika Wizara hii ambao watazijua sheria hizi ili waweze kuzisimamia kwa karibu kuweza kuwasaidia wafanyakazi wa Tanzania waweze kupata ajira ya kutosha kutokana na nafasi hizi za watu kutoka nje kuja kuwekeza katika nchi yetu.

Kuhusu suala la migogoro ya wafanyakazi. Migogoro ya wafanyakazi inatokea kwa sababu nyingi. Lakini moja ya sababu zinazosababisha migogoro ya wafanyakazi ni kwa wafanyakazi kutoelewa sheria na kanuni zilizowekwa na Serikali. Sasa kwa sababu Mheshimiwa Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo ameleta Muswada huu ambao tuna imani kabisa utapitishwa kuwa sheria inabidi wawepo wafanyakazi watakaofanya kazi kwa makini kuielezea vizuri sheria hii na kuwaelimisha wafanyakazi juu ya haki na wajibu wao na kuwaelimisha wawekezaji watakaokuja juu ya haki na wajibu wao kwa wafanyakazi ili kuweza kuepusha migogoro inayotokea sehemu za kazi.

Halafu ni kufafanua hizi *terms* zilizotumika katika Muswada huu, *contract of employment,* tunaomba Wizara itoe tafsiri zilizo sahihi kwa sababu kuna *contract* nyingine wanasema ni *oral contract* halafu na nyingine ni *written contract.* Kwa nini *oral contract?*

Kisheria wanasema inaandikwa pale *oral contract,* lakini bado wanaweza kuandikiana Mkataba. Lakini tatizo ni kwamba wale wanaokuwa na uelewa wa sheria wanaweza wakaelewa maana yake nini? Lakini wengi sana ambao wamekuwa wafanyakazi katika Mashirika ya Umma yaliyopita walikuwa hawaelewi jambo hili na mara kwa mara kulikuwa kunatokea migogoro kwenye mambo haya ya *oral contract,* sasa mtoe tafsiri iliyosahihi ili kila mfanyakazi atakayeingia katika Mikataba hii aweze kuelewa anafanya nini anapoingia katika Mikataba hii mbalimbali ambayo imewekwa.

Halafu mikataba mingine wanasema ni ya watoto, mikataba hiyo itakuwa ya namna gani? Naomba sana Wizara izingatie mambo hayo.

Kuhusu suala la kulipia mtu anapopeleka kesi katika Mahakama, hizi fedha ambazo zimewekwa kulipia *filing fees* wenzangu wamelizungumzia. Naiomba Wizara na Mheshimiwa Waziri wafikirie vizuri zaidi kuona ni jinsi watakavyoweza kuwasaidia wafanyakazi wa Tanzania kuhusu suala hili. Kwa sababu si wote wanaokuwa na uwezo wa kuweza kulipia gharama hizo. Sasa itafutwe mbinu itakayosaidia ni jinsi gani ya kuwasaidia hao wafanyakazi ambao watakuwa na kesi zao katika Mahakama.

Kuhusu suala la Makampuni haya ambayo yanafilisika kwa kweli ingekuwa busara kabisa Wizara iangalie ni jinsi gani ya kufikiria kuwalipa kwanza haki wale wafanyakazi kuliko kuanza kufikiria madeni mengine ndiyo yanalipwa, halafu wafanyakazi wanabaki kuhangaika miaka nenda miaka rudi. Kuna kesi nyingi sana ambazo Serikali inaelewa wafanyakazi wa iliyokuwa Afrika Mashariki katika Bandari, Railways na nini? Mpaka leo limekuwa ni tatizo hatuelewi malipo yao yanakwenda namna gani? Kwa sababu Serikali inawachukulia kama walivyo wanaingia katika ajira nyingine, lakini malipo yao ya kule nyuma yameleta migogoro mingi sana.

Sasa Shirika linapofilisika tunaiomba Serikali iingilie kati kuhakikisha kwanza kwamba wafanyakazi wanalipwa kwanza kabla ya kufikiria kulipa madeni mengine, kwa sababu watu ni muhimu sana katika uzalishaji mali. Halafu kuhusu suala la kufungua Akaunti Benki kwa ajili ya wafanyakazi wale ambao hawako kwenye Chama cha Wafanyakazi. Suala hili lisipotiliwa maanani na tukaendelea kufungua Akaunti nyingi kwa ajili ya wafanyakazi wale ambao hawapo katika *Trade Unions* zile zitapunguza nguvu za Vyama vya Wafanyakazi. *(Makofi)*

Mimi nilichokuwa nafikiria ni vizuri akaunti hizi zikafunguliwa katika akaunti zile zile za Vyama vya Wafanyakazi na matatizo yao yanapotokea, basi waweze kuyashughulikia kama wanavyoshughulikia matatizo mengine kuliko kuwatenga kama ilivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya, mimi naunga mkono hoja na ni matumaini yangu kwamba Wizara itatilia maanani yale ambayo Waheshimiwa Wabunge wamechangia kujaribu kuboresha Muswada huu ili uweze kuwasaidia Watanzania na siyo kuwakomoa wafanyakazi wa nchi hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. STEVEN M. KAHUMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naunga mkono Muswada huu kwa sababu unao mwelekeo wa kuwasaidia watumishi wasiendelee kudhulumiwa kama siyo kumyanyasa kama alivyofanyiwa na anaendelea kufanyiwa Mama Mkemwa na *TRA* na siyo vibaya tukisema na Wizara ya Fedha ambayo licha ya wewe kama Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo ulitoa uamuzi wa kumrejesha *Mrs.* Mkemwa kazini kwake.

Naomba Mheshimiwa Waziri anapohitimisha hoja aelezee jinsi sheria hii itakavyompa uwezo zaidi ya Mawaziri wenzako kuhusu malalamiko ya wafanyakazi na maamuzi ya Wizara yako na wewe mwenyewe binafsi. Naunga mkono hoja.

**MHE. PHILLEMON NDESAMBURO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa nafasi hii. Muswada huu umekuja wakati muafaka kwani utakuwa ni ukombozi wa wafanyakazi, wengi wamenyanyasika katika nchi yao. Pia Muswada unatoa mwongozo mzuri kwa waajiri ili wasiende kinyume na sheria za nchi.

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi nitoe maoni yangu na mchango wangu katika Muswada ambao upo mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, ningependa kuwatoa wasiwasi Waheshimiwa Wabunge kwamba chimbuko na madhumuni ya Muswada huu unatokana na nguvu za kutoka nje au za wawekezaji.

Mheshimiwa Waziri alipokuwa anatoa hoja ya kuuleta Muswada huu hapa alisema Sheria tulizonazo sasa zimetungwa kati ya miaka ya 1949 na 1967 na kutokana na mabadiliko ya kiuchumi na utandawazi kwa ujumla ni dhahiri sheria hizi zilikuwa zimepitwa na wakati na hivyo tulihitaji kuzifanyia mabadiliko. Kwa hiyo, chimbuko la msingi na madhumuni ni sheria hizi ziweze kwenda na wakati tukitilia maanani kwamba ni za muda mrefu sana.

Lakini jambo la pili, ambalo ningependa kulichangia la ujumla ni kwamba sehemu kubwa ya mapendekezo ya wadau ambao hata dada yangu Mheshimiwa Hadija Kusaga, amezungumzia hapa yametiliwa maanani. Ndiyo maana Muswada ambao uliletwa hapa Kusomwa kwa Mara ya Kwanza hata ule ambao ulipelekwa kule Morogoro ukiuangalia una mabadiliko makubwa sana na huu ambao tumekabidhiwa hapa wa sasa. Lakini pamoja na hayo bado tuna mapendekezo mengine ambayo yametolewa kufuatana na Muswada huu, hii ni kuonyesha kwamba tumejitahidi kuzingatia karibu yote ambayo tumeona kwamba yakiingia humu ndani hayatatuletea mgogoro katika mahusiano ya kazi na ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningeomba nianze kuchangia hoja za kiongozi wa upande wa Upinzani katika Wizara hii Mheshimiwa Khalifa Mohammed Issa, yeye alisema kwenye kifungu cha 15(b) neno *place of recruitment* libadilishwe na badala yake liwekwe neno *place of domicile.*

Najua tatizo linalotukuta hapa kuna watu tunaowafikiria wale ambao wameshaajiriwa tayari ambao wanao wa kuwasemea, Vyama vya Wafanyakazi, lakini tungepaswa vile vile kuangalia na upande wa pili. Wale ambao hawajaajiriwa, lakini wanaitafuta hiyo ajira. Unaponipa mimi masharti kwamba nikitaka kumuajiri mpiga pasi pale kwangu lakini nimrudishe kule alikozaliwa ndiyo *domicile* hiyo au huyu mwingine anasema ahaa mimi Bwana niko tayari hapa hapa unaponiajiri.

Kwa mwajiri wa sekta binafsi ni dhahiri atamchukua huyu mwenye gharama ndogo na tusipoangalia katika hili tutafikia mahali wale ambao wanatoka Mchinga, Urambo, Wete hawatakuwa na urahisi wa kupata ajira za Dar es Saalam au kwenye machimbo ya migodi ya Mwanza, maana yake kila mtu anafikiria nimchukue yule wa karibu, hii ndiyo hofu yetu sisi. Sasa wapo wanaowafikiria tayari wameshaajiriwa, lakini hili nataka niwathibitishieni linawezekana kabisa kutatuliwa katika Mikataba ya hiyari ambayo Muswada wetu huu umewekea nguvu kweli kweli juu ya Mikataba ya hiyari.

Kifungu cha 40(3) mwajiri akikataa amri ya kumrudisha mfanyakazi kazini alipe fidia ya miezi 18 badala ya miezi 12 iliyopendekezwa na sheria hii.

Ningeomba kuwafahamisha Waheshimiwa Wabunge kwamba huyu anapokataliwa kurudishwa kazini ana haki zake tayari za kisheria, lakini ili kumfanya huyu mwajiri asiwe na kiburi cha kumfanya huyu mtu asirejeshwe kazini, ndiyo maana tunamwambia basi zaidi ya hayo malipo yake ya kisheria lazima umlipe na fidia ya miezi 12. Kwa hiyo, hii miezi 12 ni kumfanya huyu mtu aone uvivu hivi wa kumkatalia huyu aliyerejeshwa kazini kuja kwenye sehemu yake. Kwa hiyo, hii ni ziada tu ya malipo yale ya lazima ya kisheria ambayo tayari yapo.

Kifungu cha 42(1) malipo ya kiinua mgongo kwa nini ni ya siku saba kila mwezi kwa miaka 10 ni kidogo bora yale ya zamani. Malipo haya yatakuwa yanalipwa pamoja na pensheni ya mfanyakazi kinyume na ilivyo sasa ambapo mfanyakazi analipwa kimojawapo kinachoonekana ni kikubwa zaidi. Sisi tunaamini kwamba kiwango hiki kinaweza kuongezwa kupitia Mikataba ya Hiyari kuliko kama tungekiacha cha mwanzo kama kilivyo, pengine kingekuwa kinamuumiza zaidi mfanyakazi huyu tunayemtetea sote hapa badala ya huu mpango wa sasa ambao tunaamini Mikataba ya Hiyari, na ndiyo lengo kubwa sasa hivi mikataba ya hiari ndiyo maana imepewa nguvu ya kisheria katika Muswada huu.

Kifungu cha 42(2)(b), malipo ya kiinua mgongo yafanyike kwa mfanyakazi ambaye amemaliza kipindi cha majaribio na siyo kigezo cha kufanya kazi miezi 12. Hofu yetu hapa ni ndogo tu, kiinua mgongo ni pamoja na mchango wa mfanyakazi kwa mwajiri wake, unapompa huyu kiinua mgongo cha miezi 12 kunatoa mwanya kwa mfanyakazi wa aina hiyo kulipwa kiinua mgongo ambacho hajakitolea mchango wake kwa mwajiri wake.

Kifungu cha 42(3)(b) kuondoa maneno *any other employer* katika kifungu cha 42(3)(b) na hii nayo hofu yetu ipo katika kumlinda mfanyakazi. Tujalie Shirika moja limeamua kugawanywa katika sehemu mbili katika haya mabadiliko. Huyu mwajiri ana haki ya kuhakikisha mfanyakazi huyu badala ya kubakia bila kazi anamuwezesha kuingia katika kitengo kingine kilichozaliwa kutokana na hiki kipya na tunaweza tukayaona kabisa haya kwa yale Mashirika ambayo yamefanyiwa mabadiliko yakatokea sehemu mbili, sijui *Holding Company,* sijui kitu nini, kama huyu angeachwa hivi hivi bila kipengele hiki cha *any other employer* kuna hatari mfanyakazi huyu atabakia bila ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningeomba niwathibitishie Waheshimiwa Wabunge kwamba madhumuni makubwa ya Muswada huu ni kuhakikisha kwamba mfanyakazi analindwa na siyo kumuinua mwajiri peke yake.

Kifungu cha 72(d) kuvitaja Vyama vya Wafanyakazi kufungua akaunti mbili, moja kwa ajili ya michango ya wanachama na ya pili, ni kwa ajili ya wafanyakazi wasio wanachama ni kuongeza urasimu. Hili linashangaza kidogo kuna wafanyakazi ambao kwa hiyari zao wenyewe kwamba mimi nitakuwa mwanachama wa Chama kadhaa, mfanyakazi mwingine anasema ahaa mimi nitachangia kwa sababu ndiyo sheria inanitaka

hivyo. Sisi tunasema akaunti hizi mbili kuzichanganya pamoja kwa mtu wa hiyari yake na mwingine ambaye anachukuliwa tu mchango wake kwa sababu ni mfanyakazi ni kumnyima haki huyu kwa sababu ile akaunti moja wengine wana haki ya kuisemea na hawa wengine hawana.

Lakini Waheshimiwa Wabunge akaunti hizi zote mbili zinaendeshwa na Chama cha Wafanyakazi hicho hicho, hakuna akaunti ambayo inaendeshwa na watu wengine, wao ndiyo wanatunza na wao ndiyo wana-*operate* hizo akaunti. Tunafanya hivi kwa maana tu ijulikane kila kundi mambo yake yanakwendaje? Sasa hili hatuoni kwa nini linapigiwa kelele hivyo kuna nini hasa? Kama akaunti zote mbili wanazi-*operate* wenyewe, huu woga uko wapi mpaka mnataka tuzichanganye pamoja tupate hata tabu ya kujua kundi hili wamechangia kiasi gani na kundi hili wamechangia kiasi wasiwasi wetu uko wapi?

Mimi naomba Waheshimiwa Wabunge tusiwe na wasiwasi na hili, nia yetu njema na akaunti zote mbili zitasimamiwa na Vyama vya Wafanyakazi wenyewe, hakuna mkono wa Serikali wala mkono wowote utakaoingia katika akaunti hizo.

Mheshimiwa Mgana Msindai, alizungumzia kama Muswada umezingatia hoja ya kuwa na Mikataba ya Kazi. Ni kweli kabisa Muswada huu umezingatia na ukiangalia kifungu cha 96 chote kinaeleza habari hii ya Mikataba. Kama maslahi ya wafanyakazi waliogoma yanalindwa, naam kifungu cha 83 kinamzuia mfanyakazi aliyeshiriki katika mgomo halali asifukuzwe au asifunguliwe kesi ya madai au jinai. Mwajiri huyo ataendelea kuwasilisha michango ya mfanyakazi huyo katika Mfuko au sehemu zinakostahili. Aidha, kama mfanyakazi amepewa nyumba na mwajiri hatakiwi kumfukuza hadi hapo suala hili litakapokuwa limekamilika. Kwa hiyo, maslahi au mafao yao yanaangaliwa.

Lingine alisema kama mazingira ya kazi yanaboreshwa katika Muswada huu. Muswada huu unaboresha mazingira ya kazi na sehemu ya pili ya Muswada huu ambayo inazungumzia haki za msingi za mfanyakazi, na pia sehemu ya tatu ya Muswada imeweka viwango vya chini ambavyo kila mwajiri atatakiwa kuvizingatia. Kwa hiyo, Muswada huu unalinda mazingira ya wafanyakazi.

Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe, yeye alizungumzia sana kifungu cha 7(4), akataka kifungu hiki kiandikwe upya kuzingatia Utaifa, tunazungumzia ubaguzi kwenye kifungu hiki. Nataka nikuthibitishie kwamba kifungu hiki kinamtanguliza mfanyakazi ambaye tayari yupo kwenye ajira siyo yule ambaye anatakiwa kuajiriwa.

Sasa huyu mtu akishaajiriwa basi asibaguliwe kwa namna yoyote kwa misingi iliyoonyeshwa palekwenye kifungu cha 7(4), kama ni mlemavu, kama ana Ukimwi, kama sijui ana umri ambao haruhusiwi kapitwa na wakati, ingawa umri wa kufanya kazi upo, yule ambaye tayari yupo kazini siyo anayetaka kuajiriwa. Sasa mtu akiajiriwa basi haya yaliyokuwepo hapa ndiyo yaangaliwe, na hii watu wengine wanaipigia kelele hii tribe hawaitaki, lakini lazima tukubaliane ukabila upo, ukabila upo. Ukiniachia mimi kwenye nafasi yangu kuna hatari nitamleta Mmachinga tu. Sasa tuweke humu ili

ukabila tunaozungumza hapa siyo wa namna wa kuajiri, huyu aliyeajiriwa asinyanyaswe kwa sababu ya *a, b, c, d* kama ilivyoonyeshwa kwenye kifungu cha 7(4).

Mheshimiwa Benedicto Mutungirehi, alizungumzia kifungu cha 7(6)(b) anapinga kuhusu ubaguzi unatokana na matakwa ya kazi yenyewe, lile neno *inherent* nafikiri ndiyo limempa taabu sana, akatoa mpaka mfano kwamba Chama fulani kinaweza kuchukua chipukizi kikawafundisha, kika-*collapse their mental,* akataka nisimjibu kisiasa na mimi sitaki kumjibu kisiasa.

Huu siyo ubaguzi, tunachozungumzia hapa ajira ilingane na matakwa ya kazi yenyewe, kama anayetakiwa ni dreva wa *Class C* basi huyo wa *Class D* asiajiriwe tu kwa sababu eti anajua kuendesha gari tu aende, ndiyo maana hii hapa. Siyo chipukizi kufundishwa gwaride la Chama cha Mapinduzi, hata kidogo.

Kifungu cha 5(1) watoto kuajiriwa na Vyama vya Siasa ndiyo hilo nimelizungumzia. Lakini alisema kunakuwepo na Afisa Kazi katika majadiliano kati ya mwajiri na mfanyakazi, hakuna kifungu kama hicho katika Muswada huu. Majadiliano yanaposhindikana wahusika wanakwenda kwenye *Commission* ya Usuluhishi. Sijui aliitoa wapi hii?

Mheshimiwa Leonard Derefa, alizungumzia haki ya watumishi wa Umma ya kuanzisha Vyama vya Wafanyakazi. Chini ya Muswada wa Sheria hii wafanyakazi wanaruhusiwa kujiunga na kuanzisha Vyama vyao. Kwa hiyo, wasiwe na wasiwasi wakiwa tayari au wakijisikia wanaweza wakafanya hilo.

Tofauti ya mishahara kati ya watumishi ya Serikali kwa kweli masuala haya hayahusiani na Muswada huu, kwamba kwa nini Wizara moja viwango vyake vya mishahara vinaanzia hivi wakati Serikali ni hiyo hiyo, humu haipo ni masuala ya utekelezaji na mimi naamini wanaohusika na hilo watakuwa wame-*take note.*

Kuhusu ubaguzi katika mishahara migodini, Muswada huu unazuia ubaguzi na unaimarisha ukaguzi kazini ili kubaini aina hizo za ubaguzi. Kwa hiyo, Muswada huu ukipita utawasaidia wakaguzi wetu kuyafuatilia hayo.

Amezungumzia habari ya *on call allowance* kwa daktari hasa wakati ule wa mlipuko wa kipindupindu. Malipo haya hayahusiani na Muswada huu ni masuala ya utekelezaji. Kwa hiyo, nafikiri wale watekelezaji wataona namna nzuri ya kuweza kulishughulikia eneo hili.

Kifungu cha 6(1) neno *may,* hili lilizungumza na dada yangu Mheshimiwa Rosemary Nyerere, tunaliondoa tumekubali. Kifungu cha 6(2)(c) ulikuwa unataka ufafauzi wa kipengele kile cha 2(c) hivi maana yake nini?

Kipengele hiki kinamzuia kwa mfano, mfungwa kwenda kufanya kazi kwa Mheshimiwa Rosemary Nyerere. Tunapozungumzia *community services* kuna masuala ya shule, kujenga madarasa, Zahanati, lakini siyo ile ambayo sasa unaweza ukaiona

anakuja kwangu Mudhihir anafanya kazi, sasa hii siyo kazi za kijamii hizi. Nafikiri litatolewa ufafanuzi zaidi kwenye ule Muswada wa mambo ya wafungwa utakapofika.

Mheshimiwa Margareth Mkanga, alizungumzia waajiri watakaoajiri walemavu wapewe motisha, hili tunaliogopa sana hili. Hatupendi Serikali ionekane kama kuajiri mlemavu ni kumpendelea, mlemavu kama ana sifa ana haki kama Mtanzania mwingine yeyote kuajiriwa. Sasa watu wasije wakajenga ile kwamba huyu ameajiri walemavu basi apewe motisha namna hii. Mlemavu kama Mtanzania mwingine yeyote ikiwa anayo sifa na haki ya kuajiriwa na anayeajiri anafanya hivyo kwa kutekeleza wajibu wake kwa mujibu wa Muswada huu, na hivyo hahitaji motisha au zawadi ya namna ya pekee.

Kuhusu kifungu cha 19, je, Serikali inarudisha Jumamosi kufanya kazi mbona kuna siku sita? Msingi wa hii hapa ni kwamba saa za kufanya kazi kwa wiki ni 45, sasa hata hivi leo Serikali mwanzoni tulikuwa tunamaliza kazi saa 8.30, ili tuipate siku ya Jumamosi tukaamua kusogeza mpaka saa 9.30, wale watumishi wa siku nyingi wanafahamu na hata leo kuna baadhi ya Mashirika kama Benki, wanasema wakiacha kufanya kazi siku ya Jumamosi wataumiza wateja wao. Kwa hiyo, wanakwenda kufanya kazi mpaka saa 6.00 au saa 7.00 mchana wakapumzika, saa 8.00 wakarudi ili zipatikane zile saa zao 45. Kwa hiyo, hatufuti siku ya Jumamosi lakini waajiri wana namna yao ya kuhakikisha kwamba hizi saa 45 kwa wiki zinapatikana.

Mheshimiwa Leonard Shango, alisema Muswada unatamka vipi kuhusu watumishi wa umma, umetamka vizuri katika kifungu cha 2(1). Muswada unasemaje kuhusu wafanyakazi wa wito? Muswada unazungumzia maslahi ya wafanyakazi wote bila kujali taaluma zao. Lakini akataka Muswada uonyeshe angalau ramani ya mazingira magumu na alitoa mfano mtu anafanya kazi Sumbawanga haiendi mpaka alikwenda Mombasa. Kwa kweli Watanzania sasa tufikie mahali tubadilike tuone kwamba kama umesomeshwa na kodi za wananchi wa nchi hii, umepata ajira nenda katumikie wananchi popote ulipopangwa na wengi hawa ni woga tu wa kwenda kuanza kufanya kazi. Kuna watu ukiwahamisha kwenda kule Lindi hawataki, wakifika Lindi ukiwahamisha wanagoma na wengine wamestaafu wamenunua mashamba pale Kineng'ene kwenye Jimbo la Mheshimiwa Mohamed Abdulaziz.

Kwa hiyo, ni suala la kwenda tu lakini tukianza kutenga marupurupu kwamba anayekwenda mahali fulani alipwe hivi, watu wa Dar es Saalam watadai na sisi hapa tuna hatari ya majambazi na Arusha tupewe motisha ya namna fulani. Kwa hiyo, tuwatumikie wananchi kwa kadri ya uwezo wetu.

Mheshimiwa Aggrey Mwanri, alizungumzia kulinda maslahi ya wafanyakazi katika sekta binafsi. Kwa mujibu wa Muswada huu kama vifungu vinavyowalinda wafanyakazi. Kwa mfano, sehemu ya pili ya Muswada inayozungumzia haki za msingi za mfanyakazi. Suala la uwezo wa Vyama vya Wafanyakazi la kuleta wafanyakazi katika kujiunga na majadiliano na waajiri tunakubaliana kwamba sekta binafsi wamekamata mpini, wana utaalam wa ku-*organize,* wana utaalamu wa kujadiliana na Muswada huu pamoja na kuwapa nafasi Vyama vya Wafanyakazi, lakini Serikali kwa kushirikiana na *ILO, DANIDA USAID* tumeendelea kufanya mikutano ya kuwahakikisha kwamba Vyama

vyetu hivi vya Wafanyakazi vinaweza kupata nguvu ya kujadiliana na wenzao kutokana na ukweli kwamba waajiri wana wafanyakazi wao na wenyewe Vyama vya Wafanyakazi wanajua hili tumefanya nao Mikutano kwa mfano, pale Arusha, Mbeya, Bagamoyo vya angalau kuwapiga *brush* watokane na kule tulikokuwepo mwanzo kwamba hivi ni vyama vilivyokuwa *affiliated* na Chama Tawala. Sasa hivi mpambano ni wa kweli kweli siyo ule wa kutegemea kwamba kuna Serikali au kuna chama cha kunibeba, Kwa hiyo, tunafanya hilo.

Kifungu cha 1(1)(2)(3) kwamba vifungu hivi vinaonekana kama vinapingana na hii inazungumziwa kwa madhumuni ya ajira ya mtoto. Ajira ya shuruti na ubaguzi havitaruhusiwa kwenye majeshi pia ndiyo maana yake. Hii inayozungumza kwenye kifungu cha 1(1)(2)(3), hii ajira ya kuburuzwa, ajira ya watoto kwenye majeshi yetu vile vile haitoruhusiwa. Sasa kuna watu wanasema lakini kule kwenye Jeshi, mbona kuna amri tu kule kaa chini, amekaa, huko siyo kushurutishwa hapana, ile ni namna ya kufanya kazi ile kwa ufanisi zaidi.

Kifungu cha 4, kutaja sheria ya *Labour Institutions, 2004* ambayo hapa haipo na dada yangu pia alilizungumza. Mnajua hapa tatizo ni la kiutaalamu, sheria hii kwa kawaida ilitakiwa iletwe Muswada mmoja tu wa *Labour Institutions and Labour Standard,* lakini kwa maana ya kuufanya Muswada kusomeka vizuri tulifikiria kutenganisha na ndiyo maana yote tumeiunganisha pamoja. Lakini kingine hakiwezi kuwezekana bila kingine. Sasa tumepata matatizo ya kuku na yai nini kianze, lakini madhumuni yetu kwa kweli ni kwamba Muswada huu kama mtaupitisha leo ili ufanye kazi lazima uwe na *Labour Institutions.*

Sasa tungeanza na ile *Labour Institutions* ndiyo ingekuwa baya zaidi, mnatuletea *Institutions* zifanye nini? Kwa hiyo, ingekuwa kuku na yai nani ameanza, mtatuwia radhi sana kwa hilo nia yetu ilikuwa ni njema.

Mheshimiwa Rosemary Nyerere, anaendelea wafanyakazi wanaotoka nje ya nchi vipi? Tutakujibu baadaye, lakini Muswada uangalie namna ya kutatua migogoro haraka. Suala hili limezingatia katika Muswada katika kifungu cha 86 hadi 95 ambayo kwa kweli inaondoa urasimu ulikuwepo hapo mwanzo.

Kuhusu kuwajibisha Vyama vya Wafanyakazi visivyotimiza wajibu wake, nataka nikuthbitishieni kwamba nia ya Vyama vya Wafanyakazi siku zote ni kuwasaidia wafanyakazi wao maana ndiyo wateja wao, sasa unaweza kukatokea udhaifu wa ubinadamu. Katiba zao kupitia Muswada huu zikishasajiliwa wanayo mamlaka wale wanachama wa kuwajibisha viongozi wao. Lakini nataka niwahakikisheni kwamba siku zote Vyama vya Wafanyakazi nia yao ni kuwasaidia wafanyakazi wao maana ndiyo kuwepo kwao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uhamisho wa wafanyakazi uzingatie maslahi ya familia, hili ni suala la kiutendaji ambalo litazingatia shauri na shauri, mahali fulani na mahali pengine haliwezi kuwa *uniform* kwa maeneo yote kwa hivyo likakaa kwenye Muswada.

Mheshimiwa Zahor Juma Khamis, alizungumzia kuhusu Muswada unatoa mwanya kwa nini tunaajiri watoto wenye umri wa miaka 14 na 17? Inawezekana mtoto mmoja maumbile yake yanaweza kubeba uzito wa tani 80, lakini mwingine akawa na uwezo wa kubeba kilo 80 tu. Sasa kuondoa utata kwa nini tusifute kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumezingatia sana umri wa watoto wetu wanaomaliza Shule za Msingi na ambao hawana nafasi ya kuendelea Sekondari. Wengi wanamaliza kwenye miaka 14, 15 mpaka 16. Kumweka tu mtoto huyu na baba na mama mpaka ndevu zitoke na sauti ibadilike miaka 18 unaweza kuwa ni mzigo mwingine kwa wazazi.

Kwa hiyo, tukasema basi ziwepo zile kazi ambazo mtoto huyu akifanya hatoathirika na ndiyo maana kifungu cha 5(3) Waziri amepewa uwezo wa kutangaza aina ya kazi ambazo zinaweza kuathiri watoto. Kifungu cha 6(1), tutawezaje kudhibiti ajira kulazimisha katika majumba. Muswada wa *Labour Institutions* ambao utafuata, utadhibiti hali hiyo na maelezo yake yako humo.

Kifungu cha 20(1) kazi ya usiku hazitoathiri watoto wanaonyonya. Kwa kweli tulichojitahidi hapa ni kuleta uwiano kati ya mama, mtoto na mwajiri. Katika kifungu cha 20 (2) (b). Tunafikia mahali kule tulikotoka na pengine imechangia hata kufa kwa Mashirika yetu. Mtu anaweza akakaa siku 180 lakini hapo tunafikiria huyu mama anahitaji kufanya kazi. Ana haki yake ya kufanya kazi na yule mtoto ana haki ya kupata maziwa kutokana na pato la mama yake tunapomweka huyu nje ya kazi kwa muda wote huo sio yeye tu anapoteza hata mwajiri wake naye anapoteza haki yake ya *services* za mtumishi wake.

Kwa hiyo, tulichofanya hapa ni kupata uwiano wa wote watatu, mtoto, mama na mwajiri na ndiyo maana kwenye *objectives* Waziri alisema madhumuni ya Muswada huu sio tu kulinda maslahi ya wafanyakazi lakini pamoja vile vile na kuinua kiwango kile cha uchumi au tunaita *productivity* sijui Kiswahili chake

**WAZIRI MKUU:** Tija.

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO:** Nashukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Kifungu cha 31, kupunguza siku za sikukuu za kwenye likizo. Sisi tunaomba ibakie kama ilivyo sasa kwamba siku 28 zinamtosha mfanyakazi kupumzika. Lakini katikati yake kukitokea Sikukuu, Jumamosi na Jumapili tuziondoshe kwa kweli katika hali ya utandawazi sasa hivi tutakuja kupoteza ajira kweli kweli na ndiyo tunawakaribisha wageni ambao hayo mengine kwao si ya muhimu kuchukua nafasi zetu.

Mheshimiwa Zahor Juma Khamis, anauliza kwa nini mjamzito anaonekana kifungu cha 33 ana alama zote kwa nini aombe *medical certificate?*

Kwa kweli tunachozuia hapa ni udanganyifu tu. Wapo wanaodanganya sio kazini tu hata ndani ya majumba. Mimi nina imla hapa niangalie hivi hivi. Anakwenda hospitali anakutwa amefunga matambara kibao. Sasa hakuna matatizo hospitali zipo apimwe ionekane kweli amebakiza miezi mitatu. Wakati mwingine inaweza kuwa ni tambazi tu pengine sio ujauzito. *(Makofi/Kicheko)*

Halafu akauliza swali lingine Mheshimiwa Zahor Juma Khamis, matumizi ya neno *same time* kwa mama aliyezaa mtoto zaidi ya mmoja. Mwingine hujaliwa akazaa mtoto wa kwanza, sasa hivi ikapita saa tatu akazaliwa mwingine ndiyo *same time.* Kwa kweli mantiki inakataa kwamba hata huyu anayezaa wakati ule watoto wote wawili au watatu wanatoka kwa pamoja. Hapana, kuna anayetangulia akafuata mwigine, hawatoki wote. Kwa hiyo, tunaona ibaki ilivyo *same time,* inafahamika wakitoka wote kwa pamoja itakuwa habari kubwa. *(Makofi/Kicheko)*

Kifungu cha 42, msingi ule wa *severance pay* ya siku 7. Hii ifahamike kwamba ni ziada ya malipo ya awali sio kwamba ndiyo malipo yenyewe. Mtu mmoja alisema kwamba mbona tunabadilisha mafao tu kwa hofu hii. Kwa kweli haya ni malipo ya ziada. Usajili wa Vyama kwa nini usubiri miezi sita? Hili Waziri atatoa jibu Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mohamed Missanga, alizungumzia kwa uchungu sana juu ya *Workmen's compensation.* Sheria hii ya fidia itashughulikiwa katika awamu ya pili ya sheria za kazi ile *phase II* yaani *Employment promotion.* Ndiyo maana humu huioni kama ulivyoitarajia.

Mwajiri anayeshindwa kupeleka michango ya wafanyakazi kwa nini apewe *reasonable grounds. Reasonable grounds* hii hapewi kumlinda yeye hapana, itakapofikia shauri hili limefikishwa toka Mahakamani aeleze sasa Mahakama inataka aeleze kwa nini usichukuliwe hatua. Sio yeye anaamua Mahakama inataka kumwuliza yeye hebu tupe kwa nini wewe usichukuliwe hatua kwa kushindwa kufikisha michango ya huyu mtu katika sehemu inayohusika.

Kwa hiyo, hapa ndiyo kama hana *reasonable grounds* Mahakama inamtia hatiani. Lakini huwezi kwenda Mahakamani huyu amenidhulumu pale pale wakasema tu kuanzia sasa hivi wewe una hatia. Sheria kwa kawaida zinakuwa na kinga mle mle ukishindwa kumaliza yote yale kujikinga basi hapo ndiyo inakuwa umechukua kimeo hapo. Mtazamo wa marekebisho ya kumlinda mwajiri badala ya mfanyakazi. Kwa bahati mbaya tulikuwa na uwoga tu kwamba tumeona mabadiliko yamekuja kwa kazi mno kiasi ya kufikiria kwamba Muswada huu unalinda mno haki ya mtumishi kuliko mwajiri. Huku ni kukifanya kivuli cha paka kuwa ni kimvuli cha chui.

Kwa kweli Muswada huu unalinda pande zote mwajiri na mtumishi na ningependa nikuthibitishieni Waheshimiwa Wabunge kupitia kwako Mheshimiwa Naibu Spika, kwamba Serikali hii inaamini kwamba kuwepo kwake ni wafanyakazi wa nchi hii. Kama alivyosema Mheshimiwa Aggrey Mwanri, Serikali hii inaongozwa na Chama cha Mapinduzi na wanachama wake ni pamoja na wafanyakazi na wakulima. Kwa hiyo, hata

siku moja hatuwezi tukageuka tukaanza kula nyama na kunywa damu za wafanyakazi ambao ndio wanachama wetu na wapiga kura wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kupunguza mafao ya mfanyakazi yaliyopo kwenye sheria ya sasa kifungu cha 32(2). Ningependa kulifahamisha Bunge lako Tukufu kwamba hapa madhumuni makubwa ni kulinda uwiano muafaka kati ya maslahi ya mfanyakazi na kukua kwa uchumi wenyewe. Kwa kweli lazima tufanye kazi na wakati ule wa kwamba kiwanda kimezalisha, hakikuzalisha mimi nitapata mshahara wangu, nitakwenda likizo, nitatibiwa sasa umekwisha. Katika sekta binafsi *survivor* ya Kampuni au Shirika ni uzalishaji wake. Kwa hiyo, Muswada huu unalenga kila mmoja kutimiza wajibu wake. Mfanyakazi a-*provide services* na mwajiri a-*provide wages* kwa ajili ya *services* za yule mtu.

Kuhusu likizo ya ugonjwa, gharama zinatakiwa kubebwa na kwa kweli likizo ya ugonjwa na utakapoletwa ule Muswada wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii. Mifuko hii ya Hifadhi ya Jamii inalipwa na Mashirika yanayohusika *NSSF, PPF, LAPF* na kadhalika. Itakapofikia ile utaona kwamba kwa mwajiri maadamu ameshatoa michango yake kule kunakohusika mambo mengine yote yanahama kwake tuje tukamatane wenyewe kwenye mifuko yetu ya jamii.

Mheshimiwa Henry Shekiffu, Sheria ya Ajira ya mwaka 1999 kweli ipo na ilikuwa haijaanza kutumika na baada ya kuja hili wazo la *employment promotion* awamu ya pili ya sheria hizi za kazi tumeamua hii nayo iboreshwe baada ya kukutana na wadau wote ili ifanye kazi pamoja na awamu ile ya pili. Ndiyo maana basi ningependa nijibu kwa mpigo maoni ya Mheshimiwa Mgana Msindai, Mheshimiwa Kheri Khatib Ameir, Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe, Mheshimiwa Semindu Pawa, Mheshimiwa Tembe Nyaburi, Mheshimiwa Phillemon Ndesamburo, Mheshimiwa Rosemary Nyerere na Mheshimiwa Zahor Juma Khamis, yanayohusu ajira ya wageni nchini. Wageni wanaofanya kazi sawa wanazofanya Watanzania na bado wanalipwa sawa sawa. Wawekezaji wanaotumia nafasi ya umaskini wetu kuweka mikataba ya kuleta wafanyakazi kutoka nje hata wasiostahili.

Ningeomba kutoa jibu la ujumla kwamba suala zima la mfumo, sera na sheria ya kuajiri wageni nchini ni mojawapo ya mambo yanayoshughulikiwa katika awamu ya pili ya marekebisho ya sheria za kazi. Zoezi hilo limeanza na mojawapo ya mambo ya kuangalia ni ukuzaji wa ajira, uboreshaji wa stadi za kazi pia suala zima la kuwawezesha Watanzania kupata kazi nje ya nchi katika mfumo huu wa utandawazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimejitahidi kwa kadri ya muda ulivyoniruhusu ninaamini Mheshimiwa mtoa hoja mwenyewe atakuja kukamilisha mle mote ambamo mimi nimeacha. Nakushukuru sana kunipa nafasi hii na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuelezea yale ambayo yameibuliwa na Waheshimiwa Wabunge katika Muswada huu unaoitwa

Ajira na Mawasiliano ya Kikazi wa Mwaka 2003 *(The Employment and Labour Relations Bill, 2003).*

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa jinsi walivyochangia kwa hamu na mantiki kubwa Muswada huu, hii inadhihirisha kwamba kwa kweli Muswada huu ulikuwa unahitajika na umekuja kwa wakati muafaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa niwatambue Waheshimiwa Wabunge ambao wamechangia. Kwanza waliochangia kwa maandishi nao ni Mheshimiwa Semindu Pawa, Mheshimiwa Stephen Kahumbi, Mheshimiwa Tembe Kerenge Nyaburi, Mheshimiwa Herbert James Mntangi, Mheshimiwa Margareth Mkanga, Mheshimiwa Phillemon Ndesamburo na Mheshimiwa Teddy Kasella-Bantu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge ambao wamechangia kwa kuzungumza ni Mheshimiwa Sophia Simba, ambaye vile vile alizungumza kwa niaba ya Kamati ya Maendeleo ya Jamii, Mheshimiwa Khalifa Mohamed Khalifa ambaye alizungumza kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Mgana Msindai, Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe, Mheshimiwa Benedicto Mutungirehi, Mheshimiwa Leonard Derefa, Mheshimiwa Aggrey Mwanri, Mheshimiwa Rosemary Nyerere, Mheshimiwa Margareth Mkanga, Mheshimiwa Leonard Shango, Mheshimiwa Zahor Khamis, Mheshimiwa Mohamed Missanga, Mheshimiwa Henry Shekifu, Mheshimiwa Christopher Wegga, Mheshimiwa Teddy Kasella-Bantu, Mheshimiwa Khadija Kusaga, Mheshimiwa Ludovick Mwananzila na Mheshimiwa Mudhihir Mohamed Mudhihir, Mbunge wa Mchinga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru Kamati ya Maendeleo ya Jamii kwa michango ambayo ilikuwa imekusudia kuboresha zaidi Muswada huu na kama sote tulivyoona yote ambayo walikuwa wamependekeza kwa kweli tumezingatia katika *amendments* ambazo tumeweza kuzileta hapa Bungeni. Mchango wao ambao ulizingatia hasa hasa majadiliano ya utatu yalikuwa ni ya maana na sisi hatukuyapuuza.

Pili, naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Mudhihir Mudhihir, Mbunge wa Mchinga, kwa mchango wake ambao kwa kiasi kikubwa umenisaidia kufafanua baadhi ya hoja za Waheshimiwa Wabunge. Nina hakika kwa jinsi ambavyo alivyoweza kujitahidi kufafanua sasa mashaka mengi yaliyokuwepo yametoweka na nina hakika Waheshimiwa Wabunge tutakwenda pamoja.

Tatu, naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Khalifa Mohamed Khalifa, Msemaji wa Kambi ya Upinzani kwa kuunga mkono hoja hii na pia kwa mawazo yake mazuri. Mengi ambayo Mheshimiwa umeyazungumza nina hakika Mheshimiwa Mudhihir ameyajibu vizuri kutokana na ulivyokuwa umeyapanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya shukrani hizo sasa naomba nijielekeze katika kujibu, kuelelezea na kufafanua baadhi ya hoja za Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, napenda kuwakumbusha kwamba kama nchi au kama Taifa tulishaamua kwamba tubadilishe sera zetu za uchumi katika nchi hii. Sidhani kama

tumekuja hapa kufumua mjadala upya. Tulifanya hivyo kwa hiari yetu wenyewe na wala sio kwa kushinikizwa na mtu, Taifa au Taasisi yoyote kama vile ambavyo watu wengine huwa wanajaribu kupotosha ukweli wa mambo. Sote tuliamua na kwa hiyo tunajua kuwa uchumi wetu sasa unaendeshwa kwa misingi ya uchumi wa soko *(Free Market Economy).* Katika mfumo wa aina hii sekta binafsi inakuwa muhimili wa uchumi.

Mheshimiwa Aggrey Mwanri alipokuwa akichangia, alisema kwa kuwa sera yetu tumeamua iwe hii, basi ni muhimu tukakubali vile vile kwamba zipo sheria, kanuni na taratibu zinazoongoza na zinazosimamia mfumo wa uchumi wa aina hii. Kwa hiyo, hatuwezi kuzigundua zingine ndiyo mazingira ambayo tumekubali twende nayo mapya katika kuboresha uchumi wa nchi yetu katika mwelekeo mpya tulionao, kwa hiyo zipo taratibu, sheria na kanuni ambazo zinabidi kuheshimika.

Kwa hiyo, ningependa kusisitiza tena kwa Waheshimiwa Wabunge kwamba hii ni moja ya sababu kuu za kuleta hizi sheria hapa kwa pamoja na kwamba nyingi zilikuwa zimepitwa na wakati kama nilivyozungumza wakati nilipokuwa nikiiwasilisha hoja hii ya kuleta sheria hii kwamba waajiri, wawekezaji, wafanyakazi, Waheshimiwa Wabunge na wananchi kwa ujumla sote tumekuwa tukiona kwamba sheria hizi zimepitwa na wakati ndiyo maana hizi sheria zimekuja. Lakini msingi wake ni kwa sababu tunataka sasa kwenda na mazingira ya *Free Market Economy,* uchumi wa soko.

Tumekuwa tukijuliza ndani na nje ya Bunge kuwa pamoja na mazingira mazuri ya utulivu na amani ambayo nchi yetu imekuwa nayo muda mrefu mbona ajira haiongezeki.

Waheshimiwa Wabunge, sisi wenyewe huwa ni mahodari sana kila tunapotoa mifano utasikia kwa mfano wenzetu Kenya, Uganda tunataja nchi za jirani hapa kuonyesha jinsi mambo yao yanavyokwenda. *NARC* walipokuwa wanatafuta kuingia Serikalini moja ya vitu walivyozungumza pale ni kuona kwamba sisi mkituchagua tutatengeneza ajira laki tano kwa mwaka. Ilikuwa ni kwa sababu walikuwa wana sheria ambazo wanajua zimeandaa mazingira ambayo yanaendelea kuwavutia wawekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, moja ya vikwazo sugu ambavyo wawekezaji wa sekta binafsi na kwa ujumla wamekuwa wakielezea ni sheria za kazi ambazo zimepitwa na wakati. Ukizungumza na wawekezaji na sekta binafsi wanakwambia kwa kweli Tanzania kwa amani na utulivu hakuna tena katika Bara la Afrika. Kwa kweli Tanzania sera zenu za uchumi *the best,* lakini tatizo lenu ninyi sheria zenu zimepitwa na wakati *they are fake.*

Kwa hiyo, lazima mzibadilishe sheria zifanane na yale mnayokusudia katika sera zifanane na mazingira yenu ya amani, utulivu na mshikamano mlionao ili watu waje wawekeze katika nchi yenu. Turufu tunayo ya amani na utulivu, lakini bila kubadilisha hizi sheria haiwezekani tukavutia wawekezaji na tukaiamsha hata sekta zilizopo ndani ya nchi hii. Watu wanadhani tumeleta sheria hizi eti kujibu hoja au kwa sababu ya shinikizo la uwekezaji. Si kweli, hata sekta yetu binafsi yenyewe hapa ndani ya nchi wanalalamikia sheria yetu kwamba ni kikwazo kinawakwamisha. Tukishalielewa hili inakuwa rahisi kujibu haya yafuatayo:-

Hii ilichangiwa na Mheshimiwa Mohamed Missanga na Mheshimiwa Hadija Kusaga. Anasema kweli wafanyakazi wameshirikishwa lakini mangapi ambayo umeyakubali.

Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wabunge Mheshimiwa Mohamed Missanga, anasema kushirikishwa *is one thing,* lakini tuchukue yale ambayo mlikuwa mnayazungumza *is another thing.*

Mimi nakubaliana na yeye, lakini tukumbuke kwamba tunaendeshwa na kanuni ya utatu na hili ndilo tatizo ambalo tunalo. Tunadhani kwamba Serikali kazi yake daima ni ku-*protect* wafanyakazi hata kama wanaonekana hawastahili kulindwa. Hii ni makosa, tujue kwamba Serikali ni moja katika wale watatu ambao *actually* kazi zake ni *regulate* alikuwa kama *referee.* Mfanyakazi apate haki yake na mwajiri apate haki yake, tukilitambua hilo basi tutakuwa tumepiga hatua.

Tunapokwenda katika majadiliano ya utatu kuna *give and take.* Usidhani yote ambayo wafanyakazi waliyaleta eti yote yakubalike na wenzao Vyama vya Uajiri nao watakuwa na kwao. Sasa katika mjadala ndio tukafika tunasema hili sawa. Nyie waajiri hili sawa tunakubali na nyie wafanyakazi hili tunakubali. Sasa kinachohojiwa hapa ni kwamba yote ambayo yanaletwa wafanyakazi yote yakubalike, hata kama hayaendani na mazingira ya sasa haiwezekani. Hii ndiyo nasema Mheshimiwa Mohamed Missanga hatutaweza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Sheria hizi zinamlinda sana mwajiri na zaidi ya mfanyakazi na hivyo tunavyosema si kweli Mheshimiwa Mohamed Missanga. Najua ulikuwa una-*belong* kwenye Chama cha Wafanyakazi lakini nataka kukuhakikishia kwamba na mimi vile vile ni trade unionist. Tena mwenzio nilipanda vile vile sana nilikuwa *Easternt Zone Representative* wa *RAO.*

Sheria hizi ukiziangalia sawa sawa msingi wake umewekwa katika *documents* ambazo zinalinda haki za binadamu. Kamati maalum ilipoanza kazi zilikubaliana kwamba kwa pamoja kuna haja ya kuangalia upya mambo yaliyotajwa hapo juu pamoja na kwamba kila mtu anatoka katika sekta ya uwakilishi tofauti. Lakini waliamua waongozwe na kile ambacho wataona ni chenye maslahi kwa nchi yao na ndiyo wakabuni kauli mbiu wakasema nchi kabla ya jimbo au *constituency* au *country before constituency.* Pia waliamua kuziandika upya kabisa sheria za kazi badala ya kuziba viraka. Kamati iliamua kuwa katika kupima sera na sheria za sasa za kazi watumie vigezo vya jinsi vinavyokithi matarajio yafuatayo:-

Kwanza, Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hivi Katiba yetu kweli ni Katiba ya kuonea kwamba Katiba inaonea wafanyakazi. Kwa sababu ndio kilikuwa kigezo cha kwanza.

Pili, Katiba ya Umoja wa Afrika *(The African Chart).*

Tatu, mapendekezo mbalimbali toka Mahakama ya Rufaa na Mahakama ya Kazi. Chombo ambacho ndicho kinatafsiri sheria ambazo tunatunga sisi Waheshimiwa Wabunge hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nne, mikataba ya Shirika la Kazi la Dunia au Duniani *(ILO)* iliyoridhiwa na Bunge na inayokusudiwa kuridhiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, msingi wa sheria zote za kazi tunazojadili hapa ni kutoka katika Shirika la Kazi la *ILO*. Sisi tulipotengeneza rasimu ya sheria hizi Muswada huu tuliwapelekea vile vile vile *ILO* wakaleta maoni yao na hayo nayo tutayazingatia kwa kiasi kikubwa. Kwa hiyo, mimi nakataa kwamba Muswada huu eti uko hapa kumlinda tu mwajiri, mfanyakazi hapana. Si kweli mfanyakazi huku tumechukua maoni ya sehemu zote tatu katika utatu wetu.

Vile vile mwelekeo wa uanishaji wa sheria za kazi katika nchi za *SADC* na Afrika Mashariki. Hili nalo si la kupuuza. Hivi juzi Waheshimiwa Marais wetu wametia saini itifaki ya forodha baada ya hapo itifaki ambayo inafuata ni *Free Movement of Persons and Free Movement of Labour*. Kwa hiyo, hizi sheria lazima ziwiane katika nchi zote za Afrika Mashariki na baadaye nchi za *SADC*.

Kwa hiyo, sisi hatuwezi kubaki hapa tukasema aah, tuendelee na utaratibu wetu ule wa zamani wakati wenzetu wanasonga mbele, tutaainishaje sheria hii. Tupende tusipende tutafika mahali lazima kuwe na *Free movement of people, free movement of labour*. Haya nayo lazima tuyajue na wafanyakazi wetu tuwaandae katika mazingira hayo wayajue. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mohamed Missanga, mimi nakuhakikishia kwamba hakuna uonevu wowote na ni mangapi ambayo yamekubaliwa.

Nilipokuwa nazungumza wakati nawasilisha hoja hii nilizungumza jinsi ile Kamati Maalum ilivyofanya kazi. Kwanza ilikuwa Kamati Maalum ika-*commission* watu kwenda kuandika *concept papers* kutoka wataalam mbalimbali wanaojua sheria. Akaja na M-*consultant* kutoka Afrika ya Kusini ambaye ni mtaalamu wa *Labour Law II* naye akaandika makala zake. Wakayajadili yale lakini ili wayafanyie *justice* wakaunda *technical committee* kuyajadili hayo. Ndani ya Kamati Maalum *(Task Force)* nadhani hii *technical committee (TUKTA)* walikuwemo. Tumezungumza nao na wakayaona hayo. Tumetoka pale tumekwenda kwenye *Public Hearing*. Tumefanya vikao katika Mikoa mbalimbali, maeneo ambayo tunaamini kwamba wako waajiri wengi na viko viwanda vingi. Michango imetolewa, Vyama vya Wafanyakazi vilikuwepo, watu binafsi walikuwepo. *NGOs* zilikuwepo uwazi gani zaidi ya hapo unahitaji Mheshimiwa Mohamed Missanga. Tumejitahidi sana.

Lakini vile vile baada ya hapo wakarudi tena Dar es Salaam wakakaa kama Kamati wakayachambua. Baada ya hapo ikatungwa Miswada nikaleta hapa ukasomwa kwa mara ya kwanza ukaleta mazungumzo makubwa sana nchini. Tukarudi tukakaa *special seminar* Morogoro na makundi yote matatu ya wadau husika. Vyama vyote vya Wafanyakazi, ninaambiwa nivitaje kimoja kimoja ningeweza kuvitaja sasa na watu binafsi walikuwepo walikuwa zaidi ya watu mia mbili pale, walikuja. Wameshiriki na

wametoa michango yao wakatoa mapendekezo ikabidi Serikali ikae tena kuangalia katika yale ambayo mapendekezo ambayo wameleta wameweza wakayachukua yapi bila kuathiri utatu wetu, tukayachukua. Kwa hiyo, ukichukua tangu mwanzo wa zoezi mpaka kufikia hapa zaidi ya nusu ya mapendekezo kutoka Vyama vya Wafanyakazi yamekubaliwa katika Muswada huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, narudia tena kwamba kwa mazingira tuliyonayo ya mfumo mpya wa uchumi, utandawazi na ushirikiano wa Kijumuia kati ya Afrika Mashariki na *SADC* wafanyakazi wetu lazima wajipange upya, wafanyakazi wajue kuwa haki bila wajibu ni kuliangamiza Taifa. Wajue vile vile kwamba kuendelea kusisitiza kupumzika badala ya kuzalisha kutawakimbiza wawekezaji wetu wengi na hata sekta binafsi iliyomo katika nchi itadumaa na hii italetwa mazingira mabaya zaidi kwa sababu ajira itaendelea kudumaa na kupungua zaidi.

Kwa hiyo, ndugu zanguni kila mwaka tunapokaa hapa makundi makubwa ya vijana yanaingia katika soko la ajira. Kwanza wapo wanaomaliza Shule ya Msingi zaidi ya laki tano, wako wanaomaliza Sekondari, wako wanaomaliza Vyuo Vikuu bila kuandaa mazingira ambayo yatazalisha ajira mpya tutaendelea kung'ang'ania ajira zile zile za zamani eti kwa sababu ya ukiritimba ule tuliokuwa tumeuzoea wa zamani tutafika mahali itahatarisha hata amani ya nchi kwa Waheshimiwa Wabunge na Waheshimiwa na wafanyakazi.

Ninawaomba kabisa kwamba hii tuliyoyaleta hapa ni kwa faida yetu sisi kama Watanzania na kwa faida ya nchi. Sasa hii kudai eti mfumo wa uchumi wa soko unafurahia sana makundi makubwa ya watu kutokuwa na kazi. Hili nalo lilielezwa na Mheshimiwa Mohamed Missanga kwamba bwana suala la mfumo tulionao sasa waajiri wanafurahi kuwa na makundi makubwa kule nje na kwa hiyo bila kujali kwamba hii inahatarisha amani. Nataka nikuhakikishie kwamba mfumo wa uchumi wa soko unachohitaji ni kutengeneza faida ili watengeneze kazi nyingi zaidi ili waweze kuajiri watu wengi zaidi. Kwa sababu ingekuwa hivyo unayoyasema kwamba ndio kweli tuchukue bepari mkubwa ni Marekani hapa lakini agenda kubwa ya uchaguzi ni *unemployment.* Tuchukue Uingereza *agenda* kubwa ya uchaguzi ni *unemployment.* Tuchukue Ujerumani *agenda* kubwa ya uchaguzi ni *unemployment.*

Kwa hiyo, nataka nikuhakikishie kwamba katika mfumo huu *the problem of unemployment* imo ndani. Kwa hiyo, mimi nawahakikishia Waheshimiwa Wabunge kwamba si kweli kwamba sheria hizi zimeletwa hapa kwa sababu ya lengo la kumkandamiza mfanyakazi na kumpendelea mwajiri hapana. Ninachotaka kujua ni kwamba tumeleta sheria ambazo kama zikizingatiwa vizuri na zikisimamiwa vizuri zitakuza ajira na zitalinda haki na maslahi ya wafanyakazi wenye kuwajibika.

Mheshimiwa Naibu Spika, mengi haya yalikuwa ni haya ya jumla yanayogusa sera, lakini mengi yale ambayo ya kifungu kimoja kimoja Mheshimiwa Naibu Waziri ameshayajibu. Labda niende kwenye lile moja alilokuwa amebakiza nalo ni la Vyama vya Wafanyakazi kusubiri miezi sita kusajiliwa, hatusemi visubiri miezi sita. Tunasema tunavipa miezi sita viwe vimekwishasajiliwa, vinginevyo basi vimeshindwa ku-*exist.*

Kwa hiyo, chama kama kitakuwa tayari ndani ya mwezi mmoja kitasajiliwa. Chama kama kitakuwa tayari ndani ya miezi miwili kitasajiliwa. Ila tumetoa *a maximum of six months* kwamba chama hicho kiwe kimeshafika mahali kimepata *submission of membership* ya kuweza kuwa-*operate* pale mahali pa kazi.

Mengine ambayo yamezungumzwa ni hawa ambao waliochangia jioni hii, tukianza na Mheshimiwa Henry Shekiffu. Anasema elimu itolewe kwa wananchi, tena hili limeguswa na Mheshimiwa Hadija Kusaga vile vile. Ni kweli katika baada ya Miswada hii kupita hatua inayofuata ni *penalisation* ya sheria zile za kazi. Ili uweze ku-*pressurised* lazima basi namna ambazo zinaanza kutekelezwa. Ili uanze kuzitekeleza lazima uende kutoa elimu kwa wahusika wadau wote. Vyama vya Waajiri na Vyama vya Wafanyakazi. Lakini vile vile suala la elimu ni suala la endelevu. Mimi nategemea vile vile kwamba Vyama vya Wafanyakazi navyo vitajizatiti katika kuelimisha wanachama wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, zamani Vyama vya Wafanyakazi tulikuwa tuna utaratibu wa kupeana kutoa semina kwa kupelekwa kozi. Mimi nakumbuka nilishakwenda mpaka Afrika ya Kusini kwenda kusomea baadhi ya taratibu za namna ya kuendesha chama cha wafanyakazi. Sasa nitashangaa kama jukumu hili sasa hivi halipo eti naambiwa tu Serikali peke yake ndiyo ifanye.

Kwa hiyo, mimi nina hakika kama tukifanya sisi wote waajiri wafanye, Vyama vya Wafanyakazi vifanye na Serikali kwa kushirikiana na Mashirika ya Kimataifa hasa Shirika la Kazi la Dunia tukifanya sisi wote, hili suala la elimu litasambaa kwa kasi kubwa zaidi na wafanyakazi na waajiri watajua majukumu yao katika sheria hii mpya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wameajiriwa miaka zaidi ya miwili lakini bado wanaendelea kuhesabika vibarua. Mheshimiwa Shekiffu, sheria ukiisoma sawa sawa inasema hata ule utaratibu wa kusema leo unaniita Juma Kapuya miezi mitatu unanifuta unaniita Juma Masanja, baada ya hapo nikibadilisha jina ninakuwa John Nani. Katika sheria *as long as* ni sura ile ile baada ya miezi sita unalazimika wewe mwajiri kumuhesabu kwamba ni mfanyakazi wa *of unspecified contract period. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuajiri mfanyakazi wa miaka 14 majumbani ndio wengi. Sasa hili kwanza tunategemea *moral conscious* yako itakukataza kuajiri katoto kidogo. Kwa sababu unajua sheria zinakataza. Lakini la pili tunaimarisha kaguzi zetu za ndani ya majumba na ndani ya viwanda. Kwa hiyo, tutawakamateni tu. Najua na wengine tuko humu humu lakini mimi nina hakika tutawakamateni tukikamilisha kaguzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Jumuiya ya Afrika ya Mashariki, utandawazi wafanyakazi wetu wamejiandaa vipi kutokana na ukiritimba kuajiriwa.

Hili nimeshalizungumza nilipokuwa nikitoa mambo ya jumla hapa. Ni kweli wafanyakazi wetu wanahitaji kujiandaa vizuri. Kujiandaa kwa maana ya kwanza kusema kwamba sheria zilizokuwepo hazitawafikia wawekezaji.

Lakini la pili kujua kwamba na wao wabadilike katika utendaji wao wa kazi. Kama tutaendelea kuwa ni wafanyakazi ambao tunatambulika kwa kulalamika tu nina hakika waajiri watakuja katika nchi hii wataanzisha ajira lakini watakuwa wanawakwepa Watanzania kujua kwamba hawa ni tatizo. Ukimweka katika kiwanda mmoja tu ni tatizo. Kwa hiyo, hili nalo naomba wafanyakazi wetu walijue.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitakupa mfano kuna Benki moja ya kigeni iko hapa, alikuja Meneja wake kunitembelea. Akaniambia Mheshimiwa Waziri, mimi nimekuja kukutembelea. Unajua nchi hii mna wafanyakazi wa ajabu sana.

Mimi nimeweka *local supervisors, local supervisors* hawa wanashindwa kuwa-*reprimand* wafanyakazi walioko chini yao kwa kuogopa sijui mlikuwa na vipengele vya zamani mnasema kiongozi asiwe mkaripiaji, asiwe mnyapara, sasa mimi nimewaambia wao wasipowa-*reprimand,* nitawa-*reprimand* mimi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa haya ndiyo mazingira mapya, ile *altitude* yetu *there must be a change of mindset* ya kazi, tubadilike ndugu zanguni, bila kubadilika kwa kweli tutaangamia. Lakini baada ya hapo Serikali nayo sasa iandae namna ambavyo inaweza ikatoa mafunzo ya elimu ya ufundi stadi kwa wafanyakazi hawa ili waendane na teknolojia zinazohitajika hivi sasa. *(Makofi)*

Ni kweli baadhi ya makampuni yanalalamika kuhusu mafundi stadi kama alivyozungumza Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe pale, kwamba ufundi stadi bado kidogo uko chini. Lakini ukizungumza na watu wa migodi wameridhika sana na *level* ya mafundi wetu, wamechukulia kama *threshold.* Wakiwachukua wakiwapa mafunzo kidogo tayari wamekuwepo katika uzalishaji mpya huu. Kwa hiyo, nataka kuwahakikishia kwamba tunajitahidi kubadilisha hata mitaala ya ufundi stadi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la kiingereza ni kweli, waajiri wengi wanakuja kulalamika ofisini kwangu wanasema kwamba: *"Your people cannot communicate."*

Katika suala hili ndiyo maana mnamuona Waziri wa Elimu anakuwa mbogo anapoambiwa eti sasa tuanze kufundisha kwa Kiswahili tangu shule ya msingi mpaka *University.* Hicho hicho *broken* kinatusaidia kidogo, sasa tukishakataa kabisa si ndiyo tatizo! Si bora tuwe na hicho hicho cha kuvunja vunja angalau kidogo tutapata nafuu kuliko kukikataa kabisa! Ninachoomba ni kwamba, tumsaidie Waziri wa Elimu kung'ang'ania dhana hii na aimarishe mafunzo ya Kiingereza ili tuweze kushindana, hatuna *choice.* *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Christopher Wegga, anasema mtu anaambiwa: "Kama hutaki mshahara wangu mdogo basi nenda kalime." Watu wanadharau sana kilimo.

Mheshimiwa Wegga, nadhani wewe una umri wa kuweza kukumbuka mambo ya kikoloni, hizi ni *legacy* za ukoloni kwa sababu wakoloni walipokuja kitu cha kwanza walichofanya ni kuhakikisha kwamba tunadharau tamaduni zetu, kwamba kucheza ngoma ya Mwinamila ni ushenzi, hilo la kwanza.

Lakini la pili, wakatufanya tuamini kwamba kazi za mikono si kazi za mtu aliyestaarabika, lakini kwao kule kazi za mikono zina thamani kubwa sana. Sasa suala si kazi za kilimo tu, ni kazi zote za mikono. Kijana wa leo ukimwambia nenda kafanye kazi za mikono anaona wewe umemuangamiza, umemlaani na tuna tatizo hata katika ku-*define* ajira ni nini. Sasa nataka nikuhakikishie kwamba, kwa msimamo wa Serikali kilimo ni kazi kama kazi zingine zozote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mishahara ya wageni, hiyo nadhani tumeshazungumza katika Muswada huu jinsi ambavyo tunapiga marufuku ubaguzi wa mishahara kutokana na *national origin.* Najua ni eneo gumu, lakini madhali sheria ipo, Vyama vya Wafanyakazi vikikaa imara na sisi tuhakikishe kwamba tunasimamia sheria inawezekana. Lakini tatizo ni kwamba wale wale wanaoajiriwa huwa hawataki hata kuzungumza, ukimuendea anakwambia: "Bwana wewe niache unanifuatafuata nini, kwanza nikija Serikalini unanipa kidogo zaidi, hapa si afadhali."

Ni kweli, Mheshimiwa Tembe Nyaburi aliyechangia ametoa mfano wa *Geologist* mmoja aliyeko *East African Goldmine,* ule mgodi wa Nyamongo. Anasema yuko *Geologist* Mtanzania kasoma sawa sawa na yule mtu wa kutoka Canada analipwa shilingi 900,000/=, lakini yule wa Canada analipwa kati ya dola 4,000 mpaka dola 6,000. Hayo ndiyo mambo ambayo tumekusudia kuyaondoa katika Muswada huu, kama sheria itapita itawabana wale. Yapo mambo ambayo kama mgeni atastahili kupata, hayo huwezi ukayapinga, lakini yapo yale ya kawaida kwamba hivi kweli *gross salary* inapishana kiasi hicho, kama ni posho si zinajulikana? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo limeguswa na hisia za watu wengi sana ni *court fee.* Serikali inajua kwamba hii *Industrial Court* tuliyonayo sasa *actually* ilikuwa katika mfumo wa *tribunal.* Sasa tunakwenda tunaihamisha kutoka mfumo wa *tribunal* inakwenda kuwa sehemu ya Mahakama Kuu ya Tanzania *(The Department of The High Court).*

Waheshimiwa Wabunge, kutokana na hoja zenu Serikali imekubali kwamba itaweka kipengele katika Muswada huu kumuomba *Chief Justice* atengeneze kanuni itakayokuwa inahakikisha kwamba masuala yanayohusu kazi yasitozwe ada, hiyo Serikali imekubali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu vifaa vya kutendea kazi, ni kweli popote utakapokwenda hivi sasa wafanyakazi hawapati vifaa vya kutendea kazi. Kwa mfano,

mtu anaweza kuwa anafagia barabarani kuna vumbi anahitaji *mask* hapati. Lakini nataka niwahakikishieni kwamba, tutakapoanza kuimarisha kaguzi zetu za kazi, tutakapoimarisha kitengo chetu cha *Constitutional Offence Safety Agency,* nataka niwahakikishieni kwamba makosa haya yatasahihihswa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Teddy Kasella-Bantu umezungumza kuhusu kufukuzwa kwa ajili ya ulemavu, kipengele cha 40. Nimesoma kipengele hicho sioni kama kinazungumzia kumfukuza mtu kwa ajili ya ulemavu, badala yake kinalinda watu wote pamoja na watu wenye ulemavu na tumeweka kipengele maalum kabisa kuhakikisha kwamba hakuna *diestrumation* kwa misingi ya ulemavu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu *maternity leave,* tumezungumza kabisa *maternity leave* iwe ni ya miezi miwili. Kuhusu likizo ya ugonjwa, ndugu zanguni haya mambo ya likizo ya ugonjwa, ya matibabu tukisisitiza sana pamoja na hili suala la *domicile* ambalo Mheshimiwa Naibu Waziri ameshalitolea maelezo, tunachoogopa hapa ni kwamba tunaweza tukajikuta mahali tukaweka mazingira ya kutisha kwa waajiri na wawekezaji na Sekta binafsi. Lakini vile vile, kwa sababu umeshaingia katika mfumo huu wa uchumi wa soko, mambo haya si sehemu ya sheria hii, ni sehemu ya *social security* na hiyo inakuja katika *phase II* ambayo itakuwa inazungumzia *employment promotion.*

*Social security is the one of the articles,* tutaleta hapa kuizungumzia upya ili iweze ku-*take care* au iweze kutilia maanani matatizo ya wafanyakazi wanapokuwa wanaumwa, matatizo ya wafanyakazi wanapokuwa wamefiwa au wamefariki. Hayo yote itakuwa ni sehemu ya *social security,* si sehemu ya mwajiri, mwajiri akishalipa *social security* na wewe ukishalipa *social security* mmemalizana, anachokuja kuzungumza mwajiri na wewe ni siku ngapi ambazo utahitaji kwenda, kwenda kuzika au kusafirisha au kufanya vitu vingine kama hivyo. Hapa hatuzungumzii watu wa ugonjwa wa Ukimwi, hapana. Watu wa ugonjwa wa Ukimwi kama bado ana afya ya kufanya kazi tumesema asibaguliwe, sheria haikutaja Ukimwi, lakini tumezungumza mambo ya afya, ila tumesema apewe kazi inayofanana na afya yake. Sasa, sheria imeweka bayana mambo haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile, Mheshimiwa Teddy Kasella-Bantu alizungumza juu ya *filing fee.* Mheshimiwa Ludovick Mwananzila alizungumza kuhusu ubaguzi wa kikabila. Pia, alizungumza kwamba Muswada huu unawasaidia sana wawekezaji. Nimeishaeleza kwamba si kweli, bali unawasaidia wawekezaji pamoja na sekta binafsi ya kwetu wenyewe ndani ya nchi ambao ni waajiri wa hapa hapa walikuwa wanalalamika kwamba sheria zilizopo kwa kweli zimepitwa na wakati na wafanyakazi pia walikuwa wanalalamika kwamba zimepitwa na wakati. Wafanyakazi walikuwa wanalenga zaidi katika *compensation* ambayo nimeshasema kwamba katika awamu ya pili ambayo tayari tumeishaanza kuifanyia kazi itakuja Bungeni hapa baada ya muda si mrefu.

Baada ya maelezo hayo nina hakika kwa kiasi kikubwa tumegusia yale yote ambayo yalikuwa yamekusudiwa. Kama yapo ambayo tumeyaruka nataka

kuwahakikishieni kwamba sisi tumeyachukua, tutayafanyia kazi na kuhakikisha kwamba mahusiano ya kikazi yanakuwa ni mahusiano ambayo yanaashiria kukuza uchumi na kuongeza tija na kulinda maslahi ya wafanyakazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Pili)*

## KAMATI YA BUNGE ZIMA

### Muswada wa Sheria ya Ajira na Mahusiano katika Kazi wa Mwaka 2003 *(The Employment and Labour Relations Bill, 2003)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kama mnavyouona huu Muswada ni mrefu kwa hiyo, tunakusudia kufanya kwa sehemu ili tuumalize. Lakini hii isikuzuie kusimama wakati ambapo unaona una jambo la kusema. Katibu endelea.

Ibara ya 1

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 2

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nikushukuru sana kwa jinsi unavyoongoza shughuli za Bunge na hususan katika Kamati yako ya Bunge Zima. Nimesimama ili kwamba Kamati yako ikubali kufanya rekebisho moja la msingi sana katika Ibara ya 2 (1), ambayo inahusu *application.*

Ni ya mstari wa pili inasomeka: "... itatumika kwa Watumishi wa Serikali ya Tanzania. Endelea kusema: *"The Government of Tanzania Mainland."* Sasa inaonekana kama kuna Serikali ya *Tanzania Mainland* ambayo siyo sahihi kwa muundo wetu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, napendekeza katika ya neno Tanzania na neno *Mainland* tuingize maneno *in Tanzania.* Kwa hiyo, litasomeka: *"Those in the public service of the Government of Tanzania in Tanzania Mainland"* halafu inaendelea. Kwa hiyo, itakuwa imeleta sasa dhana nzima ya mfumo wetu kwamba Muungano wetu ni wa Serikali mbili na suala la mambo ya kazi siyo ya Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana.

**MHE. DR MASUMBUKO R. M. LAMWAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni kuboresha tu, siyo kubadilisha hayo maudhui ya hayo mapendekezo. Sasa kama ni kuongeza *in Tanzania Mainland...*

**MWENYEKITI:** Unazungumzia kifungu kile kile alichokitaja *AG?*

**MHE. DR MASUMBUKO R. M. LAMWAI:** Ndiyo hicho hicho. Kabla hatujakipitisha, labda tu kurekebisha kuwa na lafudhi nzuri tu iwe: *"The Government of the United Republic of Tanzania in Tanzania Mainland."* Namshauri Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali awe *specific.*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa *AG,* una upinzani na hilo?

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Sina *objection* yoyote, nakubali. Itakuwa: "... na Serikali ya Jamhuri ya Muungano."

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo, marekebisho hapa yatakuwa kama yale yaliyosomwa na Mheshimiwa Dr. Lamwai. *(Makofi)*

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 3
Ibara ya 4
Ibara ya 5
Ibara ya 6

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 7

**MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesikiliza maelezo ya Mheshimiwa Naibu Waziri katika kifungu cha 7 sehemu ya 4(b) ukisoma kifungu chenyewe: *"No employer shall discriminate, directly or indirectly, against an employee, in any employment policy," that's the real issue "in any employment policy or practice on any of the following grounds."*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu msingi wenyewe ni *employment policy* ninashauri kwamba, kifungu 4 (b) kifutwe. Ili kutoa maudhui kwamba watu wanaotajwa hapa ni Watanzania na kwa sababu hiyo hakuna haja ya neno hili *nationality* ili kuondoa dhana kabisa kwamba sisi tuna nchi ambayo haibagui watu wanaotafuta kazi kutoka nchi zingine. Sisi kama Taifa tutaajiri watu wa nje tu kama tunawahitaji na kama kuna makubaliano na mwekezaji ambayo ni *specific.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kifungu hicho ili nisisimame tena nashauri pia kwamba, sehemu (c) ibadilishwe iseme: *"Tribe or place of origin in Tanzania."* Kwa sababu ilivyo hivi pia inafungua mlango kwamba mtu yeyote kutoka mahali popote kwenye dunia anaweza kuja na asibaguliwe katika kutafuta kazi katika nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu (e) nashauri ifutwe kwa sababu baada ya kutobagua mtu kwa rangi yake, kabila lake na mahali anapotoka Tanzania, *race* na dini, hakuna tena sababu ya kuongelea *national extraction* wakati tunamuongelea Mtanzania. Nadhani vifungu vyote hivi vitatu vinatoa mwanya kwa wageni ambao hawastahiki kupewa kazi. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nilikuwa nauliza hapa kama Katibu alipokea mapendekezo kutoka kwako yanayotaka vifungu hivyo vifutwe, ameniambia hajapokea. Kwa sababu mambo hayo ni ya msingi na ingepaswa ulete mapema ni tofauti na ile ambayo kila mtu anajua hii ni *United Republic* na ile kila mtu anajua ni *obvious.* Sasa haya kwa sababu ni ya msingi pengine ungeleta mapema, ndiyo maana nimeuliza kama walipata au kama hawakupata. Kwa hiyo, hayakubaliki kuna utaratibu wake.

**MHE. HENRY D. SHEKIFFU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha *discrimination,* kifungu cha 7 kifungu kidogo cha 6 (c), ninachotaka tu ni kauli ya Serikali au kauli ya Waziri.

Wakati nilipokuwa ninachangia nilieleza jinsi inavyotokea kutokana na sheria ya kuajiri Watanzania haitaitwa *discrimination,* lakini pale wanapoajiriwa Watanzania. Nilikuwa nimeeleza kwamba kuna kazi ambazo zinapaswa kufanywa na Watanzania na bado vibali vinaonekana vinatolewa, sasa Waziri hajatoa kauli katika hili, hawa watu vibali hivi wanavipata wapi? Je, anaruhusu niombe Bunge lako tuunde Tume ichunguze mambo haya kwa undani? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kutoa maneno yafuatayo ya ufafanuzi.

Kwanza suala la kibali cha mfanyakazi wa kutoka nje limegawanywa katika maeneo mawili. Kuna lile la wawekezaji ambao wanakuwa na *quarter* maalum kupitia *TIC,* lakini lipo vile vile la hawa *Class B* ambao wanaomba kupitia kwa Wizara inayohusika na si suala tu la Wizara ya Mambo ya Ndani kwa maana ya Idara ya Uhamiaji na Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo peke yake. Kama huyu mtumishi anaangukia kwenye Wizara labda ya Viwanda na Biashara, inaanzia huko inakuja kwenye Wizara yetu tuone kama kweli hiyo Wizara inamuhitaji huyo mtu, hakuna mwingine wa namna hiyo?

Lakini vile vile, wakati tunatoa maelezo hapa wakati tunachangia hoja tulieleza kwamba masuala mazima ya ajira za wageni au watu kutoka nje ya nchi yetu yatashughulikwia kikamilifu katika *Employment Promotion Bill* ambayo ni sehemu ya

pili ya Muswada huu ambao tunauzungumzia hivi leo yaani hatua ya pili. Kwa hiyo, tulitoa maelezo haya na mimi ninaamini pengine alikuwa hayumo ndani.

**MHE. HENRY D. SHEKIFFU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sijaridhika kwa sababu bado wapo watu wanafanya kazi pale Dar es Salaam na nilitoa mfano wanauza maduka, tena wapo wanaonekana na ukienda hata leo maduka yapo yanaendeshwa na Wachina sijui na watu wengine, wanatengeneza redio, hawa watu hivi vibali vya kufanya hizo kazi wanavipata wapi, hawapitii Wizara hii? Kama haamini, basi tuunde Tume ili ikaliangalie hili na watoe taarifa. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda tena kurudia yale yale kwamba, Muswada huu tulionao hauzungumzii, hauna kipengele kinachozungumzia juu ya *permits* iwe *Class B* au *Class A* ya wale watu wanaokuja.

Suala hili zima tutaliweka katika ule Muswada utakaofuata, lakini kwa humu ndani sioni, Mheshimiwa sijui anazungumzia kipengele gani katika hili eneo, labda angetutajia pengine tungeweza kuwa na nafasi nzuri zaidi ya kumpa ufafanuzi anaoutaka.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

**MHE. HENRY D. SHEKIFFU:** Mheshimiwa Mwenyekiti ...

**MWENYEKITI:** Imeshapita bwana, ahadi umepewa kuna Muswada unakuja kwa hiyo jiandae vizuri zaidi.

Ibara ya 8
Ibara ya 9
Ibara ya 10
Ibara ya 11

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 12
Ibara ya 13

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 14

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 15
Ibara ya 16
Ibara ya 17
Ibara ya 18
Ibara ya 19
Ibara ya 20
Ibara ya 21
Ibara ya 22
Ibara ya 23
Ibara ya 24

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 25

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 26

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 27

**MHE. LEONARD N. DEREFA:** Mheshimiwa Missanga.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Derefa, mimi niko mbele naona zaidi kote huko. *(Kicheko)*

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi hii.

Kwa sababu kifungu hiki kina mambo matatu ambayo nataka kuyazungumza naomba niruhusiwe kueleza yote matatu, ni kifungu hicho hicho.

Kwanza kwenye ukurasa wa 74 kifungu cha 27 niliomba maelezo kwamba tatizo lililopo ni kwamba, pale ambapo kiwanda kinafilisika wafanyakazi madai yao hawalipwi mpaka mwisho kabisa baada ya wadai wote kumalizika na kama kuna bakaa, chochote kama kitakuwepo ndiyo wanapewa.

Sasa sikupata maelezo na kama Muswada huu umezingatia tatizo hilo ambalo ni kubwa sana na wafanyakazi wengi katika viwanda hivi ambavyo vinabinafsishwa wamekosa chochote.

**MWENYEKITI:** Mtoa hoja hajapata ni kifungu gani unazungumzia.

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA:** Kifungu cha 27.

**MWENYEKITI:** 27.

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA:** Ndiyo, lakini kama hicho sicho, basi aniambie ni kifungu gani ambacho suala hilo lipo, kwa sababu nilieleza katika mchango wangu mapema kabisa kwamba hicho kifungu 27 au aje afafanue ni kifungu gani ambacho kina-*take into consideration* tatizo hilo ambalo nimelieleza.

Halafu la pili, pamoja na maelezo mazuri ya Naibu Waziri na Waziri Profesa, ameonyesha uprofesa wake leo katika kueleza, lile suala la *Sea Cliff* nilisema hivi kweli katika kuboresha sheria hata kile ambacho tayari mfanyakazi anacho unamnyang'anya hivi ni sawa sawa kweli? Kwa sababu sheria ya sasa inasema likizo *with full pay* ya ugonjwa miezi sita. Likizo *half pay* miezi sita, ndivyo ilivyo sasa. Sasa, hata kile ambacho tayari mfanyakazi anacho unamnyang'anya hivi kweli ni *justification?*

Tunawawakilisha watu, hawa watu tunaowawakilisha huko nje, tukitoka huku tunakwenda kuambiwa: "Ninyi mmekwenda kutuondolea hata kile ambacho tayari tunacho!" Tutawaambia nini? *(Makofi)*

Halafu pili, miezi 12 halafu ukafanya siku 126 uwiano wake hata haueleweki! Ni kigezo gani ambacho Serikali imetumia katika kuzipunguza siku zile kutoka siku 180 mpaka siku 126?

Pamoja na nia nzuri ya kuwavutia wawekezaji, lakini nadhani hapa kuna kasoro. Halafu suala la ugonjwa hakuna mtu anayeomba. *Operation* kwa mfano, mgonjwa anachukua *operation* miezi 9 au miezi 12. *Operation* za akinamama hawa zinachukua muda mrefu au mguu umevunjika *operation* inachukua muda mrefu sana. Tafsiri yake ni kwamba, ukiumia ukafanyiwa *operation* au ukivunjika mguu ikifika tu siku zako 126 wewe nenda zako. Sasa huu utakuwa ubinadamu kweli? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu ni pale ukurasa wa 85 kifungu cha 40 kifungu kidogo cha tatu nilisema: "Pale ambapo Mahakama au msuluhishi ameshaamua kwamba Missanga arudi kazini, hivi ni kwa nini tena huyo mwajiri anatoa uwezo wa kuamua nirudi au nisirudi?" Haina uhusiano na mambo ya uwekezaji haya au ya kuvutia mtaji!

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwamba nilikosa nikapelekwa mahakamani, vinginevyo basi hata haja ya kumpeleka mtu mahakamani hakuna kwa sababu tayari nina *powers* za kum-*dismiss* huyu mtu. Sasa kama kaenda mahakamani karudishwa, leo tunachompa fursa ya kwamba aamue kumrudisha au kutomrudisha mimi siielewi hii. Kwa hiyo, naomba nipate maelezo juu ya hiyo kitu. *(Makofi)*

**WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu kinachohusu *bankruptcy* ukiangalia kwenye

marekebisho ule ukurasa wa kwanza, kifungu (e) panasema: *"In clause 28 by relieving sub clause 6."* Kwa hiyo, unaitafuta *sub clause 6* ambayo iko pale. Hayo ndiyo maneno ambayo yana-*define* haki za mfanyakazi wakati Kampuni inapofilisika.

**MWENYEKITI:** Bado mengi hujajibu, *leave* ya ugonjwa na nini.

**WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO:** Hilo la kwanza. La pili kuhusu likizo ya ugonjwa, ni kweli kwamba zamani tulikuwa tuna miezi sita *full pay,* miezi sita nusu mshahara.

Lakini tukumbuke kwamba mazingira haya yenye kupenda kupumzika ndiyo ambayo yametusababishia baadhi ya mashirika yetu kufilisika, ndiyo maana nikasema: "Jamani sheria tunazotengeneza hivi sasa ni sheria ambazo zinaleta uwiano kati ya kukuza uchumi na haki za wafanyakazi na maslahi ya wafanyakazi." *(Makofi)*

Tukiendelea kusisitiza haki tu tutarudi kule kule ambako tunaanzisha makampuni mengi yanafilisika, yanakwama kwa sababu mazingira hayo yatakuwa kazi yake ni kutibu tu basi. Ni kweli kabisa *under exception services* anazogungumza Mheshimiwa Missanga kama mtu anapata *fracture* ambayo labda itahitaji zaidi ya miezi sita, hayo ni masuala ambayo yanaweza yakawekwa katika mikataba ya hiari yakazungumzwa. Lakini vile vile nimesema kwamba, hata hii wala hatuna haja ya kusuguana vichwa sana, ni suala la kati ya miezi mitatu mpaka mitano tunaleta sheria hapa kuyahamisha yote haya kwenda kwenye *social security.* Kwa hiyo, hii tunayoizungumza ni *transition period* tu, kwamba tutakapokuja kwenye Bunge lingine kama siyo Oktoba labda Januari mwaka kesho tunaleta Muswada mwingine hapa wa kuhamisha yote haya yaende kwenye *social security.* Sasa mwajiri hapo anakuwa kaondokana kabisa na utaratibu mwingine. Hizo ndiyo taratibu zinazo-*govern* aina hii ya uchumi, hatuko tena kwenye misingi ya kuwa tuna-*overload* wafanyakazi, tuna-*overload privileges* kuliko uzalishaji. *(Makofi)*

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, moja la mwisho, naomba alirudie Mheshimiwa Mwenyekiti.

**MWENYEKITI:** Hebu lirudie moja la mwisho.

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA:** Kwamba Mahakama ikishaamua kwamba mahakama ikishaamua arudishwe kazini vipi tena mwajiri anatoa hiyari ya kumrudisha wakati Mahakama na *in fact* Mahakama hiyo hiyo katika katika kifungu cha 40(1) (c) ina fursa pale ya kuamua kumfidia mfanyakazi miezi kumi na mbili. Tayari tuli-*provide* katika sheria sasa unapomwambia tena mara ya pili *duplication* mahakama iliona kwamba huyu hakuna kesi ya msingi ya kumfanya huyu alipwe fidia au aachishwe kazi, kumnyima mtu ajira maana yake ni kumnyima mtu haki ya kibinadamu.

**MWENYEKITI:**Mheshimiwa mtoa hoja, *AG,* unataka kusema?

**WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi wote ni Watanzania tunazungumza mazingira halisi,

mazingira halisi ni kwamba kesi inaweza ikachukua miaka miwili, mitatu. Kwa mtu anayezalisha kuendelea kuitunza nafasi ile kwa muda wa miaka miwili, mitatu, minne, mitano, *is none realistic.* Inawezekana kabisa kuwa *by the time* kesi inakuja kuisha huyu bwana kesha ajiri mtu mwingine katika nafasi ile. Haiwezekani awe na watu wawili wanafanya kazi ile ile. Sasa kwa sababu kosa lilikuwa ni lake ndiyo maana tumempa adhabu angalau basi amfidie huyu mtu kwa mishahra wa miezi kumi na mbili.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 28

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 29
Ibara ya 30
Ibara ya 31
Ibara ya 32
Ibara ya 33
Ibara ya 34
Ibara ya 35
Ibara ya 36

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 37
Ibara ya 38

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 39
Ibara ya 40
Ibara ya 41
Ibara ya 42

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 43
Ibara ya 44

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 45
Ibara ya 46
Ibara ya 47
Ibara ya 48
Ibara ya 49
Ibara ya 50
Ibara ya 51
Ibara ya 52
Ibara ya 53

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 54

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 55
Ibara ya 56
Ibara ya 57
Ibara ya 58

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 59

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 60
Ibara ya 61

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 62
Ibara ya 63
Ibara ya 64
Ibara ya 65

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 66

Ibara ya 67
Ibara ya 68
Ibara ya 69
Ibara ya 70
Ibara ya 71
Ibara ya 72
Ibara ya 73
Ibara ya 74

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 75
Ibara ya 76
Ibara ya 77
Ibara ya 78
Ibara ya 79
Ibara ya 80
Ibara ya 81
Ibara ya 82
Ibara ya 83
Ibara ya 84
Ibara ya 85

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 86
Ibara ya 87
Ibara ya 88
Ibara ya 89
Ibara ya 90
Ibara ya 91
Ibara ya 92
Ibara ya 93
Ibara ya 94
Ibara ya 95

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 96
Ibara ya 97
Ibara ya 98
Ibara ya 99
Ibara ya 100

Ibara ya 101

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 102

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Jedwali la 1

*(Jedwali lililotajwa hapo juu lilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Jedwali la 2
Jedwali la 3

*(Majedwali yaliyotajwa hapo juu yalipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

*(Bunge lilirudia)*

**(Muswada wa Sheria ya Ajira na Mahusiano Katika Kazi wa 2003**
***(The Employment and Labour Relations Bill, 2003)***

*(Kusomwa mara ya Tatu)*

**WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ya Bunge Zima imeupitia Muswada huu wa *The Employment Labour Relations Bill, 2003* na kuukubali pamoja na mabadiliko yaliyofanywa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa Muswada huu wa Ajira na Mahusiano katika Kazi wa mwaka 2003 sasa ukubaliwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria wa Serikali Ulisomwa Mara ya Tatu na Kupitishwa)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tumefika hapo umeona umechukua muda kwa sababu katika hatua hii lazima asome *title* ile ndefu kama inavyotakiwa ndiyo maana amechukua muda mrefu. Muda uliobaki hauwezi kumruhusu Waziri kusoma hotuba inayofuata.

Sasa kabla sijaahirisha naomba tu niseme lile ambalo pengine Profesa Jumanne Maghembe, nilimwambia angelileta mapema ni rahisi sana kufanya mabadiliko katika kutunga sheria, mradi unatoa ile taarifa mapema kwa Katibu na ile taarifa yako itakwenda kwa Serikali ili wakati tunakuja hapa katika hatua ya Kamati wote wana habari kwa hiyo uta-*move* ile kwamba unataka marekebisho fulani na hiyo ni rahisi sana na ile ukisema tu wana *knockout* kwa hiyo, ningependa turudie tena kuzisoma zile Kanuni ni rahisi sana kuendelea vizuri.

Sasa baada ya maelezo hayo sasa naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 01.36 usiku Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Alhamisi, Tarehe 15 Aprili, 2004 Saa 3.00 asubuhi)*